
# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Sita




Taasisi ya Elimu Tanzania

Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Sita

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI**
**NA TEKNOLOJIA**

*Cheti cha Ithibati*

Na. 560

Jina la Chapisho: Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-335-9

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Sita katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

**Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa**
Kamishna wa Elimu

FOR ONLINE USE ONLY

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019
Toleo la Pili 2021

ISBN: 978 - 9987 - 09 - 335 - 9

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

Simu: +255735041170/+255735041168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

Utangulizi ........................................................................................ v
Shukurani ........................................................................................ vi

**Sura ya Kwanza**
Kuwapenda watu wengine katika familia ............................................. 1

**Sura ya Pili**
Kujivunia shule na kuipenda nchi yetu ............................................. 13

**Sura ya Tatu**
Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .............. 18

**Sura ya Nne**
Demokrasia ........................................................................................ 32

**Sura ya Tano**
Kujali watu wengine ........................................................................... 47

**Sura ya Sita**
Kutunza mazingira ............................................................................. 60

**Sura ya Saba**
Kujenga uhusiano mwema na wenzako ............................................. 67

**Sura ya Nane**
Kuwa mwajibikaji na kulinda rasilimali za umma ............................... 79

**Sura ya Tisa**
Kusimamia majukumu ......................................................................... 92

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 3 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi**
Kutii sheria na kanuni ........................................................................115

**Sura ya Kumi na Moja**
Nidhamu binafsi ................................................................................ 125

**Sura ya Kumi na Mbili**
Kuvumilia katika maisha ................................................................... 140

**Sura ya Kumi na Tatu**
Kujifunza mambo kiyakinifu ............................................................... 147

**Sura ya Kumi na Nne**
Kuaminika katika jamii ....................................................................... 154

**Sura ya Kumi na Tano**
Kusimamia haki za binadamu............................................................. 163

**Sura ya Kumi na Sita**
Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine....................................... 173

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 4 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha nne katika mfululizo wa vitabu vitano vya somo la Uraia na Maadili kuanzia Darasa la Tatu hadi la Saba. Kitabu hiki cha Mwanafunzi Darasa la Sita kimeandaliwa kulingana na Muhtasari na Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundisha somo la Uraia na Maadili wa mwaka 2016, ambao umezingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi. Maudhui yaliyomo katika kitabu hiki ni mwendelezo wa yale yaliyomo katika kitabu cha Uraia na Maadili Darasa la Tano. Maandalizi ya kitabu hiki, yamezingatia mwenendo na matarajio ya nchi yetu ya Tanzania katika kukujenga uweze kuheshimu na kuithamini jamii yako, kuwa mwajibikaji na kuwa mstahimilivu. Kitabu hiki kina sura kumi na sita na kila sura imeundwa na vipengele kadhaa. Maudhui ya sura za kitabu hiki yamejengwa kwa njia ya matini, mazungumzo, visa, habari, michoro na picha. Kila sura ina mazoezi na kazi za kufanya mwanafunzi. Pia, ufafanuzi wa msamiati umetolewa mwishoni mwa kila sura ili kukusaidia kuelewa kwa urahisi zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa Kitabu hiki cha Mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

**Waandishi:** Mwl. Musa T. Mwalutanile, Mwl. Davies J. Mlay, Mwl. Godlove E. Siara na Mwl. Beatus. B. Mapunda

**Wahariri:** Prof. Willy Komba, Dkt. Rafiki Yohana, Dkt. Chediel R. Nyirenda (Mwenyekiti wa jopo la uhariri wa maudhui) na Bw. Ambrose F. Mghanga (Lugha - BAKITA)

**Msanifu**: Bi. Rehema H. Maganga

**Wachoraji:** Alama Art and Media Production Limited

**Waratibu:** Mwl. Edna M. Mathew na Mwl. Castor A. Lyuma

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kuchapisha kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 6 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kuwapenda watu wengine katika familia

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza vitendo vinavyoonesha upendo kwa watu wenye mahitaji maalumu kama vile watu wenye ulemavu wa ngozi na miguu. Katika sura hii, utajifunza dhana ya familia, mahitaji mbalimbali ya familia, vitendo vya kusaidia wanafamilia wenye mahitaji maalumu ambao ni watoto wadogo, wazee na wenye ulemavu. Vilevile, utajifunza kuthamini mchango wa wanafamilia katika maendeleo ya familia yenu, kuonesha vitendo vya heshima katika familia na kutenda vitendo vya kuwalinda wanafamilia kutokana na vikundi hatarishi. Umahiri huu utakuwezesha kutoa msaada kwa wahitaji mbalimbali katika familia na nje ya familia, kushirikiana na wengine katika kutoa huduma (msaada). Aidha, utaweza kuihamasisha jamii kuthamini mchango wa wengine bila kujali jinsi zao katika utekelezaji wa majukumu ya familia.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Dhana ya familia

Familia ni kundi la watu wenye uhusiano wa kinasaba yaani wazazi na watoto. Wakati mwingine familia huhusisha watoto wanaoasiliwa. Kwa kawaida familia huwa na baba na mama wanaowalea watoto wao kwa pamoja. Hata hivyo, zipo sababu ambazo huweza kufanya familia iwe na mzazi mmoja kati ya mama au baba. Pia, familia inaweza kuwa tandaa ikijumuisha watu wengine wenye uhusiano wa kindugu wanaotokana na ukoo mmoja. Ndugu hawa wanaweza kuwa bibi na babu wa pande zote mbili, ndugu wa baba kama vile shangazi na baba wadogo, baba wakubwa, ndugu wa mama, mfano, mjomba na mama wadogo, mama wakubwa pamoja na watoto wao.

### Mahitaji mbalimbali ya wanafamilia

Kila mwanafamilia anayo nafasi ya pekee katika familia. Tukitaka kujenga familia iliyo bora, tunao wajibu wa kutambua nafasi ya kila mwanafamilia.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wazazi na walezi wana nafasi ya pekee kama viongozi wakuu wa familia. Watoto wana wajibu wa kufuata maelekezo ya wazazi na walezi wao. Pia, ni muhimu kutambua kuwa kila mwanafamilia kwa nafasi yake anahitaji kupendwa, kusikilizwa na kuheshimiwa. Unapompenda mwanafamilia unamfanya ajisikie kuwa sehemu ya familia, hali ambayo huchangia kukuza ushirikiano katika familia.

Pamoja na mahitaji hayo ya kawaida, yapo mahitaji maalumu kwa wanafamilia wenye ulemavu wa viungo, uoni, uziwi, akili na ngozi. Pia, yapo mahitaji kwa wanafamilia wenye magonjwa, matatizo yatokanayo na uzee, na wanafamilia wenye mahitaji maalumu ya kitabia. Vilevile, watoto wadogo katika familia huhitaji uangalizi wa karibu. Hata hivyo, mahitaji haya maalumu ya wanafamilia hayawafanyi wakose haki zao kama sehemu ya familia. Tunao wajibu wa kuwapenda na kutoa misaada kwa kila mwenye uhitaji ili kuwawezesha kumudu maisha yao ya kila siku kwa furaha.

**Vitendo vya kusaidia wanafamilia wenye mahitaji maalumu:** Wanafamilia wenye mahitaji maalumu wanahitaji msaada wa vifaa na mazingira yanayowasaidia kumudu maisha yao. Misaada tunayoweza kuwapa wanafamilia wenye uhitaji ni pamoja na kubaini kile wanachokihitaji, kuwatia moyo na kuwasaidia kufanya kile wanachoshindwa kufanya bila msaada wa mtu mwingine. Yapo makundi mbalimbali ya wanafamilia wenye mahitaji maalumu. Makundi hayo ni kama yafuatavyo:

***(a) Watoto wadogo:*** Watoto wadogo wasaidiwe kujimudu na vilevile wafundishwe taratibu na namna ya kujihudumia wenyewe. Kwa mfano, waogeshwe, wavushwe barabara na tuhakikishe kuwa mazingira wanayochezea ni salama.

***(b) Wazee:*** Kundi la wazee wasiojiweza huhitaji kusaidiwa. Kundi hili linaweza kusaidiwa kubeba mizigo, kusaidiwa kazi, kufuliwa nguo, kuandaliwa chakula na kuhakikisha wanapata mahitaji yao ya msingi.

***(c) Wenye ulemavu:*** Wafamilia wenye ulemavu wasaidiwe kuweza kumudu maisha yao kama wanafamilia wengine. Kwa mfano, mwanafamilia mwenye ulemavu wa macho asaidiwe kuyaelewa mazingira anayoishi. Mazingira hayo ni kama vile, sehemu ya kulia chakula, kulala, kusomea, maliwato, na kuchezea.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 2 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia Kielelezo namba 1, kisha jibu maswali yanayofuata.



**Kielelezo namba 1:** Vitendo vya kusaidia watu wenye mahitaji maalumu

## Zoezi la 1


1. Chunguza Kielelezo namba 1, kisha mtambue mtu mwenye mahitaji maalumu.
2. Je, ni msaada gani unaotolewa katika kielelezo hicho?
3. Je, umejifunza nini katika kielelezo hicho?
4. Ni vitendo gani huwa unavitenda kuwasaidia wanafamilia wenye mahitaji maalumu?
5. Unawashauri nini wanafunzi wenzako wasiopenda kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu?



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 3 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa kuona katika shule yenu. Andika nukuu za mjadala wenu katika daftari lako la mazoezi.

**Kuthamini mchango wa wanafamilia wengine katika ustawi wa familia:** Kwa kuzingatia uhusiano baina ya wanafamilia, familia zinaweza kugawanywa katika makundi mawili makubwa ambayo ni familia zilizo na maelewano na familia zisizo na maelewano.

***Familia zilizo na maelewano:*** Familia hizi zina sifa ya kuwa na mawasiliano mazuri baina ya wanafamilia. Ili familia ziwe na maelewano, ni muhimu wanafamilia kutambua na kuthamini mchango na mahitaji ya kila mwanafamilia.

***Familia zisizo na maelewano:*** Familia hizi huundwa na wanafamilia wasiosikilizana na kuheshimiana. Hali ya kutokuelewana inaweza kusababishwa na wanafamilia kushindwa kuthamini mchango wa wengine, kutokutambua mahitaji ya kila mmoja na tabia ya kutanguliza mahitaji binafsi dhidi ya mahitaji ya wengine.

Hata hivyo, kila familia inaweza kuwa na maelewano na mwanafamilia yeyote anaweza kuwa chanzo cha ustawi wa familia ikiwa atatambua wajibu wake na kuheshimu mchango wa wanafamilia wengine. Kwa mfano, watoto wanao wajibu wa kutambua kazi kubwa ya kimalezi inayofanywa na wazazi au walezi wao. Watoto wenye tabia njema hutambua kuwa hata kama hawapati mahitaji yao yote, bado wazazi wao wana wajibu wa kuhakikisha kuwa familia inapata mahitaji yake ya msingi kama vile malazi, mavazi, chakula, matibabu na elimu.

Pia, watoto nao wana jukumu la kushiriki kikamilifu kufanya shughuli za kila siku nyumbani kulingana na umri wao. Shughuli hizi ni kama vile kuangalia usalama wa wadogo wao, kufanya usafi wa nyumba na mazingira, kufua nguo, kuchota maji, kwenda sokoni au dukani na kutii maagizo yanayotolewa na wazazi, walezi au watu wengine. Watoto wasaidie wazazi baada ya muda wa masomo au katika siku za mapumziko.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 4 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia Kielelezo namba 2, kisha jibu maswali yanayofuata.




**Kielelezo namba 2:** Kutambua mchango wa wanafamilia wengine katika familia


## Zoezi la 2

1. Je, ni kitendo gani kinachofanywa na mwanaume aliyebeba mtoto katika Kielelezo namba 2?
2. Je, kitendo anachokifanya mwanaume aliyebeba mtoto kinakufundisha nini?
3. Ni kitendo gani kingine kinafanywa na mwanaume tofauti na huyo aliyebeba mtoto katika Kielelezo namba 2?
4. Utawashauri nini wanafamilia kutokana na vitendo vinavyooneshwa katika Kielelezo namba 2?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kuthamini mchango wa kila mwanafamilia katika kuwasaidia wanafamilia wenye mahitaji maalumu. Andika nukuu za mjadala wenu katika daftari lako la mazoezi.

**Vitendo vya heshima katika familia:** Heshima ni hali ya kutambua utu wa mtu mwingine kwa kumjali, kumpenda, kuthamini mawazo yake na kumstahi pale anapokosea. Vitendo vya heshima humwezesha mtu kuishi vizuri na wanafamilia wengine. Baadhi ya vitendo hivyo ni pamoja na kuzungumza kwa kutumia kauli zinazofaa, kusalimia wanafamilia kwa nidhamu, kutosengenya watu, kuomba msamaha unapokosea na kushukuru unapopatiwa huduma au msaada. Heshima huanza kwa mtu kujiheshimu mwenyewe kwanza. Tunapaswa kujiheshimu kwa kufanya mambo mbalimbali. Baadhi ya mambo hayo ni kuvaa kwa staha, kuwa na nidhamu, kuwa msikivu na kusamehe unapokosewa.

Watu wote bila kujali nafasi na hadhi zao katika jamii wanastahili heshima sawa na si vyema kuwabagua watu kwa hali zao. Unapomheshimu mtu mwingine unamfanya na yeye akuheshimu.

### Zoezi la 3

1. Ni vitendo gani ambavyo ukivifanya shuleni vitakujengea heshima katika familia?
2. Ni muda gani tunapaswa kutenda vitendo vya heshima katika familia?
3. Je, ni kwa nini watu wote wanastahili kupewa heshima?


FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 6 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 3


Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu mambo matano mliyoyafanya na yakawaletea heshima katika familia. Andika mambo mliyojadiliana katika daftari lako la mazoezi.

**Kuwalinda wanafamilia dhidi ya vikundi hatarishi:** Katika jamii, wapo watu wasio na maadili wanaoweza kuhatarisha ustawi wa familia bora. Watu hawa, kwa tabia zao, huumiza hisia za watu wengine, huonesha mfano mbaya katika mienendo yao na wakati mwingine wanaweza kudhuru afya za watu wengine. Miongoni mwa watu hao ni wale wanaouza na kutumia dawa za kulevya, wezi, mafisadi na wabakaji. Vilevile, kundi hili linahusisha watu wanaodhalilisha watoto kingono, watu wanaowafanyisha watoto kazi kinyume na sheria na watu wanaonyanyasa wazee na wanajamii wenye mahitaji maalumu. Watu hawa wanaweza kuwa jirani zetu, na wengine wanaweza kuwa wapo ndani ya familia zetu. Wajibu wetu kama jamii ni kuhakikisha tunajilinda, tunawalinda watoto, wazee na wanajamii wenye mahitaji maalumu dhidi ya makundi haya hatarishi.

***Kuwalinda watoto:*** Mambo yanayohusu haki na ustawi wa mtoto yameelezwa vyema katika sheria ya mtoto namba 13 ya mwaka 2009 na tafsiri yake ya mwaka 2014. Kwa mujibu wa sheria hii wajibu wa mtoto ni:

(a) Kufanya kazi kwa ajili ya mshikamano wa familia;
(b) Kuwaheshimu wazazi, walezi, wakubwa wake na watu wazima muda wote na kuwasaidia pale inapohitajika;
(c) Kuhudumia jamii yake na taifa lake kwa uwezo wake wote kimwili na kiakili kadri ya umri na uwezo wake;
(d) Kutunza na kuimarisha mshikamano wa jamii na taifa; na
(e) Kutunza na kuimarisha mambo mema katika utamaduni wa jamii na taifa kwa ujumla katika uhusiano na wanajamii au taifa.

Pamoja na wajibu huu, sheria pia inaeleza haki mbalimbali za mtoto, mojawapo ya haki hizo ni kulindwa dhidi ya kuteswa na kudhalilishwa kijinsi. Watoto wasipolindwa na kupewa uangalizi wa karibu wanaweza kujiingiza au kudhurika na makundi hatarishi katika jamii. Hivyo ni wajibu wa kila mwanajamii kuwalinda watoto dhidi ya watu wasio na maadili. Pia watoto wana wajibu wa kujilinda dhidi ya vikundi hatarishi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 7 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wajibu wa kila mtoto katika jamii ni:

(a) *Kujilinda:* Kwa kuepuka kuiga tabia zilizo kinyume na maadili yetu hata kama tabia hizo zinafanywa na watu tunaowaamini;

(b) *Kuchukua tahadhari unapokuwa nje ya familia yenu:* Mojawapo ya tahadhari ni kuongozana na watu wenye maadili wanaoweza kukusaidia unapokutana na hatari; na

(c) *Kutoa taarifa:* Toa taarifa unapofanyiwa vitendo vya kikatili. Mfano, kupigwa, kuchomwa na maji ya moto, kukatwa na vitu vyenye ncha kali. Vilevile, toa taarifa unapoguswa sehemu za siri au kudhalilishwa kingono.

Kwa upande mwingine, ili kuhakikisha usalama wa watoto, serikali ina wajibu wa kutengeneza mifumo ya kushughulikia vikundi hatarishi. Pia, ina wajibu wa kuhakikisha kuwa hatua kali za kisheria zinachukuliwa dhidi ya vikundi hivyo.

## Zoezi la 4

1. Taja wajibu wa mtoto kama unavyoelezwa katika sheria ya mtoto ya mwaka 2009.
2. Eleza madhara matatu ya vikundi hatarishi yanayoweza kujitokeza katika familia.
3. Je, unapaswa kufanya nini ili kujiepusha na kuwaepusha watu wengine kutojiingiza katika vikundi hatarishi?

FOR ONLINE USE ONLY

## Kazi ya kufanya namba 4

Uliza wazazi au walezi wako kuhusu namna ya kukabiliana na vikundi hatarishi. Andika maelezo yao katika daftari lako la mazoezi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 8 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

**A:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

1. Watu wote katika familia wana mahitaji yanayofanana.______________
2. Watu wenye mahitaji maalumu wanahitaji kujiangalia wenyewe._________
3. Mtoto hana haki ya kulindwa. _____________
4. Mahitaji ya wanafamilia yanaweza kutofautiana lakini watu wenye mahitaji maalumu wana mahitaji yanayofanana.____________
5. Kuomba msamaha kwa wanafamilia tuliowakosea ni mojawapo ya vitendo vya heshima.
6. Watoto hawawezi kuwa na tabia hatarishi._______________

**B:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

7. Zifuatazo ni tabia za kuwapenda watu wengine isipokuwa:
   (a) kumsaidia mwanafamilia anayeumwa
   (b) kuwashukuru wengine wanapotusaidia
   (c) kushirikiana na watu wenye tabia hatarishi
   (d) kuamkia wakubwa kwa wadogo

8. Yatupasa tufanye nini ili tuweze kuishi vyema na watu wenye asili tofauti?
   (a) kupinga mila na desturi zao
   (b) kuwatenga katika jamii
   (c) kuheshimu utamaduni wao
   (d) kuwabagua kutokana na rangi zao

9. Kipi kati ya vifuatavyo si kitendo cha heshima?
   (a) kulewa pombe
   (b) kusalimia wakubwa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) kuvaa kwa staha
(d) kuwapenda watu wote

10. Zifuatazo ni njia za kujiepusha na vikundi hatarishi isipokuwa:
(a) kujiepusha na vikundi hivyo
(b) kushirikiana navyo
(c) kutoa taarifa ya vitendo vyao kwa wanaohusika
(d) kujiepusha na matumizi ya pombe na dawa za kulevya

11. Mojawapo ya vitendo vifuatavyo si vya kawaida kwa mila na desturi za Mtanzania:
(a) watoto kuwaheshimu watu wazima
(b) watoto kuwakaripia watu wazima
(c) watoto kuwasaidia wazee kubeba mizigo
(d) watoto kuwasalimia watu wazima

12. Vitendo vya heshima humwezesha mtu:
(a) kuwabagua walemavu na wazee kijinsi
(b) kuishi vizuri na wanafamilia
(c) kutothaminiwa na jamii
(d) kuleta vurugu katika jamii

13. Ni jambo gani kati ya yafuatayo hufanywa na jamii inayojiheshimu?
(a) kusaidia watu wenye mahitaji maalumu
(b) kukemea watu wenye tabia hatarishi
(c) kudharau mila na desturi za watu wengine
(d) kubagua watu wa kuwasaidia

14. Vitendo gani kati ya hivi vinaweza kujenga tabia hatarishi?
(a) kulewa pombe na kucheza kamari
(b) kushiriki michezo na watu wenye asili tofauti
(c) kuiga mila na desturi zinazofaa
(d) kuheshimu wakubwa na wadogo

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 10 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

15. Lipi miongoni mwa mambo haya utalifanya ili kuwalinda watu wengine kutokana na vikundi hatarishi?
    (a) kuwaelimisha na kuwapa tahadhari
    (b) kuwaruhusu kuchangamana nao
    (c) kuwaonesha wenzako vitendo vya chuki
    (d) kushirikiana na wasio na maadili

16. Ipi kati ya hizi ni sifa ya wanafunzi wenye heshima shuleni?
    (a) hukataa kutumwa na walimu
    (b) hutii wazazi, walezi, walimu na wanafunzi wenzao
    (c) hupiga kelele na kucheza darasani
    (d) hujihusisha na magenge ya wahuni

17. Zipi ni athari za vikundi hatarishi katika jamii tunamoishi?
    (a) kuimarisha ulinzi na usalama
    (b) kusababisha hofu, vurugu na vifo katika jamii
    (c) kusaidia familia kupata mahitaji ya msingi
    (d) kusimamia mgawanyo wa kazi

18. Je, ni nani mwenye jukumu la kuwasaidia watu wenye uhitaji?
    (a) serikali pekee
    (b) serikali na watu wote katika jamii
    (c) wanafamilia husika tu
    (d) Rais wa nchi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 11 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** *Katika jedwali lifuatalo, oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na kipengele kutoka **Sehemu B,** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| ***Hatari kwa wanafamilia*** | ***Tahadhari za kuchukua*** |
| 19. Vikundi hatarishi | (a) kutenganisha malazi ya wavulana na wasichana |
| 20. Watoto wa kike na wa kiume kulala chumba kimoja | (b) kuwa na mpenzi |
| 21. Kutembea peke yako usiku | (c) kutoshiriki ngono |
| 22. Kuvaa nguo zisizo na heshima | (d) kuchagua marafiki wanaofaa |
| 23. Mimba za utotoni | (e) kuvaa kanzu |
| | (f) kuongozana na watu wenye maadili |
| | (g) kuzingatia amri ya uvaaji nadhifu |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Familia tandaa | mkusanyiko wa watu kadhaa wanaohusiana kinasaba, ikianzia na babu na bibi wa upande wa baba na mama, ndugu wa pande zote yaani shangazi, mjomba, binamu na wapwa |
| Tandaa | enea kila pahali |
| Nasaba | uhusiano wa uzao mmoja wa watu kutoka kizazi hadi kizazi |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 12 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Kujivunia shule na kuipenda nchi yetu

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kuhusu kujipenda na kujivunia shule yako kwa kuijua nembo ya shule yako na kufanya kazi mbalimbali za kujitolea shuleni. Pia, ulijifunza umuhimu wa kuenzi tunu za taifa letu, ambazo ni lugha ya Kiswahili, uzalendo, umoja, uwajibikaji, upendo, heshima na utu. Vilevile, ulijifunza alama za utambulisho wa taifa letu pamoja na sikukuu za kitaifa. Katika sura hii, utabaini ujumbe uliomo katika kaulimbiu na wimbo wa shule yako. Vilevile, utajifunza juu ya mambo yanayoiletea sifa shule yako na njia zinazoweza kutumika kuitangaza shule yako. Aidha, utajifunza kuipenda nchi yako kwa kubaini njia mbalimbali za kuitangaza nchi yetu Tanzania. Umahiri huu utakuwezesha kujenga uzalendo wa shule yako, kuithamini, kuipenda, kujali na kuzingatia yanayofundishwa katika shule yako na kulinda rasilimali za shule yako. Vilevile, utakuwezesha kuithamini nchi yako na kutangaza sifa zake ndani na nje ya nchi.*

### Kujivunia shule yako

Zipo njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa kuonesha hali ya kujivunia shule yako. Baadhi ya njia hizo ni kuitangaza kaulimbiu ya shule, kufahamu na kuimba wimbo wa shule yako, kutunga ngonjera, mashairi na nyimbo za kusifia shule yako.

### Kaulimbiu ya shule

Kila shule inayo kaulimbiu ambayo hutumika kama kichocheo cha wanafunzi wanapokuwa shuleni na hata wanapomaliza shule. Kaulimbiu ya shule hujengwa na msemo mfupi wenye mantiki kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi kujifunza kwa bidii ili kufikia maono ya shule. Vilevile, kaulimbiu ya shule huwahamasisha walimu na jumuiya nzima ya shule kufanya kazi kwa bidii na kufikia malengo ya shule. Mara nyingi, kaulimbiu ya shule huandikwa kwenye nembo ya shule au kwenye kibao ili kuitambulisha shule. Pia, kaulimbiu katika baadhi ya shule huimbwa kwenye wimbo wa shule. Aidha, zipo baadhi ya shule ambazo wanafunzi hutamka kaulimbiu ya shule kabla ya kusalimia wakubwa na walimu ama kuuliza swali katika vikao



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mbalimbali vya shule. Mfano wa kaulimbiu mbalimbali za shule ni: Elimu ni Ufunguo wa Maisha, Elimu ni Mwanga wa Maisha, Elimu ni Urithi wa Watoto, Elimu ni Kazi, Hekima ni Uhuru, Juhudi na Nidhamu.

**Umuhimu wa kaulimbiu ya shule:** Kaulimbiu ya shule ni kauli inayotolewa na shule kwa lengo la kuleta hamasa kwa wanafunzi katika kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Hamasa hiyo husaidia kufikia malengo ya kitaaluma na kinidhamu ya shule husika.

### Zoezi la 1

1. Taja kaulimbiu iliyopo katika nembo ya shule yako.
2. Eleza umuhimu wa ujumbe uliopo katika kaulimbiu ya shule yako.
3. Ni jambo gani ambalo unajivunia katika shule yako?

### Kazi ya kufanya namba 1

Chora nembo ya shule yako na kisha andika kaulimbiu ya shule yako katika daftari lako la mazoezi.

### Wimbo wa shule

Wimbo wa shule ni utambulisho wa shule husika. Kila shule inapaswa kuwa na wimbo wake. Wimbo huo huimbwa katika siku maalumu iliyopangwa na shule husika. Aghalabu wimbo huo huambatana na Wimbo wa Taifa, Tanzania, Tanzania Nakupenda na Tazama Ramani.

**Umuhimu wa wimbo wa shule:** Wimbo wa shule unahimiza wanafunzi:

(a) Kusoma kwa bidii ili kufikia malengo yao kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla;
(b) Kutunza mazingira ya shule;
(c) Kushiriki katika michezo;
(d) Kuwa na tabia njema;
(e) Kujenga uzalendo kwa shule yao na taifa; na
(f) Kukumbuka wajibu wao wa kuipenda na kulinda rasilimali za shule na taifa.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 14 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mambo yanayoweza kuiletea sifa shule na njia zinazoweza kutumika kuitangaza shule yako

Yapo mambo mbalimbali yanayoweza kuiletea sifa shule yako. Baadhi ya mambo hayo ni:

(a) **Nidhamu ya wanafunzi:** Shule yenye wanafunzi wenye nidhamu husifika kwa jamii. Mara nyingi wazazi hupenda kupeleka watoto wao kwenye shule ambayo wanafunzi wake wana nidhamu, heshima na adabu;

(b) **Ufaulu wa wanafunzi:** Wazazi hupendelea kuwapeleka watoto wao kwenye shule ambayo wanafunzi wake hufanya vyema kimasomo;

(c) **Mazingira safi ya kujifunzia:** Mazingira mazuri na safi ya kujifunzia huiletea shule sifa nzuri. Hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa shule yako ina mazingira safi na salama ya kujifunzia;

(d) **Kufanya vizuri katika mashindano ya shughuli zisizokuwa za kitaaluma:** Shule husifika kutokana na kuongoza au kufanya vyema katika michezo mbalimbali mfano mpira wa miguu, mpira wa pete, mchezo wa kuogelea, kukimbia na kuruka juu; na

(e) **Mwonekano wa wanafunzi:** Mwonekano wa nje wa wanafunzi mfano usafi wa mavazi huiletea shule sifa.

Zipo njia mbalimbali zinazoweza kutumika kuitangaza shule. Baadhi ya njia hizo ni kutunga nyimbo, ngonjera na mashairi ya kuisifia shule yako.

#### Zoezi la 2

1. Andika wimbo wa shule yako.
2. Wimbo wa shule yako huimbwa wakati gani?
3. Taja faida mbili za kuwa na wimbo wa shule.
4. Eleza ujumbe uliopo katika wimbo wa shule yako.

#### Kazi ya kufanya namba 2

Tunga shairi linaloweza kutumika kuitangaza shule yako. Andika shairi hilo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuipenda nchi yetu

Kuna njia mbalimbali zinazoweza kutumika kuonesha hali ya kuipenda na kuithamini nchi yetu. Miongoni mwa njia hizo ni kuitangaza Tanzania kupitia nyanja mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 15 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) **Kijamii:** Tanzania inajitangaza kwa kuandaa michezo ya kitaifa na kushiriki michezo mbalimbali kikanda na kimataifa. Michezo hiyo ni kama vile, michezo ya Jumuiya ya Madola, Olimpiki, michezo ya kimataifa ya mpira wa miguu na pete, ngumi za kulipwa na michezo ya majeshi katika mataifa ya Afrika. Halikadhalika, kuwepo kwa kumbi kubwa za kisasa za mikutano ya kimataifa kumechangia kwa namna moja au nyingine kuitangaza Tanzania kimataifa. Kwa mfano, upo Ukumbi wa Mwalimu J.K. Nyerere wa Dar es Salaam na Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha. Kumbi hizi hutumiwa na mataifa mbalimbali kufanya mikutano yao na hivyo kuitangaza nchi yetu kimataifa. Vilevile, kuwepo kwa uwanja wa taifa wa michezo wenye kiwango cha kimataifa jijini Dar es Salaam kumesaidia kuitangaza Tanzania kimataifa. Kwa mfano, mwaka 2019 mashindano ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana wa chini ya umri wa miaka kumi na saba yalifanyika katika uwanja huo, na kutangazwa moja kwa moja kupitia vituo vya runinga vya kitaifa na kimataifa.

(b) **Kisiasa:** Tanzania imefanikiwa kujitangaza kimataifa baada ya kujiunga na jumuiya mbalimbali za kimataifa kama vile, Jumuiya ya Madola, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Pia, Tanzania inaendelea kujitangaza nchi za nje kwa kufungua ofisi za ubalozi katika nchi mbalimbali kama vile Kenya, Uganda, Marekani, Kuba, Malawi, Angola na nchi zingine nyingi.

(c) **Kiuchumi:** Tanzania imefanikiwa kujitangaza kimataifa baada ya kuanzisha kituo cha taifa cha uwekezaji. Kituo hicho kinapatikana jijini Dar es salaam. Lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuweka na kudumisha mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi. Kuishauri serikali kuhusu masuala ya biashara na uwekezaji na kuchochea uwekezaji wa ndani na nje.

Halikadhalika, Tanzania hujitangaza kupitia maonesho ya biashara ya kimataifa. Mfano mzuri ni, maonesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam ambayo hufanyika kila mwaka. Katika maonesho hayo bidhaa na vivutio vya kitalii hutangazwa kwa mataifa mengine yanayoshiriki katika maonesho hayo. Aidha, Tanzania ina hifadhi za taifa ambazo huvutia watalii kutoka nchi mbalimbali na hivyo kulipatia taifa fedha za kigeni.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 16 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

*Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

1. Ipi kati ya zifuatazo si mfano wa kaulimbiu ya shule?
   (a) elimu ni rasilimali
   (b) ajali haina kinga
   (c) nidhamu kwa taaluma bora
   (d) elimu ni ufunguo wa maisha

2. Lipi miongoni mwa mambo yafuatayo huwavutia wazazi au walezi katika shule zetu?
   (a) walimu wasiotosheleza shuleni
   (b) ufaulu mzuri wa wanafunzi
   (c) mashamba yanayomilikiwa na shule
   (d) uhaba wa nyumba za walimu

3. Ipi kati ya zifuatazo si faida zitokanazo na mwanafunzi kushiriki katika michezo?
   (a) kuimarisha afya ya mwili na akili
   (b) kumsaidia mwanafunzi kulipa kodi
   (c) kudumisha uhusiano kati ya wanafunzi na jamii nzima
   (d) kumjengea mwanafunzi hali ya kujiamini na uthubutu

4. Mambo yafuatayo yanaweza kutajwa katika wimbo wa shule, isipokuwa:
   (a) mazingira ya shule
   (b) maendeleo ya kitaaluma
   (c) maradhi ya wanafunzi
   (d) nidhamu na utii

5. Ipi kati ya zifuatazo, si njia inayoweza kutumika kuitangaza Tanzania?
   (a) maonesho ya biashara
   (b) matangazo katika vyombo vya habari
   (c) mahubiri ya dini
   (d) michezo mbalimbali

FOR ONLINE USE ONLY

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Aghalabu | mara nyingi, kwa kawaida, mara kwa mara |
| Kichocheo | kitu kinachotia ari au shauku ya kufanya jambo |
| Maono | picha ya mambo au vitu kuhusu matarajio fulani |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza muundo wa serikali katika ngazi za kata, wilaya na mkoa. Pia, ulijifunza mgawanyo wa kazi, wajibu, pamoja na umuhimu wa kuwa na muundo wa uongozi serikalini. Katika sura hii, utajifunza historia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, muundo wa uongozi wa Serikali katika ngazi ya kitaifa na majukumu ya mihimili mitatu ya dola. Vilevile, utajifunza mamlaka na majukumu ya serikali ya kijiji, mtaa, kata, wilaya, mkoa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Umahiri huu utakusaidia kuelewa historia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, muundo wake na majukumu ya viongozi katika ngazi mbalimbali. Aidha, utakusaidia kufahamu mihimili mitatu ya dola na majukumu yake.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Historia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatokana na muungano wa nchi mbili huru. Nchi hizo ni Tanganyika na Zanzibar. Tanganyika iliongozwa na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye aliwaongoza wananchi kupigania uhuru wa Tanganyika. Tanganyika ilipata uhuru wake tarehe 9, mwezi Desemba, mwaka 1961. Uhuru huu ulipatikana chini ya chama cha Tanganyika African National Union (TANU). Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika.

Zanzibar iliongozwa na Hayati Sheikh Abeid Aman Karume ambaye aliwaongoza wananchi wa Zanzibar kupigania uhuru wao kutoka kwa utawala wa Sultani. Uhuru wa Zanzibar ulipatikana kwa mapinduzi yaliyofanyika tarehe 12, mwezi Januari, mwaka 1964 kupitia chama cha Afro Shirazi Party (ASP). Baada ya kupata uhuru Hayati Sheikh Abeid Aman Karume akawa Rais wa kwanza wa Zanzibar. Tarehe 26, mwezi Aprili, mwaka 1964 nchi hizi mbili huru ziliungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya muungano huo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akawa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 18 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muungano wa Tanzania. Hayati Sheikh Abeid Aman Karume akawa Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitaifa

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo yenye mamlaka juu ya mambo yote yanayohusu muungano katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mambo yote yanayohusu Tanzania Bara. Dola imekuwa ikitekeleza maamuzi mbalimbali kupitia Serikali, Bunge, na Mahakama. Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi ya taifa umeoneshwa kwenye Kielelezo namba 1.




**Kielelezo namba 1:** Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ngazi ya kitaifa

**Majukumu ya kila ngazi ya maamuzi ni kama ifuatavyo:**

***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:*** Rais ni kiongozi ambaye huchaguliwa na wananchi kupitia uchaguzi mkuu unaofanyika kila baada ya miaka mitano. Rais anaweza kutoka upande wowote wa Muungano ama Tanzania Bara au Zanzibar. Ikitokea Rais ametoka Tanzania Bara, Makamu wa Rais atatoka Zanzibar na vivyo hivyo iwapo Rais ametoka Zanzibar, Makamu wa Rais atatoka Tanzania Bara. Rais ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amirijeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais ana madaraka ya kuteua viongozi mbalimbali. Baadhi ya viongozi hao ni: Mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, wakurugenzi wa mashirika mbalimbali ya umma na makatibu wakuu wa wizara. Katika Baraza la Mawaziri, Rais ni mwenyekiti hivyo, huongoza mikutano yote.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Makamu wa Rais:*** Makamu wa Rais ndiye msaidizi na mshauri mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla. Vilevile, humsaidia Rais katika kufuatilia utekelezaji wa siku hata siku wa mambo ya muungano. Pia, hufanya kazi zote anazoagizwa na Rais na hufanya kazi zote za Rais kama Rais hayupo kazini au nje ya nchi. Vilevile, humwakilisha Rais katika mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Makamu wa Rais huchaguliwa na wananchi kama mgombea mwenza wa Rais katika uchaguzi mkuu. Ikitokea Makamu wa Rais amefariki au kujiuzulu, Rais atamteua mtu mwingine kushika nafasi hiyo baada ya kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mfano, mwaka 2001, baada ya aliyekuwa Makamu wa Rais Hayati Dkt. Omari Ali Juma kufariki, Rais Benjamin W. Mkapa kwa wakati huo, alimteua Dkt. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais ambaye aliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Rais wa Zanzibar:*** Ni Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye huchaguliwa na wananchi wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu. Pia, huhudhuria vikao au mikutano ya Baraza la Mawaziri. Rais wa Zanzibar hushauri juu ya mambo yote yanayohusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Waziri Mkuu:*** Waziri Mkuu huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waziri Mkuu hutoka miongoni mwa wabunge wa kuchaguliwa kutoka katika majimbo ya uchaguzi. Waziri Mkuu huidhinishwa na Bunge na ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za serikali bungeni. Vilevile, Waziri Mkuu ana madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Halikadhalika, Waziri Mkuu hutekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe.

***Baraza la Mawaziri:*** Mawaziri huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kushauriana na Waziri Mkuu. Ibara ya 54 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inataja kuwepo kwa Baraza la Mawaziri ambalo wajumbe wake watakuwa ni Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na Mawaziri wote. Rais atahudhuria mikutano ya Baraza la Mawaziri na ndiye atakayeongoza mikutano hiyo. Baraza la Mawaziri ndicho chombo kikuu cha kumshauri Rais juu ya mambo yote yanahusika katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Halikadhalika, Baraza la Mawaziri litamsaidia na kumshauri Rais juu ya jambo lolote litakaowasilishwa kwenye baraza hilo kwa mujibu wa maagizo maalumu au maagizo ya jumla yatakayotolewa na Rais. Pia, Mawaziri ndio

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wasimamizi wakuu wa shughuli za kila siku za wizara zao, wakisaidiana na Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara. Ikumbukwe kuwa Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara siyo sehemu ya wajumbe wa Baraza la Mawaziri.


***Katibu wa Baraza la Mawaziri:*** Ni mtendaji mkuu katika ofisi ya Baraza la Mawaziri na hufanya kazi anazoagizwa na Rais. Miongoni mwa majukumu yake ni pamoja na kuandaa ratiba ya mikutano ya baraza na kutayarisha orodha ya shughuli za kila mikutano, huandika na kuweka kumbukumbu za mikutano ya baraza na kutoa taarifa na maelekezo ya maamuzi ya baraza kwa kila mtu au chombo cha umma kinachohusika na uamuzi wowote na kutekeleza kazi na shughuli nyingine zozote atakazoagizwa mara kwa mara na Rais.

***Mwanasheria Mkuu wa Serikali:*** Ni mtu mwenye taaluma ya sheria. Ni mjumbe wa Baraza la Mawaziri anayehudhuria mikutano ya baraza hilo na kupewa haki zote za ujumbe isipokuwa hana haki ya kupiga kura ya uamuzi katika mikutano hiyo. Pia, akiwa katika Baraza la Mawaziri, hushauri masuala ya kisheria katika baraza hilo.

## Zoezi la 1

1. Taja mamlaka kuu tatu za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Eleza kazi za Baraza la Mawaziri.
3. Taja wajumbe wa Baraza la Mawaziri.
4. Kwa nini Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaingia katika Baraza la Mawaziri wakati yeye sio waziri?
5. Eleza majukumu ya Rais wa Zanzibar katika vikao vya Baraza la Mawaziri.

## Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wenzako kuhusu Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutaja majina ya mawaziri na wizara zao. Andika majina ya mawaziri na wizara zao katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 21 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mihimili ya Dola

Dola ni chombo chenye madaraka kamili ya kusimamia shughuli za utawala na siasa ndani ya nchi bila kujali ukubwa au udogo wa eneo hilo. Dola ina mihimili mikuu mitatu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imewekwa ili kuwepo na mgawanyo mzuri wa madaraka katika nchi. Kiutendaji, kila mhimili unapaswa kufanya kazi kwa uhuru bila ya kuingiliwa na mhimili mwingine. Mihimili yote hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### Serikali

Kwa mujibu wa Ibara ya 34 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mamlaka ya mhimili wa utawala yaani serikali yapo mikononi mwa Rais. Mhimili huu ndio msimamizi wa masuala ya kiutawala na utoaji wa huduma za umma. Majukumu ya serikali yapo katika mambo yote yanayohusu muungano na yale yanayohusu Tanzania Bara. Majukumu hayo ni pamoja na kulinda katiba ya nchi, sheria zote zinazotungwa na Bunge, mipaka ya nchi na usalama wa wananchi na maliasili za taifa. Pia, serikali ina jukumu la kukusanya kodi, ushuru wa forodha na kupokea misaada kwa ajili ya nchi. Vilevile, kuwapa wananchi huduma bora za jamii kama vile elimu, afya, maji, mawasiliano na kuboresha miundombinu. Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina wajibu wa kusimamia utamaduni wa taifa, mila, desturi, siasa, uchumi, utawala bora, demokrasia na kuelimisha wananchi juu ya mambo yote ya uchaguzi, haki na wajibu wa kila raia.

### Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge ni chombo kinachotunga sheria na kuwakilisha wananchi. Pia, Bunge hujadili mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika kuongoza serikali. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Rais na sehemu ya pili ni wabunge. Rais kama sehemu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawajibu wa kulihutubia Bunge siku ambayo Bunge jipya limeitishwa ili kukutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi mkuu na siku ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha uchanguzi mkuu mwingine kufanyika. Pia, Rais anajukumu la kutoa kibali cha kutumika sheria fulani kwa kusaini miswada ya sheria hizo iliyojadiliwa na kupitishwa bungeni.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 22 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Bunge la Tanzania lina aina za wabunge wafuatao; wabunge wa kuchaguliwa na wananchi wakati wa uchaguzi mkuu na wanatokana na majimbo ya uchaguzi, wabunge wasiozidi kumi (10) wa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge wanawake wa viti maalumu ambao idadi yao haipungui asilimia thelathini (30%) ya wabunge wote, wabunge watano (5) ambao hutokana na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Majukumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

*Kutunga sheria za nchi:* Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndilo lenye jukumu la kutunga sheria zote za nchi. Ingawa sheria zingine ndogondogo hutungwa na mamlaka zingine kama vile serikali za mitaa kwa kuzingatia sheria zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Kujadili na kupitisha bajeti za serikali:* Bajeti za wizara zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hujadiliwa na hupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Bunge hujadili utekelezaji wa bajeti zilizopita za wizara hizo.

*Kujadili na kuridhia mikataba:* Mikataba mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayohitaji ridhaa ya Bunge huridhiwa na Bunge baada ya kujadiliwa.

*Kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali:* Bunge lina mamlaka ya kupiga kura ya kutokuwa na imani na Rais na serikali yake. Kupitia kura ya uamuzi, Bunge lina nguvu ya kumuondoa Rais madarakani kama atakuwa amekwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Kuchunguza mikataba na rushwa:* Bunge lina mamlaka ya kuchunguza mikataba na vitendo vya rushwa na ubadhirifu na kuutolea uamuzi.

*Kumchagua Spika:* Bunge linachagua Spika na Naibu Spika wa Bunge la Tanzania.

*Kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu:* Baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchaguliwa na wananchi na kuapishwa, huwa na jukumu la kumteua Waziri Mkuu. Baada ya Rais kumteua Waziri Mkuu, Bunge lina wajibu wa kuthibitisha uteuzi huo. Pia, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina mamlaka ya kuihoji serikali kuhusu mambo ya kitaifa na ya kimataifa, katika nyanja mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiulinzi na kiusalama.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 23 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Viongozi wa Bunge***

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina viongozi wafuatao: Spika, Naibu Spika, Waziri Mkuu, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni na Katibu wa Bunge.

*Spika wa Bunge:* Ni kiongozi wa Bunge ambaye huchaguliwa na wabunge na ni mkuu wa shughuli za vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Naibu Spika:* Huchaguliwa miongoni mwa wabunge kwa lengo la kumsaidia Spika kutekeleza majukumu yake. Endapo Spika na Naibu Spika wake hawapo bungeni, vikao vya Bunge huendeshwa na wenyeviti wa Bunge.

*Waziri Mkuu:* Ndiye msimamizi na kiongozi mkuu wa shughuli zote za serikali bungeni.

*Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni:* Huchaguliwa kutoka katika kambi rasmi ya upinzani. Pia, hutokana na wabunge wa kambi ya upinzani kutoka katika chama kilichopata wabunge wengi.


*Katibu wa Bunge:* Huteuliwa na Rais na ndiye mtendaji mkuu wa ofisi ya Bunge. Kazi yake ni kusimamia watumishi wote wa Bunge na kuandaa mikutano ya Bunge.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 2

1. Taja aina za wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Je, ni katika mazingira yapi Bunge linaweza kumuondoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania madarakani?
3. Eleza kazi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wanafunzi wenzako umuhimu wa kuwa na vyama vya upinzani bungeni. Andika umuhimu wa vyama hivyo katika daftari lako la mazoezi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 24 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mahakama**

Mahakama ni chombo cha kutafsiri sheria zilizotungwa na Bunge na kutoa haki kwa wananchi wote. Pia, husikiliza, husuluhisha na kutoa maamuzi mbalimbali ya kisheria kwa haki baina ya pande zinazovutana. Mahakama zimegawanyika katika ngazi kuu tano ambazo ni Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Mkoa, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

*Mahakama ya Mwanzo*

Mahakama ya mwanzo ndiyo mahakama ya ngazi ya chini kabisa katika mfumo wa mahakama Tanzania. Mahakama hii hupatikana katika ngazi za kata na huongozwa na Hakimu. Mahakama hii haina utetezi wa mawakili kwa watuhumiwa na walalamikaji. Mamlaka ya mahakama hii huishia katika kushughulikia migogoro, kesi za jinai na madai ya fedha kama ilivyopewa mamlaka kisheria. Hakimu wa mahakama ya mwanzo ni sharti awe na elimu ngazi ya shahada ya sheria na awe amehitimu shule ya sheria.

*Mahakama ya Wilaya*

Mahakama ya Wilaya husikiliza na kuamua kesi zote zenye madai kama ilivyopewa mamlaka kisheria. Mahakama hii huongozwa na Hakimu Mfawidhi mwenye elimu ngazi ya shahada ya sheria na aliyehitimu shule ya sheria. Hakimu huyo sharti awe na uzoefu wa muda mrefu wa shughuli za mahakama.

*Mahakama ya Hakimu Mkazi*

Mahakama ya Hakimu Mkazi pia hujulikana kama Mahakama ya Mkoa. Mahakama hii uhudumiwa na Hakimu mwenye shahada ya sheria na aliyehitimu mafunzo katika shule ya sheria. Katika mahakama hii mawakili huruhusiwa kutetea watuhumiwa katika kesi za jinai na madai. Katika ngazi hii kesi zote za jinai na madai husikilizwa isipokuwa kesi za mauaji na makosa maalumu yaliyoainishwa na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai.

*Mahakama Kuu ya Tanzania*

Mahakama Kuu huongozwa na Jaji Mkuu ambaye ni mwanasheria mwenye elimu ya kuanzia shahada ya sheria na uzoefu wa muda mrefu wa shughuli za mahakama. Mahakama Kuu husikiliza aina zote za kesi za madai na jinai, kama vile mauaji na ubakaji. Kuna mahakama tanzu chini ya Mahakama Kuu ambazo ni Mahakama maalumu za katiba, ufisadi, biashara, kazi na ardhi.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Mahakama ya Rufaa*

Mahakama ya Rufaa ni ngazi ya juu ya mahakama nchini. Kiongozi mkuu wa ngazi hii ya Mahakama ni Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa. Mahakama hii husikiliza na kuamua kesi za rufaa zilizowasilishwa kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania Bara na Visiwani. Hii ni Mahakama ya ngazi ya juu kabisa ya kutatua mashauri nchini Tanzania. Muundo wa ngazi za mahakama Tanzania umeanishwa katika Kielelezo namba 2.

**Muundo wa Ngazi za Mahakama Tanzania**




**Kielelezo namba 2:** Ngazi za Mahakama Tanzania

***Majukumu ya jumla ya Mahakama nchini Tanzania***

Kuna kazi mbalimbali zinazofanywa na mahakama zetu. Kazi hizo ni pamoja na kutafsiri sheria mbalimbali zinazotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria ndogondogo zinazotungwa na Serikali za Mitaa. Kazi nyingine ni kutoa haki kwa wananchi wote bila kujali rangi, kabila, imani na cheo cha mtu. Vilevile, husikiliza na kutoa usuluhishi wa kesi mbalimbali katika ngazi tofauti za mahakama. Halikadhalika, hutoa amri ya kufidiwa kwa watu walioathiriwa na makosa mbalimbali. Pia, mahakama zina jukumu la kusimamia na kuona haki ikitendeka kwa watu wote nchini.

Pamoja na kazi nzuri za mahakama bado kuna changamoto zinazoikabili. Changamoto hizo ni pamoja na ucheleweshwaji wa kusikiliza kesi zilizofunguliwa katika mahakama kutokana na kuchelewa kukamilika kwa upelelezi. Kuchelewa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 26 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kutoa uamuzi kwa kesi zilizokwisha kusikilizwa. Pia, kuna mazingira duni ya kufanyia kazi kwa baadhi ya mahakama hasa zile za mwanzo. Mahakama hizo zina upungufu mkubwa wa vitendea kazi na uhaba wa mahakimu. Halikadhalika, kuwepo kwa mazingira ya vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wa mahakama wasiowaaminifu.

## Zoezi la 3

1. Nini maana ya mahakama?
2. Taja mahakama ya chini kabisa nchini na kiongozi anayesimamia mahakama hiyo.
3. Eleza majukumu matano ya mahakama ya Tanzania.
4. Eleza changamoto tano zinazoikabili mahakama ya Tanzania.
5. Taja cheo cha kiongozi mkuu wa mahakama ya Tanzania.

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wanafunzi wenzako sababu zinazofanya mahakama za mwanzo kutokuwa na mawakili wa kutetea watuhumiwa na walalamikaji tofauti na mahakama za juu. Andika sababu hizo katika daftari lako la mazoezi.

**Uhusiano uliopo kati ya mihimili mitatu ya dola**

*Serikali:* Hiki ndicho chombo kinachoandaa miswada ya sheria, sera na mipango ya maendeleo na kupeleka bungeni kujadiliwa. Baadhi ya sera hazipelekwi bungeni kama hazihusu mabadiliko ya sheria.

*Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:* Hutunga sheria za nchi na hupokea miswada na mipango ya serikali kutoka kwa Baraza la Mawaziri na kuijadili bungeni.

*Mahakama:* Huzitafsiri, huzilinda na kuzisimamia sheria zilizotungwa na kupitishwa na Bunge kwa kutoa haki kwa wananchi na makundi mbalimbali ya jamii.

Mihimili hii mitatu ina nguvu sawa na hufanya kazi kwa kutegemeana lakini bila kuingiliana katika kutekeleza majukumu yao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ngazi za mamlaka ya maamuzi katika serikali

Mamlaka ya maamuzi katika serikali ni tawala zilizoundwa kisheria na zenye mamlaka kamili ya kujiendesha kwa mujibu wa sheria za nchi zinazoongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uongozi serikalini huanzia ngazi ya chini kabisa ya kitongoji hadi ngazi ya kitaifa.

**Mamlaka ya maamuzi ya serikali ngazi ya kijiji au mtaa:** Kijiji au mtaa ni ngazi ya mwanzo ya uongozi katika serikali. Ngazi ya kijiji hutumika maeneo ya kijijini wakati mtaa hutumika maeneo ya mjini. Kijiji huundwa na vitongoji kadhaa ambavyo huongozwa na wenyeviti wa vitongoji. Mtaa huongozwa na mwenyekiti anayechaguliwa na wananchi katika mtaa wake. Viongozi wa juu wa mtaa au kijiji ni Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji. Mtaa au kijiji kina mamlaka kamili ya kutoa na kusimamia maamuzi na maazimio ya kutekelezwa katika mtaa au kijiji.

**Mamlaka ya maamuzi ya serikali ngazi ya kata:** Katika ngazi ya kata kuna ofisa mtendaji wa kata ambaye ni mtendaji mkuu wa shughuli za serikali. Pia, kuna diwani ambaye ni mwakilishi wa wananchi katika ngazi ya kata. Maamuzi katika ngazi ya kata yanafanyika kwa kupitia kamati ya maendeleo ya kata ambayo mwenyekiti wake ni diwani na katibu wa kamati ni ofisa mtendaji wa kata. Kamati hiyo inajumuisha wenyeviti wa vijiji kutoka vijiji vinavyounda kata au viongozi wa mitaa inayounda kata kwa kata zilizopo mijini. Pia, kamati hiyo inajumuisha wataalamu kutoka idara mbalimbali katika ngazi ya kata kwa ajili ya ushauri. Serikali ngazi ya kata ina mamlaka ya kusimamia na kutekeleza sera na mipango ya maendeleo katika kata husika. Pia, hufuatilia na kutoa maamuzi juu ya utekelezaji wa maagizo mbalimbali kutoka mamlaka za juu serikalini.

**Mamlaka ya maamuzi ya serikali ngazi ya wilaya:** Maamuzi ya mipango mbalimbali ya maendeleo katika ngazi ya wilaya husimamiwa na serikali za mitaa ambazo ni wakala wa serikali kuu. Serikali za mitaa hujulikana kama halmashauri ya wilaya, mji au manispaa au jiji. Halmashauri ya wilaya husimamia mipango ya maendeleo katika maeneo ya vijijini. Halmashauri ya mji, manispaa au jiji husimamia maendeleo katika maeneo ya mji wenye hadhi husika.

Halmashauri za wilaya, miji au manispaa zinahusika kubuni na kupanga mipango ya maendeleo katika maeneo yao. Halmashauri au manispaa hizo hufanya maandalizi na maamuzi ya utekelezaji wa miradi kuanzia ngazi ya kijiji, kata na wilaya husika. Kamati ya maendeleo ya wilaya huratibu mipango yote ya maendeleo katika wilaya.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 28 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Mamlaka ya maamuzi ya serikali ngazi ya mkoa:** Serikali ya mkoa ni chombo cha utekelezaji cha serikali za mitaa na serikali kuu katika mkoa husika. Kupitia kamati ya maendeleo ya mkoa, serikali inaeleza na kutafsiri sera na maagizo mengine kutoka serikali kuu. Serikali ya mkoa huongozwa na Mkuu wa Mkoa. Muundo wa serikali ya mkoa unajumuisha Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa na wakuu wa vitengo kama vile elimu, afya na miundombinu.

**Mamlaka ya maamuzi ya serikali ngazi ya serikali kuu:** Serikali kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo yenye mamlaka ya maamuzi ya masuala yote ya muungano na yale yanayohusu Tanzania Bara. Kwa mfano, maamuzi katika utoaji wa haki, utungaji wa sheria na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za umma. Shughuli zote za mamlaka ya nchi hutekelezwa na kudhibitiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## Zoezi la 4

1. Taja majukumu mawili ya serikali ngazi ya kijiji au mtaa.
2. Taja mamlaka ya maamuzi ya serikali katika ngazi ya kata.
3. Kiongozi mkuu wa serikali katika ngazi ya mkoa ni nani?

## Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wanafunzi wenzako, majukumu ya Ofisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa. Andika majukumu hayo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 5

**A:** *Jibu maswali yafuatayo, andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

1. Taja kiongozi mkuu wa shughuli za serikali bungeni.
2. Chora muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
3. Nini maana ya ngazi ya uamuzi katika serikali?

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 29 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B:** *Oanisha kipengele kutoka* ***Sehemu A*** *na kipengele kutoka* ***Sehemu B****, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 4. Mhimili wa dola wenye mamlaka ya kutunga sheria | (a) Wabunge |
| 5. Huteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge | (b) Serikali |
| 6. Hutafsiri sheria na kutoa haki kwa watu wote | (c) Mahakama |
| 7. Wawakilishi wa wananchi | (d) Waziri Mkuu |
| 8. Huwapa wananchi huduma za jamii kama vile elimu, afya, na maji | (e) Bunge |
| | (f) Demokrasia |
| | (g) Polisi |

**C:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

9. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeundwa na serikali mbili, nazo ni:
   (a) Bunge na mahakama
   (b) Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar
   (c) Baraza la Mawaziri na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar
   (d) Serikali za Mitaa na Serikali Kuu

10. Ipi kati ya zifuatazo si kazi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?
   (a) kujadili na kuridhia mikataba
   (b) kutunga sheria na kupitisha bajeti
   (c) kutoa hukumu kwa wavunja sheria
   (d) kupitisha bajeti

11. Mahakama ni mhimili wa dola unaohusiana na kazi zifuatazo, isipokuwa:
   (a) kupokea mashitaka
   (b) kutunga sheria
   (c) kusikiliza na kuamua kesi
   (d) kutafsiri sheria

12. Sheria hutungwa na huanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na:
   (a) Spika wa Bunge
   (b) Rais

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Jaji Mkuu wa Tanzania
(d) Jaji Kiongozi wa Tanzania

13. Ni njia ipi hutumika kuwapata watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wasio wabunge?
    (a) kuajiriwa na serikali
    (b) kupigiwa kura na wananchi
    (c) kuteuliwa na Waziri Mkuu
    (d) kuteuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**D:** *Andika* ***Kweli*** *kwa sentensi iliyo sahihi na* ***Si Kweli*** *kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

14. Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutoka miongoni mwa wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania._______
15. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutunga sheria ambazo husimamiwa na Mahakama._______
16. Mtumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza pia kuwa Mbunge na akaendelea na utumishi wake._______
17. Majaji wa Mahakama za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge._______
18. Mapato na matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania._______
19. Jina rasmi la katiba ya nchi yetu ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977._______

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Ibara | kifungu cha maneno yenye habari inayojitosheleza kimaana |
| Jinai | shitaka la uhalifu linalomsababishia mtu mashitaka |
| Kuridhia | kuruhusu jambo au kitu kifanyike |
| Mfawidhi | mtu aliyeteuliwa kuongoza shughuli za kitengo au idara |
| Tanzu | sehemu au tawi la kampuni, kiwanda au taasisi fulani |
| Ufisadi | tendo la kufanya ubadhirifu au wizi wa mali zilizopo katika dhamana yako |



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 31 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Demokrasia

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza dhana ya demokrasia na umuhimu wa demokrasia katika ustawi wa jamii, kazi ya vyama vya siasa, umuhimu wa uvumilivu wa kisiasa na kutambua Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika sura hii, utajifunza jinsi demokrasia inavyotekelezwa nchini Tanzania, pamoja na sifa za kiongozi anayefaa kuchaguliwa katika ngazi ya taifa. Pia, utajifunza misingi ya demokrasia katika utekelezaji wa kazi, taratibu za kidemokrasia za kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, utajifunza misingi ya utawala bora, umuhimu wa utawala bora katika taifa na wajibu wa serikali katika kukuza utawala bora. Umahiri huu utakusaidia kufanya tathmini ya utekelezaji wa demokrasia nchini na kushiriki katika kuchagua viongozi wenye sifa katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya demokrasia. Aidha, kutakuwezesha kushirikiana na wengine kukemea vitendo vinavyokiuka utawala bora.*

### Matukio ya kidemokrasia yaliyofanyika nchini

Nchi ya kidemokrasia hutambulika kwa kuangalia matukio mbalimbali yanayotokea katika nchi husika. Matukio hayo yanaweza kuwa ya kisiasa, kijamii au yale yanayohusu shughuli za kiuchumi. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi ya Tanzania sharti iongozwe kidemokrasia. Kwa hiyo,Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongozwa kidemokrasia. Matukio mbalimbali yanayothibitisha utekelezaji wa demokrasia Tanzania ni kama yafuatayo:

**Uhuru wa kutoa mawazo:** Nchi yenye demokrasia huwapa wananchi wake uhuru wa kutoa maoni katika mambo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ili kutoa mitazamo yao kwa lengo la kuleta ustawi wa jamii husika. Wananchi wanaweza kutoa mawazo yao au kupata habari kupitia redio, runinga, magazeti, mitandao ya kijamii na mikutano ya hadhara.



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 32 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Uchaguzi huru na wa haki:** Nchi yenye demokrasia huwapa wananchi wake uhuru wa kushiriki katika uchaguzi kwa kugombea nafasi za uongozi au kuchagua kiongozi wanayemtaka bila kubughudhiwa. Viongozi wa serikali za mitaa na wale wa serikali kuu hapa Tanzania huchaguliwa kwa kura. Uchaguzi huendeshwa kwa kufuata sheria chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kura huhesabiwa kwa uwazi na matokeo hutangazwa. Hivyo, uchaguzi wa viongozi wa kisiasa huwa huru na wa haki.

**Kuanzisha na kujiunga na chama cha siasa:** Katika nchi yenye demokrasia, wananchi wana uhuru wa kuanzisha chama cha siasa au kujiunga na chama cha siasa kwa kufuata kanuni, taratibu na sheria zilizopo. Tangu mwaka 1992, Tanzania inaongozwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kila raia ana uhuru wa kuanzisha chama au kujiunga na chama chochote cha siasa akipendacho.

**Uhuru wa kukusanyika:** Nchi yenye demokrasia hutoa fursa kwa wananchi wake kushiriki kwenye mikusanyiko, mikutano au makongamano ya kijamii, kidini, kisiasa na kiuchumi. Kwa mfano, vyama vya siasa vinapofanya mikutano wananchi wana uhuru kuhudhuria bila kikwazo chochote. Mihadhara ya dini huruhusiwa na wananchi wapo huru kuiandaa na kuhudhuria. Pia, wananchi wana uhuru kushiriki katika makongamano ya kijamii na kiuchumi, kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria za nchi.

**Maandamano ya amani:** Nchi yenye demokrasia huruhusu maandamano ya amani kwa wananchi wake ili kuonesha hisia zao. Wananchi huonesha hisia zao kwa watawala pale wanapotaka kukosoa mambo ambayo yanawanyima haki. Pia, maandamano yanaweza kutumika ili kupongeza mambo ambayo yamefanyika vyema. Mamlaka zinazolinda usalama na amani hutoa vibali kwa ajili ya mikusanyiko na maandamano baada ya kujiridhisha kuwa maandamano hayo yatakuwa ni ya amani.

**Ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji:** Ushirikishwaji wa wananchi kwenye maamuzi mbalimbali ni jambo muhimu kwa nchi yenye demokrasia. Wananchi hupewa fursa ya kushiriki, kuweka au kupanga mipango yao ya maendeleo na kutoa uamuzi wa mambo yanayowahusu. Nchini Tanzania, mipango ya maendeleo huanzia katika ngazi ya kijiji au mtaa katika mikutano ya wananchi wenyewe. Kwa kupitia demokrasia ya uwakilishi, wananchi hushiriki katika utawala, uongozi wa nchi na utunzi wa sheria na sera. Viongozi hufanya mambo yote ya uongozi kwa uwazi na wanawajibika kutoa taarifa za mapato na matumizi kuanzia ngazi ya kijiji, mtaa hadi taifa.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 33 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Haki za binadamu:** Haki za binadamu lazima ziheshimiwe na kulindwa katika nchi inayofuata demokrasia. Haki za kila Mtanzania hulindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mfano, watu wote ni sawa mbele ya sheria, watoto hupatiwa elimu na watu wana uhuru wa kuabudu. Pia, kuna vyombo vya kutetea haki za wanawake, haki za watoto na haki za binadamu kwa ujumla.

**Utawala wa sheria:** Utawala wa sheria ni nguzo muhimu katika nchi yenye demokrasia. Utawala wa sheria hulinda raia wasionewe au kunyanyaswa na husaidia kupatikana haki zao. Vilevile, utawala wa sheria huzuia viongozi kutumia madaraka yao vibaya. Tanzania inaongozwa kwa kuzingatia utawala wa sheria na sheria kuu ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utawala wa sheria unasaidia kuwepo kwa usawa katika jamii.

**Uvumilivu wa kisiasa:** Nchi yenye demokrasia huruhusu mtu, watu, vyama au jamii zenye maoni na mitazamo tofauti, kuishi pamoja na kushirikiana bila kugombana. Huduma za jamii hutolewa bila upendeleo wa kiitikadi. Wapo Wabunge na Madiwani kutoka vyama mbalimbali lakini wote hufanya vikao pamoja ili kupanga na kujadili maendeleo ya nchi bila kuchukiana wala kupigana.

## Zoezi la 1

1. Je, ni matukio gani yanadhihirisha demokrasia inavyotekelezwa katika nchi yetu?
2. Eleza umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi katika kukuza demokrasia.
3. Kuna faida gani ya kuwa na demokrasia katika nchi yetu?

## Kazi ya kufanya namba 1

Bainisha mambo yanayodhihirisha uwepo wa demokrasia katika shule yako. Andika mambo yote uliyobainisha katika daftari lako la mazoezi.

### Misingi ya demokrasia

Tumeona baadhi ya mambo yanayoonesha kwamba Tanzania ni nchi ya kidemokrasia. Hata hivyo, Tanzania siyo nchi pekee ya kidemokrasia duniani. Zipo nchi nyingine nyingi zinazofuata misingi ya kidemokrasia. Pia, ipo misingi inayoongoza na kutambulisha demokrasia popote pale duniani.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Misingi hiyo inapokiukwa basi tunasema nchi hiyo siyo nchi ya demokrasia. Kwa ujumla, misingi ya demokrasia ni haki za binadamu, usawa, mfumo wa vyama vingi vya siasa, uchaguzi huru na wa haki, utawala wa sheria, uwazi, ukweli na uwajibikaji. Misingi ya demokrasia imewasilishwa katika Kielelezo namba 1.




**Kielelezo namba 1:** Misingi ya demokrasia

## Sifa za kiongozi

Kiongozi ni mtu anayewaelekeza au kuwaongoza wenzake ili kufikia malengo yao. Ili aweze kumudu majukumu yake vizuri, kiongozi anapaswa kuwa na sifa mbalimbali. Baadhi ya sifa za kiongozi ni kama zifuatavyo:

**Uadilifu:** Kiongozi anapaswa kuwa mwadilifu ili kuwa na mwenendo mzuri kwenye utendaji wake wa kazi. Kiongozi mwadilifu huzingatia sheria, kanuni na taratibu, hutunza mali ya umma, hatumii madaraka yake kufanya ubadhirifu wa mali ya umma, hapokei au kutoa rushwa, na hufanya kazi kwa bidii na weledi.

**Kujituma:** Kujituma ni jambo la msingi katika uongozi. Kiongozi hujituma kwa kufanya kazi kwa bidii na kushirikiana na wenzake. Pia, awe mtu wa kujitolea kuwatumikia anaowaongoza kwa hali na mali na kuwa tayari kutumika kwa masilahi ya wengine.

**Ukweli, uwazi na usikivu:** Kiongozi anapaswa kuwa mkweli, muwazi na msikivu katika utendaji wake wa kazi. Utendaji wa kazi unatakiwa ueleweke kwa wale anaowaongoza ili kufikia malengo na mafaniko yenye tija kwa taasisi au kampuni. Pia, anapaswa kuwa muwazi, kupokea ushauri na kusikiliza maoni ya watu wengine.

**Maono:** Kiongozi mzuri anapaswa kuwa na maono ya taasisi au kampuni anayoiongoza ili kufikia malengo na mafanikio yake. Anapaswa kuwa na malengo dhahiri na kuwa mbunifu ili kuleta maendeleo endelevu kwa taasisi, nchi au kampuni husika. Kwa mfano, kiongozi awe na uwezo wa kubuni miradi itakayowezesha taasisi au kampuni kukua na kujiendesha kwa ufanisi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 35 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ujasiri:** Kiongozi bora ni jasiri na anayethubutu kutoa uamuzi wa masuala magumu. Anapaswa kutoa uamuzi wa haraka na sahihi kwa manufaa ya taasisi au kampuni anayoiongoza. Kwa mfano, kufanya uwekezaji au kubadili mfumo wa utendaji ili kufikia malengo.

**Uvumilivu na ustahimilivu:** Kiongozi anapaswa kuwa mvumilivu na mstahimilivu kwa wale anaowaongoza na kuwa na subira katika vipindi vigumu. Pia, anapaswa kutoa uamuzi sahihi katika hali ngumu bila kuathiri taasisi anayoiongoza.


**Uwajibikaji:** Kiongozi ni yule aliye tayari kujibu, kubeba dhamana na kutoa maelekezo kwa wale anaowaongoza juu ya uamuzi alioufanya katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Utendaji haki:** Kiongozi anayefuata demokrasia, anapaswa kutoa haki sawa kwa wote bila ubaguzi au uonevu kwa mtu yeyote. Kiongozi amepewa mamlaka na watu, hivyo, hapaswi kujiona mwenye haki zaidi ya wale anaowaongoza mbele ya sheria.

## Zoezi la 2

1. Eleza maana ya kiongozi.
2. Taja sifa tano za kiongozi.
3. Kuna umuhimu gani wa kuwa na mawasiliano katika uongozi?
4. Taja faida tano za kuwa na kiongozi katika jamii tunamoishi.
5. Je, ni kwa nini kiongozi anapaswa kutenda haki na kuwa muwazi?

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako hasara tano za kuwa na kiongozi asiyekuwa na sifa za uongozi. Andika hasara hizo kwenye daftari lako la mazoezi.

### Taratibu za kidemokrasia za kumchagua Rais

Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hufanyika kila baada ya miaka mitano. Utaratibu wa kidemokrasia wa kumpata na kumpigia kura mgombea wa urais uko kama ifuatavyo:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Ni sharti mgombea ateuliwe na chama cha siasa kugombea nafasi ya urais;
(b) Mgombea achukue fomu katika ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, aijaze na kuirudisha;
(c) Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza majina ya wagombea urais waliokidhi matakwa ya uchaguzi kwa wananchi;
(d) Wagombea watapata fursa ya kunadi sera na ilani za vyama vyao kwa wapiga kura wakati wa kampeni za uchaguzi;
(e) Wapiga kura watapata fursa ya kupiga kura za siri katika vituo vya kupigia kura vilivyoainishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika maeneo yao wanayoishi;
(f) Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza matokeo ya uchaguzi baada ya kuhesabu kura katika vituo vyote na kumtangaza mshindi wa nafasi ya urais;
(g) Mshindi wa nafasi ya urais atakuwa Rais mteule mara baada ya matokeo; na
(h) Rais mteule ataapishwa na Jaji Mkuu wa Tanzania na kuanza rasmi kazi ya kuwatumikia wananchi.

## Sifa za mgombea urais

Sifa za mgombea wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kama zifuatazo:
(a) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa kwa mujibu wa sheria ya uraia;
(b) Awe ametimiza miaka arobaini au zaidi;
(c) Awe mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;
(d) Awe na sifa ya kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na
(e) Asiwe ametiwa hatiani katika mahakama kwa kosa la jinai kama kukwepa kulipa kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

## Taratibu za kidemokrasia za kuwachagua wabunge nchini Tanzania

Utawala wa kidemokrasia ni utawala unaohitaji ushirikishwaji wa wananchi wote katika uongozi wa nchi yao. Kwa kuwa taifa ni kubwa na watu ni wengi, haiwezekani kila mtu ahudhurie vikao vya maamuzi ya kitaifa. Kwa hiyo, wananchi huchagua wawakilishi wa majimbo ambao huwakilisha mawazo yao bungeni. Wawakilishi hawa huitwa wabunge. Uchaguzi wa wabunge hufanyika kila baada ya miaka mitano na husimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Uchaguzi wa wabunge hufanyika kwa taratibu zifuatazo:



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 37 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Kila mgombea ambaye ni raia wa Tanzania atajaza fomu ya kugombea ubunge toka Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kuteuliwa au kuchaguliwa na chama chake cha siasa;

(b) Kila mgombea atapata fursa ya kufanya kampeni katika jimbo lake la uchaguzi ili kunadi sera na ilani ya chama chake;

(c) Kila mgombea ubunge atapata nafasi ya kuwa na wakala wake katika kituo cha kupigia kura;

(d) Kila mgombea atatangaziwa matokeo baada ya kura kuhesabiwa na mshindi atatangazwa; na

(e) Mshindi wa kiti cha ubunge ataapa kiapo cha utii na uaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mbele ya Spika kabla ya kuanza rasmi kazi ya kuwatumikia wananchi wa jimbo lake.

### Sifa za mgombea ubunge

Sifa za mgombea ubunge zimeainishwa kama ifuatavyo:

(a) Awe mtu mwenye akili timamu;

(b) Awe raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja;

(c) Awe anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;


(d) Awe mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa kilichosajiliwa na Msajili wa vyama vya siasa; na

(e) Asiwe ametiwa hatiani katika mahakama kwa kosa la jinai kama kukwepa kulipa kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

## Zoezi la 3

1. Mgombea ubunge hupendekezwa na nani?
2. Mshindi wa nafasi ya urais huapishwa na nani?
3. Eleza umuhimu wa wananchi kupiga kura kwa siri.
4. Taja taratibu zinazotumika kupata wabunge.

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wenzako kuhusu kazi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Andika mambo mliyojadiliana katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 38 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Misingi ya utawala bora

Utawala bora ni mfumo wa kutumia madaraka kwa manufaa ya wananchi au wale watumikiwa. Misingi ya utawala bora ni uwazi, uwajibikaji, utawala wa sheria, ushirikishwaji, usawa, haki za binadamu, uadilifu, ufanisi, demokrasia, kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka na maridhiano.

**Uwazi:** Uwazi ni hali ya kuyaweka mambo bayana. Uwazi unasaidia wananchi kupata taarifa za uendeshaji wa shughuli za umma ili kuwapa uwezo wa kupima utendaji wa viongozi wao katika kuzingatia kanuni, taratibu na sheria. Uwazi ni muhimu katika kutoa taarifa za mapato na matumizi. Uwazi husaidia wananchi kupata taarifa za mipango na bajeti za kutekeleza mipango hiyo. Katika kuweka utaratibu wa kupata huduma za kijamii na kudhibiti uhalali wa maamuzi yanayofanywa na viongozi, uwazi ni suala la msingi.

**Uwajibikaji:** Ni hali ya utayari wa viongozi wa umma na taasisi inayowawezesha kujibu, kubeba dhamana, na kutoa maelezo ya kina kwa wananchi kuhusu maamuzi au vitendo walivyovifanya katika kutekeleza majukumu yao ya kikazi kwa dhamana waliyopewa.

**Utawala wa sheria:** Huu ni utawala unaoongoza kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa kama mwongozo wa sheria. Kusudi kuu la utawala wa sheria ni kutenda na kudumisha haki. Viongozi hupaswa kufuata sheria za nchi ili kutenda haki, kwa maana ya watu wote kuwa na haki sawa mbele ya sheria. Utawala bora huzingatia uendeshaji wa shughuli za umma pamoja na kufanya maamuzi kwa kufuata sheria za nchi. Baadhi ya misingi ya utawala wa sheria ni:

(a) Kila mtu anayevunja sheria huadhibiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusu adhabu kulingana na kosa lake;

(b) Kila mtu ana haki ya kufuata sheria;

(c) Mtuhumiwa ana haki ya kufikishwa mahakamani haraka na siyo kushikiliwa rumande kwa muda mrefu; na

(d) Askari polisi anapaswa kumweleza mtuhumiwa sababu za kumkamata na haki zake baada ya kumkamata.

**Ushirikishwaji:** Hii ni hali ya ujumuishaji wa jamii katika kuyafikia maamuzi yenye masilahi kwao. Viongozi wanapaswa kuwahusisha wananchi wa jinsi na makundi yote katika kupanga na kufanya uamuzi wa mambo yanayowahusu. Ushiriki wao, waweza kuwa wa moja kwa moja katika vikundi, mikutano ya hadhara au kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 39 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Usawa:** Usawa ni uwepo wa hali inayofanana. Usawa ni kipengele muhimu sana cha haki kwa sababu kinahusisha hali ya utoaji haki bila upendeleo. Usawa hujitokeza zaidi pale wananchi wanapopewa fursa sawa ya kushiriki katika mambo mbalimbali yanayowahusu katika jamii yao. Baadhi ya mambo hayo ni; kupata na kutoa huduma, kuendesha shughuli za umma bila ubaguzi au upendeleo, kuthaminiwa kwa utu wa watu wote bila kujali tofauti zao, kutambua makundi yote katika jamii na kutoa fursa sawa katika kuboresha hali zao.

**Haki za binadamu:** Haki ni ile hali ya kumpatia mtu kile ambacho anastahili au ni stahiki yake. Haki za binadamu ni stahiki ya binadamu ambayo ipo kulingana na maumbile yake. Hivyo, haki za binadamu ni stahili anazokuwa nazo mtu kwa sababu tu yeye amezaliwa binadamu. Haki hizi hujumuisha mambo yafuatayo; uhuru wa kujieleza, uhuru wa kuabudu, kupata elimu, kuishi maisha bora, usawa, uhuru wa kufanya mikutano na kutoa au kupata habari. Haki hizi hulindwa na kuzingatiwa ili kumfanya binadamu aishi kwa uhuru, furaha na amani katika kujitafutia maendeleo yake.

**Uadilifu:** Uadilifu ni hali ya kuwa na mwenendo mwema au usawa katika kutenda haki na kujali usawa kwa watu wote katika utendaji kazi. Uadilifu unahusisha kujali haki za binadamu, kuhakikisha masilahi binafsi hayagongani na wajibu wake kama kiongozi wa umma, kutaja mali zake anapoingia madarakani na baada ya kuacha madaraka. Pia, kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, kuepuka vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kuwa mkweli na kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

**Ufanisi:** Ufanisi ni ile hali ya kuweza kutumia rasilimali zilizopo kwa malengo yaliyokusudiwa tu. Iwapo fedha zimetengwa kwa ajili ya mradi au huduma fulani basi zitumike kwa lengo hilo tu na si vinginevyo. Pia, ni uwezo wa kutumia vizuri rasilimali za umma ili kuleta manufaa makubwa. Inahusisha pia kubana matumizi ili rasilimali chache ziweze kuleta matokeo makubwa kwa jamii.

**Demokrasia:** Uongozi wenye misingi ya utawala bora huzingatia demokrasia kwa kushirikisha wananchi kikamilifu katika maisha yao kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa mfano, kuchagua viongozi wao, kuwa na uchaguzi huru na wa haki, na kutoa uamuzi.

**Kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka:** Kudhibiti ni hali ya kuzuia mambo yasiende kinyume na ilivyokusudiwa. Hii ikiwa pamoja na kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka. Kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka husaidia kuzuia vitendo vya rushwa au kupokea kitu chochote cha thamani ili kutoa




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 40 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

upendeleo katika kutenda haki. Vilevile, kuzuia matumizi mabaya ya mali ya umma kwa mfano kutumia fedha na rasilimali za nchi kwa manufaa binafsi. Pia, serikali kutumia nguvu badala ya sheria au kukiuka katiba ya nchi ni matumizi mabaya ya madaraka.

**Maridhiano:** Uongozi unaozingatia misingi ya utawala bora huhimiza kuwepo kwa mawazo mbalimbali ili kupata muafaka au uamuzi wa pamoja unaozingatia masilahi ya jamii. Misingi ya utawala bora imewekwa kwa ufupi katika Kielelezo namba 2.




**Kielelezo namba 2**: Misingi ya utawala bora

## Umuhimu wa utawala bora katika jamii

Pale ambapo misingi ya utawala bora huzingatiwa, uendeshaji wa shughuli za serikali huwa na manufaa makubwa. Katika utawala bora, viongozi na wananchi wanawajibika kwa kila wanachokifanya. Panapokuwa na utawala bora hakuna rushwa. Kila mtu anapewa haki yake na kwa wakati. Katika utawala bora, serikali huwasikiliza wananchi wake na kufanya mipango mizuri ya kutatua changamoto na shida za wananchi. Katika utawala bora viongozi ni watumishi wa wananchi. Kwa vile utawala bora huhusisha ushirikishwaji wa wananchi, haki za binadamu, usawa na uadilifu.

Dhana ya utawala bora na dhana ya demokrasia zinahusiana kwa karibu sana. Haiwezekani kuwa na demokrasia bila utawala bora na vievile hapawezi kuwa na utawala bora usiokuwa wa kidemokrasia. Hivyo, faida zote zinazotokana na demokrasia zinapatikana katika utawala bora. Jamii yenye kutekeleza utawala bora ina mafanikio katika maendeleo ya binadamu. Hii ni kwa sababu viongozi na wananchi huhakikisha kwamba rasilimali hazipotei bure.




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 41 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Eleza maana ya uadilifu.
2. Kwa nini haki za binadamu zinahitajika kulindwa?
3. Taja misingi mitano ya utawala bora.
4. Je, una maoni gani kuhusu viongozi wasiofuata misingi ya utawala bora?


## Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wenzako jinsi misingi ya utawala bora inavyo tekelezwa nchini Tanzania. Andika misingi hiyo katika daftari lako la mazoezi.

### Dhana ya mgawanyo wa madaraka

Dhana ya mgawanyo wa madaraka katika demokrasia ndiyo inayoonesha dhahiri jinsi demokrasia inavyohusiana na utawala bora. Katika dhana hii, utawala wa dola hugawanywa katika mihimili mikuu mitatu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Kila mhimili unajitegemea katika majukumu yake ambayo ni tofauti na mhimili mwingine. Kazi za mamlaka ya Serikali ni utendaji; mamlaka ya Bunge ni kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali; na mamlaka ya Mahakama ni kutafsiri sheria na kutoa haki. Mgawanyo wa madaraka unazuia mhimili mmoja kutawala, kuingilia na kufanya kazi za mhimili mwingine. Lengo la mgawanyo wa madaraka ni kuimarisha utawala bora na kuongeza ufanisi na kuleta uwajibikaji wa vyombo hivyo vya dola. Mgawanyo wa madaraka Tanzania umeainishwa katika Kielelezo namba 3.




**Kielelezo namba 3:** Mgawanyo wa madaraka



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 42 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Je, kuna umuhimu gani wa kuwa na utawala bora?
2. Elezea uhusiano kati ya utawala bora na demokrasia.
3. Taja viashiria vinne vya kukosekana kwa utawala bora.
4. Unafikiri ni kwa nini demokrasia haiwezi kufanikiwa bila mgawanyo wa madaraka?

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wanafunzi wenzako namna misingi ya utawala bora inavyofuatwa katika shule yenu. Andika misingi hiyo katika daftari lako la mazoezi.

### Wajibu wa serikali katika kukuza utawala bora

Serikali inawajibika kukuza utawala bora katika ngazi zote za uongozi ili kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi wake. Serikali yenye kupenda na kujali wananchi wake hukuza utawala bora kwa kutekeleza mambo kadhaa kama ifuatavyo:

(a) Kuweka katiba bora ya nchi na sheria nyingine ili ziweze kuiongoza serikali kutekeleza majukumu yake. Katiba ya nchi ndiyo sheria mama na viongozi wote wa Tanzania huapa kiapo cha kuitunza na kuiheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) Kugawanya madaraka katika mihimili mitatu ya dola katika utawala bora ambavyo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Hii husaidia kila mhimili kusimamia mhimili mwingine ili kuleta ufanisi. Kazi ya serikali ni utendaji katika kuwapatia wananchi huduma za jamii na maendeleo yao kwa ujumla. Kazi za Bunge ni kutunga sheria na kuisimamia serikali katika utendaji wake. Kazi ya mahakama ni kutafsiri sheria na kutoa haki;

(c) Kuweka sheria na taasisi za kutetea na kuendeleza haki za binadamu ili kuzuia ukiukwaji na kuwezesha kila mtu kupata haki yake kwa mujibu wa sheria;

(d) Kuruhusu jumuiya, asasi binafsi kushiriki na kutoa changamoto kwa serikali dhidi ya vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka;

(e) Kupambana vikali na rushwa na ufisadi katika taasisi, mashirika yake na katika miradi mbalimbali ya maendeleo ili wananchi wake wapate huduma muhimu kwa usawa na bila upendeleo; na

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Kuhakikisha kuwa rasilimali za taifa zinatumika kwa usawa, kwa manufaa ya wananchi wote na sio kutumiwa na mtu au kikundi cha watu wachache kwa masilahi binafsi.

## Zoezi la 6

1. Ni mambo gani ambayo asasi au jumuiya za kiraia hupigania katika jamii?
2. Katika nchi ya kidemokrasia, katiba ina umuhimu gani?
3. Taja njia nne za kukuza utawala bora nchini Tanzania.

## Kazi ya kufanya namba 6



Jadiliana na wenzako madhara yatakayojitokeza endapo serikali itashindwa kutekeleza wajibu wake katika kukuza misingi ya utawala bora. Andika majibu uliyoyapata katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 7

**A:** *Oanisha kipengele kutoka* ***Sehemu A*** *na kipengele kutoka* ***Sehemu B****, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Ni msingi wa kidemokrasia ambapo watu wapo huru kuzungumza bila kuingiliwa | (a) Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| 2. Wananchi wote wapo huru kujiunga na vyama vya siasa na kuchaguliwa | (b) kiongozi bora |
| 3. Chombo chenye jukumu la kumtangaza mshindi wa nafasi ya urais | (c) haki za binadamu |
| 4. Anajituma kwa waliompa nafasi aliyonayo | (d) uhuru wa kujieleza |
| 5. Kila mtu ana haki ya kuishi na kupata elimu | (e) uwazi na uwajibikaji |
| | (f) uwepo wa vyama vingi vya siasa |
| | (g) usawa |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 44 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

6. Kiongozi anayepatikana kwa njia ya kidemokrasia ana sifa zifuatazo, isipokuwa**:**
   (a) anafuata utawala wa sheria
   (b) anakubali kukosolewa
   (c) anaheshimu mawazo ya waliomchagua tu
   (d) anatumikia watu wote

7. Mfumo wa vyama vingi vya siasa una manufaa yafuatayo:
   (a) unaweza kuwagawa wananchi kwa itikadi
   (b) viongozi wa vyama wanaweza kuteua mgombea asiyekubalika
   (c) wananchi wana haki ya kujiunga na vyama wanavyovitaka
   (d) vyama vyote vinapata ruzuku

8. Zifuatazo ni haki za binadamu isipokuwa:
   (a) kuishi popote bila kubughudhiwa
   (b) kupata elimu
   (c) kufanya kampeni za uchaguzi
   (d) uhuru wa kuwa na familia

9. Mojawapo ni hatua ya kumpata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:
   (a) kuteuliwa na wananchi wa jimbo lake
   (b) kupendekezwa na marafiki zake
   (c) kuteuliwa na chama chake
   (d) kupendekezwa na Bunge

10. Uvumilivu wa kisiasa ni msingi wa demokrasia kwa sababu:
   (a) unawapa watu ushindi wa kura bila kampeni
   (b) unasaidia kunyamazisha walioshindwa uchaguzi
   (c) unaleta kuelewana kwa pande zinazopingana kiitikadi
   (d) unafurahisha wahisani

**C:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

11. Demokrasia ni utawala wa watu ambapo watawala hutawala kwa ridhaa ya watu.________

12. Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huchaguliwa kwanza katika vyama kabla ya uchaguzi wa kitaifa kufanyika.________

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 45 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

13. Kiongozi bora anapokea maagizo kutoka ngazi za juu za uongozi na kuyatekeleza pasipo wahusika kushirikishwa.________

14. Katika demokrasia mawazo ya wachache yanastahili kusikilizwa pia.________

15. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuchaguliwa huapishwa na Bunge.________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Asasi | chombo kikubwa kama vile shirika linalohusika na utoaji wa huduma kwa watu katika jamii |
| Haki | stahili ya mtu kupata |
| Utawala | hali ya uendeshaji wa mamlaka ya serikali |
| Wajibu | jambo ambalo mtu analazimika kulifanya |
| Weledi | hali ya kuwa na maarifa makubwa kuhusiana na kitu au jambo fulani |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 46 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kujali watu wengine

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kutambua na kuepuka vitendo visivyodumisha amani nyumbani na shuleni. Pia, ulijifunza kukemea na kutoa taarifa za vitendo visivyokubalika. Vilevile, ulijifunza kushiriki shughuli za maendeleo ya familia na kuleta uhusiano mzuri katika jamii. Aidha, ulijifunza kukuza uhusiano bora na majirani na kushiriki katika kutatua matatizo. Katika sura hii, utajifunza kutenda vitendo vinavyowavutia wenzako, kujiepusha na tabia hatarishi na kuwatanguliza watu wenye mahitaji maalumu na uhitaji wa haraka kupata huduma. Pia utajifunza kuomba unasihi pale unapohitajika na kutenda vitendo vinavyoonesha usawa. Umahiri huu utakuwezesha kutenda vitendo vinavyokubalika katika jamii, kuepuka tabia hatarishi na kuhamasisha wenzako kutenda matendo ya tabia njema. Pia, utaweza kudumisha usawa na kutoa huduma ya haraka kwa watu wenye uhitaji*.

### Vitendo vinavyowavutia wenzako kujiepusha na tabia hatarishi

Tabia hatarishi ni vitendo ambavyo tunavifanya na mwishowe vinatuingiza katika matatizo ya kiafya, kijamii na kiuchumi. Tabia hatarishi zina madhara kwa jamii na husababisha ukosefu wa usalama wa watu na mali zao. Kuwajali wengine ni pamoja na kuwaepusha dhidi ya tabia hatarishi. Hii huwezekana kama tunajenga tabia ya kuwasiliana na wenzetu na kuhakikisha kuwa tunawasaidia ili waweze kujiepusha na tabia hatarishi.

Tunapowasiliana na wenzetu ni vyema tuyafahamu maisha wanayoyapitia ili kujua namna ya kuwasaidia bila kuhatarisha maisha yao. Vitendo vinavyowavutia watu kuachana na tabia hatarishi huwajenga na kuwawezesha kuwa na heshima na tabia njema. Vitendo hivyo ni kama kushiriki katika michezo, kushiriki katika imani za kidini, na kuisaidia jamii. Tabia nyingine ni kujiepusha na makundirika hatarishi, kuhudhuria masomo shuleni na kuwa na huruma kwa wengine.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Lusi na Regina ni wasichana wanaosoma Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Kisiwani. Marafiki hawa hutoka pamoja nyumbani kwao kila waendapo shuleni ambako ni umbali wa kilometa tano. Pamoja na umbali wa shule, watoto hao wamekuwa na jitihada ya kuwahi shuleni na mara baada ya masomo hurudi nyumbani pamoja. Siku moja Lusi aliugua na kushindwa kwenda shuleni. Wazazi wake walimpeleka hospitalini kwa ajili ya kupata matibabu. Baada ya kufanyiwa vipimo, Lusi alikutwa na malaria kali na daktari aliamuru alazwe. Lusi alilazwa hospitali kwa muda wa siku tatu. Baada ya kutoka hospitali, Lusi alitakiwa kupumzika nyumbani kwa siku nne.

Wakati wa ugonjwa wa Lusi, Regina alikwenda shuleni na kurudi nyumbani peke yake. Siku moja wakati akirudi nyumbani alikutana na kijana aliyekuwa akiendesha bodaboda. Kijana huyo alisimama na kumsalimia Regina. Regina aliendelea na safari yake, lakini yule kijana alimfuata akimwambia ampe lifti. Regina alikataa na yule kijana akaondoka. Siku iliyofuata yule kijana alipita na bodaboda yake na alipomwona Regina akasimama. Akajitambulisha kwake kuwa anaitwa Sele. Alimsihi Regina apande bodaboda ili amuwahishe nyumbani. Kwa kuwa Regina alikuwa amechoka, alikubali akapanda na Sele akamshusha karibu na nyumbani kwao. Siku iliyofuata Sele alipita tena na kumkuta Regina akirudi nyumbani na kumsihi apande bodaboda. Regina alikubali na akashushwa karibu na nyumbani kwao. Regina aliendelea na mtindo huu kila jioni na Sele hakuwahi kumdai nauli yoyote.

Lusi alipona malaria na akaanza masomo yake tena. Asubuhi waliondoka na Regina kwenda shuleni. Jioni walipokuwa wakirudi nyumbani, Sele akapita na bodaboda yake ili amchukue Regina. Alipowakuta na Lusi alijaribu kumshawishi na Lusi ili wote wapande awarudishe nyumbani. Regina alitaka kupanda lakini Lusi alimkataza. Sele alijaribu kuwashawishi wote wapande, lakini baada ya muda Regina naye alimsikiliza rafiki yake na hakupanda ile bodaboda. Hatimaye Sele aliondoka na kuwaacha marafiki hawa.

Baada ya hapo, Lusi alimsihi Regina kuacha kabisa tabia ya kupenda lifti hasa kwa watu asiowajua kwani inaweza kumuingiza katika mazingira hatarishi. Alimsihi kuwa yule kijana angeweza kuhatarisha maisha na masomo yake kwa kumrubuni kwa lifti. Alizungumzia hatari ya kujiingiza katika tabia za ngonozembe, tabia ambazo zinaweza kumsababishia mimba au magonjwa ya zinaa kama vile UKIMWI na kaswende. Pia, angeweza kudhurika mwili wake kwa kujeruhiwa au kuumizwa.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sele alipita tena kesho yake na alipowakuta Lusi na Regina alisimama. Regina alimuonya kuwa asiendelee kuwafuata tena vinginevyo atawajulisha wazazi wake. Baada ya kuona hivyo, Sele hakurudia tena kuwafuata. Alipofika nyumbani, Regina aliwaeleza wazazi wake kuhusu tabia ya Sele. Wazazi wa Regina walimshukuru Lusi kwa ushauri alioutoa kwa mtoto wao.

## Zoezi la 1

1. Unafikiri nia kubwa ya Sele kwa Regina ilikuwa nini?
2. Je, Lusi ameonesha tabia gani?
3. Ni mambo gani yangemtokea Regina kama asingemsikiliza Lusi?
4. Ni ushauri gani mwingine ungeweza kumpa Regina zaidi ya ule aliopewa na Lusi?
5. Je, umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

## Kazi ya kufanya namba 1

Andika faida tano za kujiepusha na tabia hatarishi katika maisha. Andika faida hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Hasara atakazopata mtu anayejihusisha na vitendo hatarishi

Vitendo hatarishi kama vile ulevi wa pombe, kuuza na kutumia dawa za kulevya, kushiriki ngonozembe, ugomvi na ubaguzi katika familia, kushiriki katika wizi na ujambazi, huweza kusababisha hasara kubwa kwa mtu anayevitenda na pengine kwa jamii nzima inayomzunguka. Hasara hizo ni kama zifuatazo:

(a) Kupata maradhi na hata kifo kwa mtu anayeshiriki ngonozembe, ulevi, ujambazi na kutumia dawa za kulevya;

(b) Kusababisha uharibifu wa mali za familia na za umma kutokana na ulevi wa kupindukia. Ulevi unaweza kusababisha uuzaji wa mali za familia na hata za umma ili kupata pesa za kutumia;

(c) Mtu anayetumia dawa za kulevya mara nyingi hukosa makazi bora ya familia yake, hukosa marafiki wa kweli na kukosa kuheshimiwa na familia yake na hata jamii inayomzunguka; na

(d) Mara nyingi mtumiaji wa dawa za kulevya, huwa mgomvi na hali hiyo huweza kumsababisha apate majeraha na ulemavu wa kudumu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 49 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Tega na Kizenga ni marafiki wanaosoma Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Bombambili. Mara nyingi wao huenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja. Kizenga ni mwanafunzi mtukutu. Njiani wakati wa kwenda na kurudi shuleni hupenda kuchezea vitu hatarishi kama vile, nyaya za umeme zinazoning'inia, makopo machafu na kucheza kwenye madimbwi ya maji machafu. Siku moja wakiwa njiani, Kizenga aliona nyoka mkubwa akikatisha katikati ya barabara. Tega aliogopa sana, hakutaka kupita tena eneo lile lakini Kizenga aliokota jiwe na kuelekea alipopita nyoka ili ampige kwa jiwe.

Tega alimuonya rafiki yake, asimpige nyoka kwani anaweza kumuuma na hatimaye kumsababishia kifo kutokana na kuwa na sumu kali. Hata hivyo, Kizenga hakusikia, akaendelea kumfuata huyo nyoka vichakani. Nyoka alipohisi vishindo alijificha. Kizenga alipomkaribia, nyoka aliruka na kumuuma mguuni. Kizenga alipata maumivu makali na kuanza kulia huku akimuita rafiki yake Tega amsaidie. Tega alipofika alimsogeza pembeni mwa barabara na kumpa huduma ya kwanza kwa kumfunga kamba mguu uliong'atwa na nyoka ili sumu isisambae mwilini. Tega aliomba msaada kwa wapita njia wamsaidie kumpeleka Kizenga hospitalini. Familia ya Kizenga ilimshukuru sana Tega kwa kumsaidia rafiki yake na kumfikisha hospitalini mapema. Kizenga alitibiwa kwa gharama kubwa sana hadi kupona kwake.

## Zoezi la 2

1. Tega na Kizenga wanasoma shule gani?
2. Katika habari uliyoisoma, nani hakuwa na maadili mazuri? Kwa nini?
3. Je, ni vitendo gani hatarishi alivyovifanya Kizenga katika habari hii?
4. Ni sababu gani iliyomfanya Tega kumfunga mguu Kizenga?
5. Umejifunza nini kutokana na habari hii?

## Kazi ya kufanya namba 2

Andika vitendo vitano ambavyo ni hatarishi vinavyotendwa na wanafunzi wenzako shuleni kwako. Andika vitendo hivyo katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kuwatanguliza watu wenye mahitaji maalumu na uhitaji wa haraka kupata huduma

Utoaji wa huduma kwa jamii uzingatie kwa kuanza na watu wenye mahitaji maalumu na wale wenye uhitaji wa haraka. Kwa kufanya hivyo huonesha hali ya kuwajali, kuwaheshimu na kuwathamini wenzetu wenye mahitaji maalumu na wenye uhitaji wa haraka. Baadhi ya watu wenye mahitaji maalumu na wale wenye uhitaji wa haraka katika jamii ni wazee, watoto, wagonjwa mahututi, walemavu wa aina mbalimbali, wajawazito na watu waliobeba watoto wachanga.

Katika nchi yetu, huduma nyingi za jamii hutolewa kwa watu kupanga foleni. Mfano wa huduma hizo ni huduma za hospitali, uandikishwaji wa wapiga kura, kupiga kura, huduma za benki na huduma mbalimbali katika maeneo ya shuleni. Tunapokuwa kwenye foleni ya kupata huduma mbalimbali za kijamii ni vyema tuwapishe watu wenye uhitaji wa haraka na wale wenye mahitaji maalumu. Mfano iwapo upo katika foleni ya kupata huduma hospitalini na iwapo nyuma yako kuna mama mwenye mtoto mchanga, mpishe mama huyo atangulie na kupata huduma kabla yako au watu wengine waliopo kwenye foleni.

### Zoezi la 3

1. Je, kuna umuhimu gani wa kuwatanguliza watu wenye mahitaji maalumu na uhitaji wa haraka kupata huduma za jamii?
2. Taja watu wanaostahili kutangulizwa katika utoaji wa huduma za jamii.
3. Taja sababu moja ya kumpisha mgonjwa mahututi kupata huduma ya matibabu kabla ya watu wengine.

### Kazi ya kufanya namba 3

Andika katika daftari lako la mazoezi maeneo mengine matano tofauti na hayo uliyoyasoma ambapo watu wenye uhitaji wa haraka wanatakiwa kuhudumiwa kwanza kabla ya wengine.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 51 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Unasihi

Unasihi ni mazungumzo yanayoongozwa na mtu mwenye ujuzi, utaalamu na uzoefu wa kusikiliza na kutoa mwongozo wa namna ya kutatua tatizo la mtu au kikundi cha watu katika jamii. Huduma hii huhitaji pande mbili yaani mshauri na mshauriwa. Pia, huhitaji chumba au eneo maalumu lenye utulivu kwa ajili ya kutolea huduma hii muhimu kwa jamii.

### Umuhimu wa kupata huduma ya unasihi

Huduma ya unasihi ni muhimu kwa sababu zifuatazo:

(a) Huwawezesha watu kujitambua na kujiongoza;
(b) Huwajengea watu uwezo wa kujitambua katika kukua kwao;
(c) Huwafanya watu wajirekebishe kimwenendo ili wakubalike katika jamii;
(d) Huwawezesha watu kuwa na mwelekeo mzuri kitaaluma na hatimaye kuwa na kiwango cha juu cha kujifunza;
(e) Huwawezesha watu kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha; na
(f) Huwasaidia watu kuishi vizuri na jamii zenye tamaduni tofauti.

### Zoezi la 4

1. Eleza maana ya unasihi.
2. Je, umewahi kupata huduma ya unasihi shuleni kwako?
3. Unasihi huo ulikuwa unahusu nini?
4. Kwa nini kuna umuhimu wa kupata unasihi?
5. Unafikiri ni kwa nini huduma ya unasihi huhitaji eneo au chumba maalumu?

### Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wenzako umuhimu wa kuwepo kwa huduma ya unasihi shuleni. Kisha orodhesha sehemu zingine ambazo huduma hii ya unasihi inaweza kutolewa. Andika mlichojadili katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 52 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Unasihi katika kukabiliana na vikwazo vya kitaaluma**

Katika mazingira ya kujifunza kuna vikwazo mbalimbali vinavyowakabili wanafunzi katika kujifunza kwao. Unasihi unahitajika ili kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na vikwazo hivyo.Vifuatavyo ni baadhi ya vikwazo vya kitaaluma vinavyohitaji unasihi:

***Kushindwa masomo:*** Unasihi unahitajika ili kuwarudishia matumaini wanafunzi walioshindwa kufanya vizuri katika masomo yao na kuwajenga kisaikolojia ili wasikate tamaa.

***Kukosa mbinu sahihi za kujifunza:*** Unasihi unahitajika ili kuwawezesha wanafunzi kupata mbinu za kujifunza na kuwaepusha kusoma bila mpango. Kwa mfano, namna ya kuweka ratiba ya kujisomea, matumizi sahihi ya muda, na kusoma kwa vikundi.

***Kukosa mahitaji muhimu ya shule:*** Katika jamii kuna baadhi ya watu ambao kutokana na hali zao duni za kimaisha au mitazamo, hushindwa kuwapatia watoto wao mahitaji ya shule kwa wakati. Wanafunzi wanaotoka katika kundi hili huhitaji unasihi ili wasikate tamaa katika masomo yao.

***Hofu ya mitihani:*** Mara nyingi mitihani inapofanyika mwanafunzi hupata hofu au homa ya mtihani, hivyo unasihi husaidia kumjengea mwanafunzi ujasiri katika kujiandaa na kufanya mitihani bila hofu.

***Masuala mtambuka:*** Unasihi ni muhimu ili kukabiliana na masuala mtambuka katika jamii. Baadhi ya masuala mtambuka ni dawa za kulevya, rushwa, ugonjwa wa UKIMWI na utandawazi.

***Changamoto katika mawasiliano:*** Mawasiliano katika upashanaji habari yamekua na kuenea na kufanya dunia kuwa kama kijiji. Hivyo, unasihi unahitajika ili kuwapa wanafunzi muongozo wa matumizi sahihi ya vyombo vya mawasiliano kama vile simu za mkononi, ili kuepuka kujiingiza katika tabia hatarishi.

***Kukosa tabia shupavu:*** Mwanafunzi anahitaji unasihi ili kumjengea uwezo wa kuamua jambo katika kukabiliana na mazingira yanayotatanisha, hali hiyo huitwa tabia shupavu. Unasihi unamsaidia mwanafunzi kujitambua na kufanya uamuzi kutokana na hali halisi. Vilevile, humsaidia kuchunguza matarajio ya maamuzi yake na namna ya kutekeleza uamuzi huo ili asiathirike katika masomo. Kwa mfano, jinsi ya kukabiliana na vijana wakware na magenge ya uvutaji bangi katika jamii.

FOR ONLINE USE ONLY




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 53 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Eleza kwa kifupi maana ya tabia shupavu.
2. Taja mambo matano yanayohitaji unasihi katika taaluma.
3. Kuna faida gani ya kupata unasihi katika masomo shuleni?
4. Je, unafikiri ni kwa nini wanafunzi hupata hofu ya mtihani?

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wenzako namna unasihi unavyokusaidia katika maisha ya shuleni. Andika mlichojadili kwenye daftari lako la mazoezi.

### Unasihi katika kukabiliana na matatizo ya kijamii

Jamii yoyote ile hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Matatizo ya kijamii yanaweza kugawanywa katika nyanja mbalimbali kama vile za kimaadili, kisaikolojia, kisiasa na kiuchumi. Katika jamii kuna taasisi au watu wenye uzoefu na taaluma za kutoa unasihi. Watu hawa hutumiwa na jamii katika huduma ya unasihi na kuiwezesha jamii husika kukabiliana na matatizo yanayowakabili.

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Mwalimu:** Leo hii tumepata bahati ya kutembelewa na Mnasihi. Napenda kutumia fursa hii kumkaribisha azungumze nasi. Karibu mnasihi!

**Mnasihi:** Asante sana mwalimu, vijana safiii!

**Wanafunzi wote:** Safiii!

**Mnasihi:** Asante sana.Tumekutana hapa kushauriana kuhusu mmomonyoko wa maadili katika jamii. Mnaelewa nini kuhusu mmomonyoko wa maadili?

**Mwanafunzi wa 1:** Mmomonyoko wa maadili ni tabia ya watu kutenda vitendo visivyokuwa na heshima mbele ya jamii.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mnasihi:** Ni vitendo gani hivyo vinavyochangia kusiwepo na heshima katika jamii yetu?

**Mwanafunzi wa 2:** Vitendo hivyo ni pamoja na uvutaji bangi, ulevi wa pombe, mavazi yasiyokuwa na staha, uzinzi na kutumia lugha ya matusi.

**Mnasihi:** Mnadhani nini kifanyike ili kuondoa tatizo hili?

**Mwanafunzi wa 3:** Tunaomba kusikia kutoka kwako kwani vijana wanapelekwa mahabusu lakini hawabadiliki.

**Mnasihi:** Sawasawa! Kwanza kabisa ni kweli kuwa mmomonyoko wa maadili husababishwa na mambo mliyoyataja. Hivyo, tunapaswa kukabiliana na vitendo hivyo ili kuondoa hali hii. Pili, tunapaswa kufahamu madhara ya vitendo vinavyosababisha mmomonyoko wa maadili. Kwa mfano, uvutaji bangi husababisha ugomvi, vurugu, hasira, uamuzi usiokuwa na busara. Ulevi wa pombe unaweza kusababisha kukosa heshima, kutukana, vurugu, kutumia fedha vibaya na kukosesha familia amani. Mavazi yasiyo staha husababisha mtu kuhusishwa na vitendo viovu kama vile wizi, ngonozembe na kukosa heshima mbele ya jamii.

**Mwanafunzi wa 4:** Tunashukuru sana Mnasihi. Je, tunawezaje kuepukana na madhara ya hali hii?

**Mnasihi:** Swali zuri sana! Kwanza kabisa tunapaswa kujitambua na kukubali kuacha vitendo visivyofaa katika jamii. Pili, kutoa ushauri kwa wanafunzi wenzenu kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali wa ushauri. Tatu, kuvichukia vitendo hivi kwa kuvikemea hadharani. Nne, kutii na kufuata mafundisho ya dini. Kuunda vikundi vya vijana kulingana na rika na kuzungumzia suala hili. Tano, jamii nzima kuhamasishwa ili kupambana na suala hili katika shughuli mbalimbali za kijamii.

**Mwanafunzi wa 5:** Tunakushukuru sana kwa ushauri wako mzuri, tunapenda kukukaribisha tena shuleni kwetu.

**Mwalimu:** Tunashukuru sana kwa ushauri wako mzuri kwa wanafunzi wetu, tunakukaribisha tena shuleni kwetu.

**Mnasihi:** Asanteni, nami nashukuru kwa ushirikiano mzuri.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

1. Ni nini malengo ya mazungumzo haya?
2. Ni mambo gani katika mazungumzo haya yanahitaji unasihi?
3. Unafikiri katika jamii unamoishi ni mambo yapi yanahitaji unasihi?
4. Ni kundi gani linaloathirika sana kimaadili katika jamii?
5. Njia gani zitumike ili kurekebisha maadili katika jamii?

## Kazi ya kufanya namba 6



Shirikiana na wenzako kuandaa igizodhima kuonesha umuhimu wa kuwapa unasihi wanafunzi kabla ya kuanza mitihani yao. Igizo hilo lifanyike darasani wakati wa kipindi.

### Vitendo vinavyoonesha usawa katika maisha

Ni muhimu kutenda vitendo vinavyoonesha usawa kwa watu wengine bila kujali jinsi, kipato au nasaba ya mtu. Inafaa kujenga uhusiano chanya kati ya watu kwa kutambua mipaka ya uhusiano huo na umuhimu wa kuthamini utu wa watu wengine.

Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Juma na Roza ni watoto wa familia moja wanasoma katika Shule ya Msingi Majohe. Wazazi wa Juma na Roza ni wakulima ambao muda mwingi hushinda shambani wakilima. Juma na Roza wakitoka shuleni husaidiana kufanya kazi zote za nyumbani kwa pamoja kama vile, kupika, kulisha mifugo, kufagia uwanja, kufua nguo zao na za wadogo wao, kuosha vyombo na kumwagilia bustani.*

*Siku moja wazazi wao waliwaambia kuwa, katika maisha yao ya kila siku inatakiwa kufanya kazi zote kwa usawa bila kujali jinsi, umri au kipato cha mtu. Vilevile, wanatakiwa kuthamini makundi maalumu ya watu katika jamii kama vile wazee, watoto, wajawazito, wagonjwa na walemavu. Kutenda vitendo hivyo kutaonesha wanayajali na kuyathamini makundi hayo. Kwa mfano, kuwapa kipaumbele watu kwenye kupata huduma za kijamii kama*



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 56 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*vile, kuingia na kutoka katika vyombo vya usafiri, hospitalini, benki na kupewa nafasi ya upendeleo ya kupiga kura kwa wakati kipindi cha uchaguzi.*

*Pia, kuwapenda, kuwaheshimu na kuwashirikisha katika kujadili na kutoa maamuzi katika masuala ya kifamilia na kitaifa. Baada ya kupata maelezo hayo kutoka kwa wazazi wao walikuwa na ari zaidi na nguvu mpya ya kusaidiana kutekeleza majukumu yao ya nyumbani na shuleni kwa usawa.*

## Zoezi la 7

1. Orodhesha watu wenye uhitaji maalumu katika jamii.
2. Ni kwa namna gani utaonesha kuyathamini makundi maalumu katika jamii?
3. Vitendo gani vya usawa wanavyovionesha Juma na Roza katika kutekeleza majukumu yao nyumbani?
4. Orodhesha kazi zinazofanywa kwa ushirikiano kati ya wanaume na wanawake katika jamii yenu.

## Kazi ya kufanya namba 7

Bainisha kazi zinazofanywa na wanafunzi shuleni kwako kwa kuzingatia usawa wa jinsi, kisha ziandike kazi hizo katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 57 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

**A:** *Katika jedwali lifuatalo, oanisha kipengele kutoka* ***Sehemu A*** *na kipengele kutoka* ***Sehemu B,*** *kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| ***Tabia isiyofaa*** | ***Maelezo ya tabia*** |
| 1. Kulewa pombe | (a) tabia hatarishi ya kuwatumikisha watoto wadogo katika kazi ngumu |
| 2. Wizi au ujambazi | (b) ujauzito kutokana na kujiingiza katika ngono kabla ya kufikia umri wa utu uzima |
| 3. Utoro shuleni | (c) matumizi ya kilevi yanayoweza kuathiri afya za watumiaji wa pombe |
| 4. Ajira za utotoni | (d) tabia hatarishi ya kuchukua kwa nguvu na bila ridhaa mali isiyo yako |
| 5. Mimba za utotoni | (e) tabia ya kutohudhuria masomo darasani |
| | (f) kutumia dawa za kulevya |
| | (g) tabia ya kula bila mpangilio |

**B:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

6. Kipi ni miongoni mwa vitendo vinavyoonesha mtu anayejihusisha na tabia hatarishi?
   (a) kufanya kazi kwa bidii
   (b) kushiriki katika michezo
   (c) kuzurura usiku
   (d) kula na kuimba

7. Ipi kati ya zifuatazo ni hasara anayoweza kupata mtu anayejihusisha na tabia hatarishi?
   (a) kupata madhara ya kiafya
   (b) kushirikiana na marafiki
   (c) kupata heshima kwa jamii
   (d) kufanya kazi kwa ufasaha

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Lipi kati ya yafuatayo ni kundi la watu wenye uhitaji wa kuhudumiwa kwa haraka?
   (a) Viongozi wa dini, madiwani na wazee
   (b) Wagonjwa, watoto, wazee, wajawazito na walemavu
   (c) Watoto, vijana, wagonjwa na wazee
   (d) Viongozi, watoto na walimu

9. Yafuatayo ni mambo muhimu yanayoonesha usawa isipokuwa:
   (a) kuchagua na kuchaguliwa katika ngazi ya uongozi
   (b) kushirikishwa katika uamuzi
   (c) kupendelewa katika kupata huduma za jamii
   (d) kushiriki katika majadiliano

10. Tunawezaje kuwasaidia wenzetu kutohatarisha usalama wao?
   (a) kwa kuwa mfano bora kwa vitendo vyetu
   (b) kwa kuwaacha waendelee na uzembe wao
   (c) kwa kuwasifia kwa ubaya wa tabia zao
   (d) kwa kuwaingiza katika matumizi ya dawa za kulevya

**C:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

11. Kutumia dawa za kulevya ni tabia hatarishi._______

12. Ulevi hauwezi kumsababishia mtu kujihusisha na tabia hatarishi._____

13. Kupata majeraha ni moja ya hasara za kujihusisha na tabia hatarishi. _______

14. Kushiriki katika michezo kunasaidia kujiepusha na tabia hatarishi. _______

15. Tunapopata matatizo ya kukosa mahitaji muhimu si lazima kupata unasihi._______

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Nasaba | uhusiano wa mzao mmoja wa watu kutoka kizazi hadi kizazi waliokuwepo zamani na waliopo hivi sasa |
| Ukware | ashiki ya kimahaba imshikayo mtu |



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Kutunza mazingira

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza jinsi ya kuithamini jamii kwa kutathmini hali ya uharibifu wa mazingira katika eneo unaloishi. Katika sura hii, utajifunza kutathmini changamoto zinazoikabili jamii katika utunzaji wa mazingira, kuthamini uwepo wa miti ya asili na ile ya kupandwa katika mazingira yako na kubaini sheria zinazolinda mazingira. Umahiri huu utakuwezesha kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto za utunzaji wa mazingira na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutii sheria za kuhifadhi mazingira na kudhibiti vitendo hatarishi vya uharibifu wa mazingira.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Changamoto zinazoikabili jamii katika utunzaji wa mazingira

Jamii yoyote inapaswa kuelewa umuhimu wa mazingira na kuwajibika kuyatunza muda wote. Utunzaji wa mazingira yetu unahitaji tathmini ya mara kwa mara ili kukabiliana na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatavyo:

**Umaskini:** Umaskini ni hali ya mtu kushindwa kupata mahitaji yake ya kila siku kama chakula, mavazi na malazi. Umaskini wa kipato husababisha watu kujihusisha na shughuli mbalimbali zinazosababisha uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, kukata miti ovyo kwa ajili ya kuchoma mkaa, kupata kuni, uwindaji haramu, ujenzi holela na kilimo kisichozingatia utunzaji wa mazingira ili kupata kipato cha kujikimu katika maisha yao. Kukata miti ovyo husababisha maji kupungua, mito kukauka, ardhi kumomonyoka na hatimaye kusababisha ukame na jangwa.

**Kutozingatia elimu ya mazingira:** Kutozingatia elimu ya mazingira katika shughuli za kila siku kama vile uchimbaji wa madini, ukosefu wa usimamizi na mwongozo wa uchimbaji madini pamoja na kilimo na ufugaji wa kisasa. Hii husababisha uharibifu wa mimea, mmomonyoko wa udongo na ardhi kuwa na mashimo. Hii ni hatari kwa maisha ya viumbe.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 60 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Gharama za juu za nishati mbadala:** Gharama za juu za nishati mbadala kama gesi na umeme zimeifanya jamii kutumia kuni na mkaa kwa wingi hivyo kuathiri mazingira.

**Ujenzi holela:** Watu wamejenga makazi yao bila kuzingatia mipango miji hivyo kusababisha ukosefu mkubwa wa miundombinu ambayo ingerahisisha ukusanyaji wa takataka husuan katika makazi ya mjini. Pamoja na changamoto hiyo, watu hujenga karibu na vyanzo vya maji na kutiririsha maji machafu kwenye vyanzo hivyo. Hii huchangia uchafuzi wa maji na kusababisha magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu na kichocho.

**Ubovu wa miundombinu:** Miundombinu ya majitaka ikiwa michache na iliyochakaa katika eneo husika husababisha kusambaa ovyo kwa maji hayo na kuchafuka kwa mazingira katika makazi na kusababisha mlipuko wa magonjwa.

**Kutokuwashirikisha wadau:** Baadhi ya viongozi hushindwa kuwashirikisha wanajamii katika kufanya tathmini ya utunzaji wa mazingira, mipango na mikakati waliyojiwekea. Hali hii hufanya wanajamii wajione wametengwa na kutoona faida ya utunzaji wa mazingira kwao. Wengine husema kuwa, utunzaji wa mazingira ni kazi ya serikali. Dhana hii ni potofu kwa maendeleo ya jamii.

## Zoezi la 1

1. Kuna changamoto gani za utunzaji wa mazingira katika eneo unaloishi?
2. Wadau na wanajamii unamoishi wanashirikishwaje katika utunzaji wa mazingira?
3. Ni mambo gani hufanyika kuonesha vitendo vya utunzaji mazingira katika eneo unaloishi?
4. Nini kifanyike ili kuondoa changamoto zinazokabili utunzaji wa mazingira nchini?


FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 61 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wenzako njia mbalimbali zitakazotumika kuhamasisha utunzaji wa mazingira katika shule yenu. Andika mlichokijadili katika daftari lako la mazoezi.

**Umuhimu wa miti ya asili na ile ya kupandwa katika mazingira yetu**

Mazingira yetu hutupatia mahitaji yote muhimu yakiwemo chakula, maji na miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Ili tufanikiwe kupata mahitaji hayo kwa muda mrefu, inatupasa kuyatunza na kuyathamini mazingira yetu. Miti ni makazi ya viumbe wengi kama vile wanyama, ndege na wadudu. Miti huhifadhi vyanzo vya maji kama vile mito au chemchemi. Ukitembelea sehemu zenye miti ya asili utaburudishwa na sauti za ndege. Pia, utaona wadudu kama vipepeo wakiruka huku na kule. Miti husababisha mvua kunyesha na kuwepo kwa hewa safi kwa viumbe hai. Pindi mazingira yanapoharibiwa kwa ukataji miti ya asili, yatupasa kupanda miti mingine katika eneo husika ili kusaidia maisha ya viumbe wengine kuendelea.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Ihanga ni kijiji kilichopo kandokando ya mto Barali. Miaka mingi iliyopita, kijiji hiki kilikuwa na hali mbaya ya ukame kwa sababu watu wake waliharibu mazingira. Wanakijiji walikata miti ovyo kwa shughuli za ujenzi, ufugaji, uwindaji, kilimo, uvuvi, kutengeneza samani, nishati ya mkaa na kuni. Mazingira ya kijiji yalibadilika sana na maisha ya watu yalikuwa magumu kwani joto liliongezeka, mazao yalikauka na mifugo kukosa afya. Pia, baadhi ya vyanzo vya maji ya Mto Barali vilivyopo katika Mlima Nyangonje vilikauka. Siku moja mwenyekiti wa kijiji hicho aliitisha mkutano wa dharura wa wananchi wote ili kujadili hali ya ukame iliyojitokeza kijijini kwao. Baada ya majadiliano, wananchi walikubaliana kuthamini na kutunza mazingira yao ili kuepukana na ukame. Waliafikiana kupanda miti maeneo yote ya wazi na kwenye vyanzo vya maji. Vilevile, kutunza na kuweka sheria ndogondogo zitakazosaidia uhifadhi wa miti ya asili iliyopo kijijini hapo. Miaka michache baadaye, Kijiji cha Ihanga kilikuwa na miti mingi ya asili na ya kupandwa. Mvua za kutosha zilinyesha katika misimu yote na Mto Barali ulitiririsha maji ya kutosha kwa shughuli za*

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*kilimo na ufugaji kijijini hapo na katika vijiji vya jirani. Pia, maeneo ya kulisha mifugo yakawa na majani ya kutosha. Hali hiyo iliwawezesha wanakijiji wa Kijiji cha Ihanga kuvuna mazao ya kutosha kwa chakula na biashara.*

## Zoezi la 2

1. Ni tatizo gani lilikikumba Kijiji cha Ihanga kwa miaka mingi?
2. Kwa nini Mto Barali ni muhimu kwa wakazi wa Ihanga?
3. Ni shughuli gani zilizosababisha wananchi wa Ihanga kukata miti ovyo?
4. Je, baada ya majadiliano wananchi wa Ihanga walikubaliana kufanya nini?
5. Mlima Nyangonje una faida gani kwa maisha ya wananchi wa Ihanga?

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu faida ya kutunza na kuthamini miti ya asili na ya kupandwa katika maeneo mnayoishi. Andika mlichojadili katika daftari lako la mazoezi.

### Sheria zinazolinda mazingira

Tanzania ina sheria ya usimamizi wa mazingira iliyotungwa mwaka 2004 na kufuta sheria ya mazingira ya mwaka 1983. Sheria hii inabainisha kuwa ni haki ya kila mtu kuishi katika mazingira safi. Haki hii inafafanuliwa kwamba, kila mtu anayeishi Tanzania ana haki ya kuwa katika mazingira safi na salama. Haki ya kuwa na mazingira safi na salama inahusisha haki kwa kila raia kutumia mazingira yanayomzunguka kwa madhumuni ya burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na uchumi.

Haki nyingine ni ile ya kufungua madai mahakamani kuhusu uharibifu wa mazingira. Pale ambapo haki iliyoelezwa hapo juu imetishiwa kutokana na kitendo cha mtu kutotimiza wajibu kunakoweza kusababisha madhara kwa binadamu na mazingira, mtu yeyote anaweza kufungua mashtaka dhidi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 63 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya mtu huyo. Sheria hii inawawajibisha watu wanaohusika kusisimamia utunzaji wa mazingira, vilevile inamwajibisha kila mwananchi kulinda na kutunza mazingira. Kipengele cha sheria hii ya wajibu wa kulinda mazingira kinabainisha wazi kuwa, mtu yeyote anayeishi Tanzania atakuwa mdau na atawajibika kutunza na kuendeleza mazingira na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu shughuli au jambo lolote ambalo kwa kiasi kikubwa linaweza kuathiri mazingira. Sheria hii inaelekeza kuundwa kwa kamati za kudumu za miji, kata, vijiji na vitongoji zitakazowajibika katika kusimamia mazingira kikamilifu katika eneo ilimoundwa.

### Kukemea ukiukwaji wa sheria zinazolinda mazingira

Kila mwananchi mwenye mapenzi mema na mazingira katika eneo analoishi, ana wajibu wa kukemea tabia zote zinazokiuka sheria ya usimamizi wa mazingira. Miongoni mwa sheria zinazotumika katika kulinda mazingira dhidi ya uharibifu ni hizi zifuatazo:

(a) Ni marufuku kutupa takataka, au kuacha takataka kwenye nyumba, biashara, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabarani au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.

(b) Ni marufuku kwa gari lolote lililobeba takataka ngumu kuwa wazi; gari la taka ni sharti lifunikwe kiasi cha kuzuia takataka ngumu zisionekane wala kumwagika chini na kuleta adha kwa watu wanaotumia barabara. Pia kila mmiliki wa gari la abiria anapaswa kuweka chombo cha kuhifadhia takataka ndani ya gari lake. Abiria au mwenye gari yeyote haruhusiwi kutupa takataka ovyo barabarani.

(c) Ni marufuku kujisaidia ovyo haja kubwa au ndogo katika maeneo yasiyo rasmi kwa kazi hiyo. Kila mmiliki wa nyumba katika eneo lake anatakiwa kuwa na choo bora na safi kwa matumizi ya wakazi wa nyumba yake.

(d) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara ya aina yoyote kwenye maeneo ambayo hayajatengwa rasmi kwa shughuli za biashara.

(e) Ni marufuku kwa mtu yeyote kunawa, kuoga au kufua nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile, chemchemi, kisima, mto au chanzo kingine chochote cha maji, au kunywesha mifugo kwenye chanzo cha maji kinachotumika kwa matumizi ya binadamu.

(f) Kuanzia tarehe 1 Juni, 2019 serikali ilisimamia utekelezaji wa sheria inayopiga marufuku utengenezaji, usambazaji, uingizaji na matumizi ya mifuko ya plastiki nchini. Mifuko hiyo ilichangia kwa kiwango kikubwa kuchafua na kuharibu mazingira katika jamii.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 64 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Eleza namna kundirika linavyosababisha uchafuzi wa mazingira.
2. Sheria ipi inatumika kulinda na kuhifadhi mazingira nchini Tanzania?
3. Tabia zipi zinakemewa katika sheria za utunzaji wa mazingira ulizosoma katika kitabu hiki?

## Kazi ya kufanya namba 3

Baini sheria ndogo ndogo zinazokemea tabia za wanafunzi zinazosababisha uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika shule yako. Andika sheria hizo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 4

**A:** *Oanisha kipengele katika **Sehemu A** na changamoto za utunzaji wa mazingira katika kipengele **Sehemu B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Gharama za juu za nishati mbadala kama vile gesi na umeme | (a) mmomonyoko wa ardhi |
| | (b) uwindaji haramu |
| 2. Uwepo wa miundombinu mibovu ya majitaka | (c) ongezeko la gesi ukaa |
| 3. Uvuvi wa kutumia baruti | (d) mvua nyingi |
| 4. Idadi kubwa ya vyombo vya moto kama magari | (e) kutoweka kwa misitu |
| 5. Uwepo wa idadi kubwa ya mifugo katika eneo dogo | (f) mlipuko wa kipindupindu |
| | (g) uhaba wa samaki |

**B:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

6. Mazingira ya nchi yetu yameathiriwa sana na ukataji ovyo wa miti. ________
7. Utunzaji wa mazingira katika maeneo tunayoishi ni jambo muhimu na linapaswa kuwa endelevu kwa kundirika tu.________



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 65 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira (Tanzania) huhusika kusimamia mazingira katika nchi yetu.________
9. Shughuli za utunzaji wa mazingira katika nchi yetu zinategemea sana wafadhili kutoka nje.________
10. Miti husaidia kutunza vyanzo vya maji.________
11. Kugeuza takataka kuwa malighafi kama vile vyuma chakavu na chupa za plastiki ni mkakati mmojawapo wa kutunza mazingira.________
12. Elimu ya utunzaji mazingira inatakiwa kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya jamii, serikali, vyama vya siasa na madhehebu ya dini.________

**Msamiati**

Wadau — watu wenye maslahi katika shughuli fulani au jambo fulani

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 66 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kujenga uhusiano mwema na wenzako

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kushiriki shughuli za maendeleo ya familia na kuweka uhusiano mzuri katika jamii. Pia, ulijifunza kukuza uhusiano bora na jirani zako. Katika sura hii, utajifunza vitendo vinavyoashiria maelewano na wenzako, vitendo vya kudumisha urafiki mwema na wenzako na njia za kutatua migogoro miongoni mwa wanafunzi wenzako. Umahiri huu utakuwezesha kuvitambua vitendo vinavyojenga uhusiano mwema na wenzako na namna ya kuvitekeleza. Vilevile, utakusaidia kuepuka vitendo vinavyoharibu uhusiano na wenzako na kutumia mbinu mbalimbali kudumisha uhusiano ulio bora.*

### Vitendo vinavyoashiria maelewano na wenzako

Maelewano ni hali ya kukubaliana miongoni mwa watu juu ya jambo fulani ili kuwa na msimamo mmoja. Kuna vitendo mbalimbali vinavyoashiria maelewano baina ya watu katika jamii tunamoishi pamoja na shuleni. Baadhi ya vitendo vinavyoashiria maelewano ni kula, kusoma na kucheza pamoja kwa amani na upendo na kusaidiana katika shughuli mbalimbali kama misiba na sherehe. Ni vyema kwa kila mtu kutambua vitendo vinavyoashiria maelewano baina ya watu katika jamii.

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali yanayofuata.

**1**




FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 67 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2



3





URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 68 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4




**Kielelezo namba 1:** Vitendo vinavyodumisha maelewano na urafiki mwema

## Zoezi la 1

1. Je, ni vitendo gani vya kudumisha urafiki au maelewano mema na wenzako unavyoviona katika picha hizo?
2. Taja vitendo vya kudumisha urafiki au maelewano mema na wenzako unavyovifahamu tofauti na ulivyoviona katika picha hizo.
3. Taja faida mbili za kutenda kitendo kinachoonekana katika picha namba 3.

## Kazi ya kufanya namba 1

Katika daftari lako la mazoezi, andika kwa kutoa mifano ya vitendo vitano unavyofanya kila siku vinavyodumisha maelewano baina yako na familia yako.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 69 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Ushauri wenye kujenga maelewano mema na rafiki yako

Ushauri ni mawazo anayopewa mtu na mwenzake ili aweze kutatua jambo fulani. Ushauri katika maisha unatokana na mambo ambayo watu huyatenda ili kujenga uhusiano mwema. Mambo hayo ni kama vile kushirikiana, kuoneshana upendo, kusaidiana katika shida na raha, kuvumiliana, kuaminiana, na kutunziana siri.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Tumaini na Edna ni marafiki wanaosoma Shule ya Msingi Maendeleo. Tumaini anatokea kwenye familia yenye uwezo wa juu kifedha lakini Edna anatokea kwenye familia yenye uwezo duni kifedha. Pamoja na Tumaini kutokea kwenye familia yenye uwezo, hakujikweza kwa rafiki yake Edna bali alishirikiana naye kwenye masomo darasani pia katika michezo na shughuli mbalimbali za nje ya darasa.*

*Siku moja Tumaini alimwalika Edna nyumbani kwao. Akawaeleza wazazi wake kuwa, Jumamosi ijayo rafiki yake aitwaye Edna atawatembelea hivyo aliwaomba wazazi wake kuandaa chakula kizuri kwa ajili yake. Wazazi wake walikubali kwani walimpenda sana binti yao. Siku ilipowadia Edna alimtembelea rafiki yake kama walivyokubaliana. Wazazi wa Tumaini walifurahi kumfahamu rafiki wa mtoto wao na walimkaribisha kwa furaha kubwa. Edna alibeba viazi vitamu kama zawadi kwa rafiki yake Tumaini, ambaye alifurahia zawadi hiyo. Tumaini alimtambulisha Edna kwa wazazi wake na kuwaeleza kuwa Edna hushika nafasi ya kwanza katika mitihani.Tumaini alieleza kuwa Edna alimsaidia katika somo la Sayansi na Hisabati na kumfanya ashike nafasi ya tano kati ya wanafunzi sitini waliopo darasani kwao. Vilevile, alieleza kuwa Edna ndiye aliyemsaidia shuleni baada ya kudondoka katika ngazi za kuingia darasani na kumsindikiza zahanati kutibiwa. Tumaini alisema "Nampenda sana Edna."*

*Wazazi wa Edna walifurahi kwa namna Edna alivyokuwa rafiki mwema kwa binti yao Tumaini. Edna naye aliwaeleza wazazi wa Tumaini kuwa rafiki yake huwa ni mkweli, mvumilivu, ana huruma na upendo. Wakati mwingine humpa kalamu na daftari na huwa wanacheza wote na kushirikiana katika shughuli mbalimbali hapo shuleni.*

*Baba yake Tumaini alivutiwa na jinsi Edna alivyokuwa na moyo wa kutenda wema na mwenye utu. Akamwuliza kuhusu shughuli za wazazi wake. Edna akasema,"Baba yangu anafanya biashara ndogondogo na shughuli za kilimo, wakati mama yangu anajihusisha na uuzaji wa vyakula kama mama lishe." Baada ya maelezo hayo baba yake Tumaini alimwambia Edna amjulishe baba yake kuwa angependa waonane jioni ya siku hiyo. Mama yake Tumaini naye*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*akasema,"Wewe ni mtoto mwema na mwenye moyo wa pekee na hofu ya Mungu. Unafaa kuigwa kwa wema wako na karibu tena nyumbani kwetu Edna".*

*Jioni ilipofika baba yake Edna alifika nyumbani kwa akina Tumaini na kumkuta baba yake Tumaini na alimkaribisha vizuri. Walizungumza mambo mengi ya maisha na jinsi watoto wao wanavyopendana na kushirikiana shuleni. Baba Tumaini alimweleza jinsi alivyofurahishwa na wema wa Edna kwa binti yake. Pia, alimweleza baba yake Edna kuwa amemwita ili amwongezee mtaji wa biashara na kumshauri afungue duka la bidhaa za nyumbani.*


*Baba Edna alifurahi na kushukuru kwa msaada aliopewa. Baada ya miezi sita kupita, baba Edna alikuwa na duka kubwa la bidhaa za nyumbani na aliuza vinywaji kwa bei ya jumla. Maisha ya familia yake yalibadilika na aliweza kujikimu kiuchumi na kusaidia watu wengine.*

*Maendeleo mazuri ya baba Edna yalimfurahisha sana baba Tumaini na familia yake. Edna na Tumaini walifurahi sana na walidumu kama marafiki wakiamini kuwa, udugu ni kufaana katika shida na raha. Wanafurahia kuwa urafiki wao umeleta manufaa kwa familia zote mbili na katika jamii.*

## Zoezi la 2

1. Kisa hiki kinakufundisha nini?
2. Je, ili kujenga urafiki mwema na maelewano inatupasa kufanya nini?
3. Je, unafikiri ni kwa nini urafiki wa Tumaini na Edna unafaa kuigwa?
4. Kuna umuhimu gani wa kuwa na rafiki mwema katika maisha yetu?
5. Kitendo cha baba Tumaini cha kumwongezea mtaji baba Edna kinakufundisha nini?

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako faida tano za kujenga urafiki mwema shuleni. Kisha andika faida hizo katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 71 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Vitendo vya kudumisha urafiki mwema katika jamii

Urafiki ni uhusiano unaofaa kati ya mtu mmoja na mwingine. Zipo njia nyingi za kujenga na kudumisha urafiki katika jamii. Njia hizo ni pamoja na kushiriki mashindano mbalimbali ya kucheza pamoja, kutoa huduma muhimu katika jamii, mfano, maji, chakula, na matibabu. Njia nyingine ni kwa kusoma na kufanya kazi pamoja, kushiriki katika matukio ya kijamii kama vile harusi, hitima na misiba.

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Nyangasada ni kijiji chenye ardhi nzuri yenye rutuba na hupata mvua za kutosha kila msimu wa kilimo. Kijiji hiki kina watu wachache wanaoishi kwa upendo na kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kila siku. Katika kijiji hicho kuna mzee mmoja maarufu aitwaye Ngullo. Mzee Ngullo ni mkulima mkubwa wa mazao ya mahindi, mpunga, maharage na alizeti. Pia, anafuga ng'ombe, mbuzi na kuku. Kipindi cha kuvuna mazao mzee Ngullo huwaalika wanakijiji wenzake kumsaidia kuvuna mazao yao. Baada ya kumaliza kazi ya kuvuna, wanakijiji hufurahi pamoja na familia ya mzee Ngullo kwa kula chakula na kunywa vinywaji alivyowaandalia. Pia, mzee Ngullo humshukuru kila mwanakijiji aliyeshiriki katika kazi ya kuvuna kwa kumgawia debe mbili za mahindi na mpunga, lita tano za maziwa na za mafuta ya alizeti. Wanakijiji wanaipenda sana familia ya mzee Ngullo kutokana na upendo wanaouonesha.

### Zoezi la 3

1. Taja sifa mbili za Kijiji cha Nyangasada.
2. Mzee Ngullo hulima mazao gani?
3. Kwa nini wanakijiji wa Nyangasada wanaipenda familia ya mzee Ngullo?
4. Je, unapata fundisho gani baada ya kusoma habari hii?

### Kazi ya kufanya namba 3

Andika katika daftari lako la mazoezi vitendo vitatu utakavyovifanya ili kudumisha urafiki mwema katika jamii unamoishi.

### Ushiriki katika matukio ya kijamii

Kila siku familia na jamii zetu zinapita katika matukio yenye kugusa maisha ya watu wengi. Matukio kama sherehe, misiba, michezo na majanga hugusa maisha ya wengi. Tunapaswa kuheshimu na kujitolea katika wakati wa shida na wakati wa furaha. Jamii inapokuwa na furaha watu huwa na furaha. Vilevile janga la mtu mmoja huwa ni huzuni ya wengi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 72 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yafuatayo.

*Katika Kijiji cha Msisimo watu wengi hujihusisha na kilimo hasa cha zao la mpunga. Kijiji hiki kipo katika bonde la mto mkubwa uitwao Mto Sisimo ambao ndipo shughuli za kilimo hufanyika. Zaidi ya kulima mpunga, wanakijiji hufuga mifugo kama kuku, mbuzi, ng'ombe, na bata. Wakulima hutegemea kilimo cha mbogamboga ambacho hufanyika wakati wa kiangazi baada ya kuvuna mpunga. Maisha ya wanakijiji hutegemea sana uwepo wa Mto Sisimo. Wakati wa kiangazi maji hupungua na wanakijiji huchimba mifereji ambayo hutumika kwa umwagiliaji wa bustani za mbogamboga. Kutokana na umuhimu wa mto huo, wanakijiji husema Mto Sisimo ni uhai wao.*

*Mwaka huu mvua zilinyesha kwa kiwango kikubwa sana. Wananchi hawakuwa na tahadhari ili kujiandaa na hali ya mvua. Hivyo, mvua zilisababisha kuongezeka kwa maji katika Mto Sisimo na kusababisha mafuriko. Maji kutoka katika mto yalirudi katika mashamba ya mpunga na kuyaharibu mashamba kijijini. Wanakijiji waliokuwa na nyumba karibu na mto waliathirika kwani nyumba zao na vyakula vilisombwa na maji. Shule ya Msingi ya Msisimo iliharibika, baadhi ya madarasa yalibomoka na wanafunzi hawakuweza kwenda shuleni. Hali ilikuwa ya taabu na watu walihitaji msaada wa makazi, malazi, na chakula.*

*Mwenyekiti wa Kijiji Mzee Maarifa, aliwasiliana na viongozi wa vijiji vya jirani, wa kata na wilaya kwa ajili ya kuomba msaada. Wanakijiji wa kijiji jirani na Kijiji cha Msisimo walifika kujitolea kuwasaidia wenzao. Pia, walileta vyakula, nguo, dawa na maji safi ya kunywa. Uongozi wa wilaya ulifika na wataalamu wa afya walitoa huduma za matibabu kwa waliopata maradhi au madhara ya kiafya. Pia, uongozi wa wilaya ulisaidia kukarabati madarasa yaliyobomoka.*

*Baada ya muda, wanakijiji wa Msisimo walirudia maisha yao ya kawaida. Shule ya Msingi Msisimo ilifunguliwa na wanafunzi waliendelea na masomo. Mwenyekiti aliitisha mkutano na kuwashukuru majirani zao kwa msaada walioutoa. Pia, aliandika barua ya shukrani kwa uongozi wa wilaya kwa msaada waliotoa.*

## Zoezi la 4

1. Ni matukio gani ya kijamii uliyosoma katika kisa hiki?
2. Je, ni matukio gani mengine ya kijamii unayoyafahamu katika mazingira unayoishi?
3. Je, ungekuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Msisimo, ungechukua hatua gani kukabiliana na tatizo lililotokea?
4. Ni tahadhari gani wanakijiji walipaswa kuwanayo?

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 73 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 4

Andika katika daftari lako la mazoezi tukio lolote la kijamii ulilowahi kushiriki katika eneo unaloishi, kisha wasimulie wenzako.

### Kutatua migogoro mbalimbali miongoni mwa jamii

Mgogoro ni hali ya kutoafikiana inayosababisha ugomvi baina ya pande mbili au zaidi. Katika jamii, migogoro hutokana na mtu au kikundi cha watu kutotenda haki kwa wengine katika masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, na kiimani. Migogoro huleta ugomvi na mfarakano katika jamii, hivyo hatuna budi kutatua migogoro mapema ili kuzuia migogoro hiyo kukua na kusababisha vurugu na maafa.

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kitongoji cha Bondeni kipo karibu na msitu wa asili pia kimepakana na msitu wa kupandwa. Siku moja, mwenyekiti wa kitongoji aliitisha mkutano ili kuzungumzia namna ya kutatua migogoro ya matumizi ya msitu huo iliyokuwa inaibuka mara kwa mara. Migogoro hiyo ilisababisha uharibifu katika msitu huo. Mtaalamu kutoka idara ya maliasili alikuwa miongoni mwa wageni walioalikwa. Wananchi walihudhuria kwa wingi katika mkutano huo na mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:

**Mwenyekiti:** Ndugu wananchi, tumekutana hapa kwa lengo la kutatua mgogoro uliopo kati ya kitongoji chetu na idara ya misitu na maliasili kutokana na vitendo vya ukataji miti, upasuaji mbao na urinaji asali katika msitu uliopo karibu na kitongoji chetu. Baadhi ya vijana wetu wamekamatwa na askari wa maliasili na kufikishwa mahakamani. Kuna wengine walijeruhiwa kwa risasi kutokana na wao kupambana na askari wakati walipokuwa wakifanya uhalifu katika msitu huo. Mbele yenu tuna mgeni kutoka idara ya maliasili ambaye atatueleza hali halisi ilivyokuwa. Ndugu mgeni wetu karibu sana.

**Ofisa maliasili:** Ndugu, mwenyekiti, ninashukuru sana! Wananchi oyee!

**Wananchi:** Oyee!!

**Ofisa Maliasili:** Ndugu wananchi, nimesimama mbele yenu ili kuwaeleza kuwa misitu inayowazunguka ni mali yenu wananchi, sisi tumepewa tu dhamana ya kuisimamia kwa faida ya vizazi



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 74 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vilivyopo na vijavyo. Ndugu wananchi, kuna uharibifu mkubwa wa misitu unaosababishwa na ukataji magogo, urinaji asali, upasuaji mbao, ukataji miti michanga pamoja na uwindaji haramu wa wanyama kama vile swala na nyati. Wahalifu hawa wanatoka miongoni mwenu na baadhi yao wamekamatwa na wengine kudhurika kutokana na kutokutii sheria. Hivyo, naomba leo tutafute ufumbuzi wa jambo hili kwa kuwa misitu ni uhai na muhimu sana kwa maendeleo yetu na taifa kwa ujumla, asanteni kwa kunisikiliza.

**Mwenyekiti:** (*naye anasimama)* Ndugu wananchi, nawakaribisha sasa mtoe mawazo yenu ili kutatua mgogoro uliopo mbele yetu.

**Mwananchi wa 1:** (*anasimama*) Ni kweli mtaalamu, ila kuna uharibifu unaosababishwa na umaskini wa wananchi. Hivyo, tunaomba mnapovuna miti mtugawie ploti za kulima kabla ya kuotesha miti mipya. Pia, mtupatie ajira ya kupakia magogo, kuotesha miti na ikiwezekana mtusaidie kujenga nyumba moja ya mwalimu katika shule yetu.

**Mwananchi wa 2:** (*anasimama*) Msitu huu si wetu kwa sababu walinzi wote wanatoka vijiji vya mbali na hakuna faida tunayopata sisi wananchi tuliopo jirani na msitu, hivyo tunaomba baadhi ya walinzi watoke katika kijiji chetu.

**Mwananchi wa 3:** (*anasimama*) Napendekeza kuundwe kamati ya pamoja ya ulinzi na mazingira.

**Mwenyekiti:** Sasa nimkaribishe Ofisa Maliasili ili kujibu hoja za wanakijiji.

**Ofisa Maliasili:** Ndugu zangu wananchi, kwa niaba ya idara ya misitu na maliasili ninawashukuru kwa kutoa maoni yenu. Kwanza, ninapenda kuwaahidi kuwa, tutashirikiana na serikali ya kijiji kupata vijana wanne wakakamavu. Tutawapatia mafunzo ya ulinzi kisha tutawapa ajira kwenye misitu yetu. Pili, tukivuna miti tutatoa ploti mia tatu za kulima kwa muda kabla hatujaotesha miti mipya. Tatu, tutakapovuna miti tutatoa ajira za muda mfupi kwa vijana wa kijiji hiki. Nne, tutaruhusu akina mama kwenda msituni kuokota kuni kila siku baada ya kupata vibali maalumu kutoka katika idara yetu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 75 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwenyekiti:** Asante sana Ofisa Maliasili kwa yote uliyotuahidi, mimi na wanakijiji tutashirikiana kwa pamoja kutunza msitu huu. Tunakutakia kazi njema.

**Ofisa Maliasili:** Asanteni sana, ninawatakia siku njema na bidii katika kujenga taifa.

## Zoezi la 5

1. Chanzo cha mgogoro ulioelezwa katika mazungumzo haya ni nini?
2. Je, unafikiri kuna faida gani ya kuishirikisha jamii moja kwa moja katika utatuzi wa migogoro?
3. Je, unafikiri migogoro huleta hasara gani kwa jamii?
4. Taja migogoro mitano unayoifahamu katika jamii unamoishi.

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wenzako njia mbalimbali zinazotumika kutatua migogoro katika jamii unamoishi. Andika mlichojadili katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 6

**A:** *Jibu maswali yafuatayo kwa kujaza nafasi zilizo wazi, majibu yaandike katika daftari lako la mazoezi.*

1. Taja vitendo vinavyodumisha urafiki mwema:
   (i) ____________________
   (ii) ____________________
   (iii) ____________________
   (iv) ____________________
2. Taja matukio manne yanayohitaji ushiriki wa watu wengi katika jamii:
   (i) ____________________
   (ii) ____________________

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 76 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) ______________________________

(iv) ______________________________

3. Ni njia zipi utakazotumia kutatua migogoro miongoni mwa wanafunzi wenzako?

   (i) ______________________________

   (ii) ______________________________

4. Je, ni mambo gani yanayoweza kuathiri maelewano mema kwa marafiki?

   (i) ______________________________

   (ii) ______________________________

   (iii) ______________________________

   (iv) ______________________________

   (v) ______________________________

**B:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

5. Lipi kati ya yafuatayo hutambulisha marafiki wema?
   (a) kuishi eneo moja
   (b) kusoma shule moja
   (c) tabia njema na upendo
   (d) kulala pamoja

6. Inatupasa kufanya nini ili tuweze kujenga maelewano mema na marafiki zetu?
   (a) kufanya udanganyifu
   (b) kuepuka tabia isiyofaa
   (c) kuanzisha ugomvi
   (d) kutosikiliza wengine

7. Kipi kati ya vitendo vifuatavyo ni muhimu katika kuishi vyema na jamii?
   (a) kushirikiana katika shida na raha
   (b) kuweka mipaka ya urafiki
   (c) kuweka mikakati ya kazi
   (d) kubagua walemavu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Utamsaidiaje mwanafunzi mwenzako mwenye tabia ya kugombana na rafiki zako?
   (a) kumshitaki kwa mwalimu wa darasa
   (b) kushirikisha wanafunzi kumkanya
   (c) kujitenga naye
   (d) kumshitaki kwa wazazi wake

9. Zifuatazo ni faida za kujenga uhusiano mwema na watu katika jamii isipokuwa:
   (a) kudumisha umoja na amani
   (b) kutatua matatizo ya familia
   (c) kuzuia maradhi ya kuambukiza
   (d) kushiriki katika kazi za pamoja

**C:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

10. Kutojali matatizo ya wengine huharibu urafiki.__________
11. Kushiriki katika michezo husaidia kutatua migogoro.__________
12. Sherehe ni tukio la kijamii linalodumisha upendo.__________
13. Uhusiano mwema ni kumshauri mwenzako kuwa mhalifu .__________
14. Kushiriki makongamano ya kidini hupunguza uhusiano na watu wengine.__________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Kujikimu | kupata mahitaji ya msingi kama vile chakula, malazi na mavazi |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 78 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kuwa mwajibikaji na kulinda rasilimali za umma

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza umuhimu wa kulinda rasilimali za umma kama wajibu wa kila raia mwema. Aidha, ulijifunza kubaini rasilimali za taifa, matumizi ya rasilimali za umma, kutunza rasilimali za taifa, kushiriki katika utunzaji wa rasilimali zilizopo pamoja na kukemea matumizi mabaya ya mali za umma. Katika sura hii, utajifunza wajibu wa jamii katika shughuli za maendeleo ya taifa, tabia ya mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo ya taifa na kubaini vitendo vya kulinda usalama wa taifa. Vilevile, utajifunza mbinu stahiki za kulinda mali za umma, vitendo vya matumizi mabaya ya mali za umma na njia anuwai za kupambana na matumizi mabaya ya mali ya umma na shughuli za kuleta maendeleo ya nchi. Umahiri huu utakuwezesha kujenga tabia ya kujituma katika kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo katika jamii yako. Aidha, utaweza kujenga tabia ya kuthamini, kulinda na kutunza mali ya umma.*

### Wajibu wa jamii katika shughuli za maendeleo ya taifa

Kujituma ni kufanya kazi kwa bidii ya hali ya juu bila kulazimishwa. Kujituma na kufanya kazi kwa bidii hutusaidia kuiletea nchi yetu maendeleo. Pia kujituma katika masomo hutuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea. Jamii ina wajibu wa kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma kufikia malengo waliyojiwekea ili kupata maendeleo yao wenyewe na taifa kwa ujumla. Vilevile, jamii ina wajibu wa kutii sheria za nchi, kulinda rasilimali za umma na kuwa sehemu ya kuhakikisha ulinzi wa taifa.

Utii wa sheria za nchi husaidia kuwa na nchi yenye amani, utulivu na usalama. Maendeleo ya nchi hutegemea amani na usalama wa nchi husika. Katika nchi yenye amani na utulivu wananchi wake hushiriki kwa uhuru katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Wananchi katika nchi zenye migogoro hutumia muda



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mwingi kujificha au kukimbia machafuko. Hivyo kukosa muda wa kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Nchi hizi hukabiliwa na njaa na magonjwa na hivyo kuathiri ushiriki wa wananchi katika shughuli za kukuza uchumi.

### Tabia za mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo ya taifa

Elimu ni mchakato ambao humwezesha mtu kupata maarifa na ujuzi wa kujitambua na kumwezesha kupambana na mazingira na mabadiliko ya mara kwa mara ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Nchi nyingi duniani zimewekeza katika elimu kwa wananchi wake. Uwekezaji huu hufanyika ili kuwa na wananchi wanaoweza kulisaidia taifa na kukua kiuchumi. Elimu ina manufaa kwa mtu binafsi na kwa jamii kwa ujumla. Inatarajiwa kuwa mtu aliyeelimika atatumia elimu yake katika kuchangia maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Baadhi ya tabia zinazotarajiwa kuoneshwa na mtu aliyeelimika na anayetumia elimu yake katika maendeleo ya taifa ni kama zifuatazo:

(a) **Mwadilifu:** Mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo ya jamii ni mwadilifu na mwenye mwenendo unaokubalika. Maadili mema ni kitu cha msingi sana katika jamii. Bila maadili mema jamii haiwezi kuwa ya kistaarabu. Msomi yeyote anatarajiwa kuwa na maadili mema, yanayokubalika katika jamii anayoishi. Kwa mfano, inatarajiwa awe mtii kwa serikali, mwenye bidii ya kazi, atoe huduma bila upendeleo na afanye kazi kwa uadilifu. Pia, aheshimu sheria, atunze siri za serikali, awe mzalendo na asitoe wala kupokea rushwa.

(b) **Hufanya utafiti:** Mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo ya jamii hufanya utafiti kupata majibu yatakayosaidia kutatua matatizo ya jamii. Vilevile, utafiti husaidia kuibua fikra na maarifa mpya kuhusu jambo fulani.

(c) **Huibua fikra mpya:** Mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo anapaswa kuonesha uwezo wa kuibua fikra mpya na kubuni njia mbadala za kufanya jambo, au kutengeneza fursa mpya iliyo bora zaidi. Ulimwengu wa sayansi na teknolojia unaundwa na wabunifu. Wasomi wanatarajiwa kuwaongoza wenzao katika jamii kubuni njia mbadala za kujiendeleza kwa kubaini fursa na kutengeneza miradi, au kubuni biashara mbalimbali.

(d) **Hujitambua, hujiamini na hujithamini:** Mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo anajitambua, anajiamini na kujithamini. Hali hii humwezesha kujua yeye ni nani, ana wajibu gani katika familia, jamii na taifa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) **Huzingatia sheria na kanuni zilizowekwa:** Mtu anayetumia elimu yake katika kuleta maendeleo ya taifa huzingatia na kutii sheria na kanuni zilizowekwa kwa ustawi wa maisha yake na jamii. Kuzingatia sheria humsaidia kutekeleza, shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Shughuli hizi ni muhimu kwa maendeleo yake binafsi, jamii na taifa kwa ujumla.

## Zoezi la 1

1. Unapaswa kufanya nini ili kufikia malengo uliyojiwekea?
2. Eleza maana ya elimu.
3. Kwa nini wasomi wanashauriwa kufanya utafiti?
4. Mtu aliyeelimika ana tabia gani katika jamii?

## Kazi ya kufanya namba 1

Andika athari tano zinazoweza kusababishwa na tabia ya kukosa maadili. Ziandike athari hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Vitendo vya kulinda usalama wa taifa

Ulinzi ni kazi ya kuangalia usalama wa watu na mali zao. Usalama ni hali ya kuishi kwa amani bila hofu ya kudhuriwa na binadamu, wanyama, maradhi au majanga yoyote. Vilevile, ni hali ya kutokuwa na vurugu au hatari katika sehemu tunazoishi.

Ulinzi na usalama wa taifa letu ni jukumu la kila mwananchi akishirikiana na vyombo vyenye wajibu wa kulinda usalama wa nchi yetu. Wananchi wana wajibu wa kulinda mipaka ya maeneo yao kwa kutoa taarifa za uhalifu katika vijiji, mitaa, wilaya na mikoa yao. Vilevile, wanapaswa kutoa taarifa kuhusiana na mwenendo wa mtu au watu wasiokuwa waaminifu wanaoishi katika maeneo yao. Aidha, wananchi wana wajibu wa kushiriki kazi ya ulinzi shirikishi na kuchangia vifaa vitakavyotumika katika kazi ya ulinzi wa eneo wanamoishi. Pia, wanawajibika kushiriki kwenye matukio ya uokoaji kama kupambana na majambazi, moto, mafuriko au wanyama wakali wanaovamia watu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 81 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vyombo vya ulinzi na usalama wa taifa la Tanzania ni pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Polisi, Magereza, Zimamoto na Usalama wa Taifa. Jamii inapaswa kujenga umoja na kushirikiana na askari wa vyombo vya ulinzi na usalama. Vitendo vinavyoweza kulinda na kudumisha usalama wa nchi ni kama vifuatavyo:

(a) **Utawala bora:** Huu ni utawala ambao unazingatia sheria, kanuni, na taratibu zilizowekwa katika nchi. Pia, ni utawala ambao watu hushiriki kutoa uamuzi wa masuala mbalimbali ya kijamii. Kwa mfano, viongozi wa serikali katika ngazi zote wanapaswa kuwa waadilifu. Hawapaswi kupendelea watu kutokana na kipato chao, jinsi zao, dini zao, rangi yao, makabila yao au vyeo vyao. Kinyume chake, kukosekana kwa utawala bora watu wanaweza kuasi na kuhatarisha usalama kwa kugoma na kufanya maandamano katika kudai haki zao.

(b) **Kushirikiana:** Ushirikiano ni muhimu katika kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarishwa katika nchi yetu. Mfano, ikiwa wananchi watashirikiana katika kutekeleza majukumu yao chini ya uongozi wa serikali kuu na serikali za mitaa, jamii itajilinda dhidi ya maadui. Bila ushirikiano, ulinzi na usalama wa mali zetu unaweza kuwa mashakani, kwani wahalifu wanaweza kutumia mwanya huo kuhatarisha usalama wa nchi.

(c) **Kuheshimu haki za binadamu:** Tamko la dunia kuhusu haki za binadamu, limeorodhesha haki ambazo kila mtu anapaswa kuziheshimu na kuzifuata. Viongozi katika ngazi zote wanao wajibu wa kuhakikisha haki za kila raia hazivunjwi na kuhatarisha usalama wa raia na mali zao. Uvunjaji wa haki za binadamu unaonekana pale ambapo raia wananyimwa haki zao za msingi. Mfano, kuwanyima watu haki ya kuchagua viongozi wanaowataka au matokeo ya kura kubadilishwa na kutangazwa viongozi ambao wao hawajawachagua. Iwapo wananchi hawa hawatatendewa haki, wanaweza kushinikiza kudai haki zao kwa njia zinazoweza kuhatarisha usalama wa nchi, wananchi na mali zao. Hivyo, ni vyema viongozi wetu kuheshimu haki za binadamu.

(d) **Matumizi mazuri ya rasilimali za umma:** Viongozi wote katika ngazi zote hapa nchini wana wajibu wa kutumia mali za umma kwa manufaa ya wananchi wote bila kufanya ubadhirifu. Ubadhirifu ni hali au tabia ya baadhi ya viongozi kutumia madaraka yao vibaya, hasa katika kutumia fedha na rasilimali za umma kwa manufaa binafsi na kukwamisha shughuli na miradi ya maendeleo katika jamii. Baadhi ya viongozi hushindwa kutoa taarifa za mapato na matumizi ya fedha za umma. Kwa hali hiyo,

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 82 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wanaweza kusababisha wananchi kuichukia serikali yao na hatimaye kuleta vurugu zinazoweza kuhatarisha usalama wa nchi, watu na mali.

(e) **Fursa za ajira au kujiajiri:** Ni vyema kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi apate fursa ya kufanya kazi. Mtu anaweza kupata fursa ya ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri ili aweze kuishi. Ukosefu wa kazi za kufanya unahatarisha usalama wa nchi, wananchi na mali zao.

(f) **Mfumo bora wa elimu:** Kuwa na mfumo wa elimu unaowasaidia wahitimu kujitenga na kuepuka matendo hatarishi. Matendo hatarishi ni kama vile matumizi ya dawa za kulevya, wizi, ujambazi, kurubuni au kurubuniwa kushiriki katika vitendo vya kigaidi na hivyo kuhatarisha usalama wa wananchi na mali zao na taifa.

(g) **Kubuni michezo mbalimbali:** Michezo ni afya na hivyo ni muhimu kwa ustawi wa wananchi. Viongozi katika ngazi zote zinazotoa uamuzi, hawana budi kubuni michezo itakayoshirikisha jinsi zote. Kupitia michezo watu hufahamiana na kujenga umoja. Michezo ni ajira inayoweza kusaidia vijana kujiepusha na vitendo viovu kama vile ubakaji, utumiaji dawa za kulevya, ujambazi na wizi. Hivyo, michezo itakuwa ni nyenzo ya kuimarisha ulinzi na usalama.

## Zoezi la 2

1. Eleza maana ya ulinzi na usalama wa taifa.
2. Ni mambo gani yanayoweza kuhatarisha usalama wa nchi, wananchi na mali zao?
3. Wananchi wanawezaje kuimarisha ulinzi na usalama wao?
4. Eleza hasara za ubadhirifu wa mali za umma.

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako kuhusu mbinu zinazotumika kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao katika maeneo mnamoishi. Andika mbinu mlizojadili katika daftari lako la mazoezi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 83 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mbinu stahiki za kulinda rasilimali za umma

Ulinzi wa rasilimali za umma ni wajibu wa kila Mtanzania kikatiba. Rasilimali zinapaswa kulindwa na kutumiwa vizuri ili ziwanufaishe watu wakati huu na kwa vizazi vijavyo. Jamii inapaswa kuwa na uelewa wa njia stahiki za kulinda rasilimali za umma ili zidumu.

Rasilimali za nchi ni jumla ya vitu vyote vinavyomilikiwa na kusimamiwa na serikali kwa niaba ya wananchi kwa ajili ya matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Rasilimali za nchi ni chanzo muhimu cha mapato ya serikali, kwa mfano, mbuga za wanyama, milima na madini huchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kutokana na pato litokanalo na matumizi ya rasilimali hizo. Pia, rasilimali kama, makaa ya mawe, gesi na maji, hutupatia nishati ya kuendesha viwanda na hata matumizi ya nyumbani. Vilevile, misitu husaidia kuboresha hali ya hewa ambayo huchafuka kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu. Misitu husababisha mvua kunyesha na kupatikana kwa maji ambayo ni muhimu kwa maisha ya watu na viumbe hai wengine. Tanzania ina sheria mbalimbali zinazotungwa ili kudhibiti matumizi ya rasilimali. Zipo mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kulinda rasilimali za umma. Baadhi ya mbinu hizo ni:

**Kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutunza rasilimali za umma:** Jamii inapaswa kuelimishwa juu ya umuhimu wa rasilimali na namna bora na endelevu ya kuzitunza rasilimali hizo.

Elimu inapaswa kutolewa kwa Watanzania wote, hususan wale wanaopakana na rasilimali zinazohitaji uangalizi maalumu. Kwa mfano, watu wanaoishi kandokando ya mbuga za wanyama wanapaswa waelimishwe juu ya umuhimu wa kutunza wanyamapori kwa uchumi wa nchi. Wananchi wanastahili kushirikishwa katika mipango ya uhifadhi wa misitu na wanyama na pia wanatakiwa kupata mrabaha yaani kurejeshewa sehemu ya faida itokanayo na matumizi ya rasilimali hizo.

**Kuwa na sheria za kuhifadhi na kutunza rasilimali za umma:** Katika kusimamia rasilimali, sheria mbalimbali zimetungwa na kuidhinishwa ili kuongoza matumizi na utunzaji wa rasilimali hizo. Pia, sheria zinalenga kuhakikisha kuwa rasilimali zinaboreshwa, zinasimamiwa na kudhibitiwa kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa. Kwa mfano, sheria ya usimamizi wa rasilimali maji ilitungwa ikiwa na malengo mbalimbali. Malengo hayo ni kuhakikisha kuwa rasilimali maji hapa nchini inatunzwa, inatumiwa na inaendelezwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kuwa na mikakati ya ulinzi na usalama wa rasilimali za umma:** Katika matumizi ya rasilimali, wananchi wanapaswa kufahamu kuwa, rasilimali zinahitaji ulinzi ili ziwe salama. Kukosekana kwa mikakati ya ulinzi na usalama husababisha matumizi mabaya ya rasilimali za taifa. Iwapo ulinzi na usalama utakosekana, watu wasioitakia mema nchi yetu watapata nafasi ya kuhujumu rasilimali zetu kama madini na mbuga za wanyama. Pia, kukosekana kwa ulinzi kunaweza kuwafanya wawekezaji kutumia maeneo waliyopewa kwa matumizi tofauti kama vile kuhifadhi wahalifu na kufanya biashara za utoroshaji madini bila kulipa kodi ya serikali. Ujangili na uwindaji wanyama bila kibali yamekuwa ni miongoni mwa matukio yanayotokana na kukosekana kwa ulinzi na usalama makini. Vilevile, kugombania rasilimali kati ya wageni na wazawa kunaweza kusababisha kuvunjika kwa hali ya usalama iwapo taratibu za umiliki na ushirikishwaji wa wananchi hazikuzingatiwa. Matumizi mabaya ya misitu kwa kuchoma mkaa yanaweza kusababisha moto na madhara kwa watu na uchumi wa nchi.


**Kuhamasisha uzalendo katika kutunza rasilimali za umma:** Katika utunzaji wa rasilimali ni vyema wananchi wakahimizwa kuwa wazalendo. Uzalendo ni hali ya kuipenda nchi yako na kujitoa kuitumikia kwa nidhamu, uaminifu na ukweli. Uzalendo utasaidia kuondoa tatizo la baadhi ya wananchi kushirikiana na wageni katika kupora rasilimali za nchi kwa manufaa yao binafsi.

Waliokabidhiwa mamlaka wanapaswa kutanguliza uzalendo mbele kwa kuzitunza rasilimali za taifa lao ili ziweze kuwasaidia kwa maisha ya sasa na ya vizazi vijavyo.

## Zoezi la 3

1. Kwa nini tunapaswa kuzilinda rasilimali za umma?
2. Elimu ina nafasi gani katika kutunza rasilimali za umma?
3. Kwa nini tunapaswa kuweka sheria za kutunza rasilimali za umma?

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wenzako jinsi mtakavyohamasisha uzalendo katika matumizi na utunzaji wa rasilimali za taifa. Andika mbinu hizo katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vitendo vya matumizi mabaya ya mali za umma

Matumizi mabaya ya mali ya umma ni matendo ya viongozi au wananchi kutothamini mali walizokabidhiwa, hivyo kuzitumia kinyume na utaratibu ulioelekezwa. Tathmini hufanywa katika sehemu mbalimbali ili kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki waliohusika na vitendo hivyo. Hii hukuza ari ya utawala bora ambao huwasaidia wananchi kupata maendeleo endelevu. Baadhi ya vitendo vya matumizi mabaya ya mali ya umma ni:

**Kutojali mali ya umma:** Mali ya umma ni kitu chochote chenye thamani kilicho chini ya mamlaka na umiliki wa jamii. Baadhi ya viongozi wa umma wanaosimamia mali hizi hukiuka taratibu zilizowekwa na kutumia mali hizo visivyo. Kwa mfano, kutumia magari na majengo ya umma kwa shughuli zenye masilahi binafsi.

**Rushwa:** Rushwa inapotolewa katika kupata huduma kama vile za matibabu, ajira, zabuni na nyinginezo, kwa mfano, ili kumwezesha mfanyabiashara kukwepa kodi, husababisha matumizi mabaya ya mali za umma na serikali kukosa mapato.

**Ufisadi:** Ufisadi hujitokeza iwapo watumishi wa umma au viongozi watafanya ubadhirifu wa fedha katika miradi ya maendeleo mfano, kwa kuongeza bei ya bidhaa zinazonunuliwa kuwa zaidi ya bei yake halisi ili kupata asilimia fulani ya fedha kutoka kwa muuzaji kwa masilahi binafsi. Ufisadi husababisha miradi ya maendeleo kutekelezwa chini ya viwango, kuwa na wafanyakazi na miradi hewa, na kuruhusu miradi mikubwa kutekelezwa bila kujali madhara kwa umma na mazingira kwa ujumla.

**Mikataba mibovu:** Kuingia mikataba mibovu katika sekta mbalimbali mfano ya madini, mashamba makubwa, vitalu vya uwindaji, uvunaji misitu, na miradi ya maendeleo ni mojawapo ya matumizi mabaya ya mali za umma. Mikataba mibovu hulitia hasara taifa na kuwanufaisha watu wachache.

**Kutumia madaraka vibaya kujipatia faida binafsi:** Baadhi ya watumishi au viongozi waliopewa dhamana katika ofisi za umma hutumia madaraka au ofisi zao vibaya kwa faida binafsi. Kwa mfano, kujimilikisha viwanja vya umma kinyume na taratibu, kunyanyasa wananchi wanaodai haki zao, kuwabambikia wananchi kesi za uongo, kuwakandamiza wafanyakazi, au kuuza dawa za hospitali za umma kwenye maduka ya watu binafsi.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Ni vitendo gani vinavyoashiria matumizi mabaya ya rasilimali za umma katika nchi yetu?
2. Vitendo hivyo vina madhara gani kwa maendeleo ya nchi?
3. Taja njia tatu za kukabiliana na matumizi mabaya ya rasilimali ya umma.
4. Kuna umuhimu gani wa kufanya tathmini ya matumizi ya rasilimali za umma?

## Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wenzako njia gani zitumike ili kujenga maadili ya viongozi wa umma. Andika njia hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Njia anuwai za kupambana na matumizi mabaya ya rasilimali za umma

Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara yenye utajiri mkubwa wa rasilimali. Baadhi ya rasilimali hizo ni pamoja na watu, ardhi na maji katika mito, mabwawa, maziwa na bahari. Pia, kuna misitu, milima na mabonde, madini kama dhahabu, rubi, almasi na tanzanaiti. Tanzania ina hifadhi za mafuta, gesi na wanyama pori wa aina mbalimbali. Vilevile, ina vivutio vingi vya kitalii kama fukwe za bahari, maziwa, mlima Kilimanjaro, kumbukumbu za mambo ya kale kama vile Ismila, Kondoa Irangi na mapango ya Amboni.

Ili nchi yetu iendelee hatuna budi kupambana na matumizi mabaya ya rasilimali. Zifuatazo ni baadhi ya njia za kupambana na matumizi mabaya ya rasilimali za nchi katika jamii zetu:

(a) Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya rasilimali za umma kupitia vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii, ili kuhamasisha jamii kuthamini rasilimali za taifa lao;

(b) Kusimamia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kuhusu matumizi bora ya mali za umma. Sheria na kanuni hizi zitasaidia kutoa miongozo

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

sahihi ya matumizi bora na endelevu ya rasilimali za umma. Pia, sheria na kanuni zitatoa miongozo ya namna ya kuadhibu wote wanaotumia vibaya rasilimali ya nchi;

(c) Kushiriki ulinzi kwa kutoa taarifa za matukio yoyote ya kihalifu au hujuma za rasilimali za umma katika mamlaka husika kama polisi na idara husika za serikali;

(d) Kutunga sera bora na kuzisimamia ipasavyo ili kutunza, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za umma kwa faida ya wananchi wote;


(e) Kushiriki kikamilifu kuepuka uharibifu wa mazingira ili kulinda rasilimali zetu katika maeneo mbalimbali kama misitu, migodi, mbuga na hifadhi za wanyama; na

(f) Kupinga vitendo vya rushwa na ufisadi kwa watumishi au viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali za umma.

## Zoezi la 5

1. Bainisha rasilimali tano za umma.
2. Eleza njia tatu za kutunza rasilimali za umma.
3. Je, nini kifanyike ili kuitunza rasilimali ardhi katika eneo unaloishi?
4. Je, katika eneo unaloishi kuna mikakati gani ya kutunza rasilimali maji?

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wenzako njia sahihi za kukabiliana na migogoro inayotokea katika maeneo yenye rasilimali za umma katika nchi yetu. Andika njia hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Kushiriki shughuli za maendeleo ya nchi yako

Katiba ya Tanzania inaeleza kuwa wananchi wana haki ya kufanya kazi, kumiliki mali na kupata ajira kwa haki. Hivyo wananchi wanatarajiwa kutumia vipaji na uwezo wao kubuni shughuli zenye kuleta maendeleo kwa taifa. Baadhi ya shughuli hizo ni:


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Kilimo cha mazao ya chakula na biashara, mfano kilimo cha mbogamboga, matunda na nafaka;
(b) Ufugaji wa wanyama na ndege kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, kanga na bata;
(c) Uvuvi wa samaki katika mabwawa, maziwa na bahari;
(d) Uchimbaji wa madini kama vile, dhahabu, almasi, tanzanaiti, chuma, bati, chokaa;
(e) Biashara ya ndani na ya nje ya nchi; na
(f) Shughuli za viwandani mfano, usindikaji na uchakataji wa malighafi.

## Zoezi la 6

1. Taja haki tatu za Mtanzania kama zinavyotajwa katika katiba.
2. Taja shughuli tatu za maendeleo zinazofanywa nchini Tanzania.
3. Taja shughuli kuu ya maendeleo inayofanyika katika bahari na maziwa.

## Kazi ya kufanya namba 6



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu faida mbili za kushiriki katika shughuli za kuleta maendeleo. Andika faida hizo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 7

**A:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

1. Kwa nini tunapaswa kutunza rasilimali za nchi yetu?
   (a) ili ziweze kunufaisha Watanzania wa leo na kwa vizazi vijavyo
   (b) kuwezesha upatikanaji wake kwa matumizi ya sasa tu
   (c) ili wageni wasipore rasilimali zetu
   (d) ili kunufaisha wawekezaji



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 89 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Ipi kati ya zifuatazo ni moja ya mbinu stahiki za kulinda rasilimali za umma?
   (a) kuziuza kwa wageni ili kupata fedha
   (b) kutoa elimu ya utunzaji wa rasilimali za nchi
   (c) kuzigawa kwa wananchi wazitumie
   (d) kuzuia zisitumike kabisa

3. Vipi ni vitendo vya matumizi mabaya ya mali ya umma?
   (a) kuzitumia kwa manufaa ya wananchi
   (b) kuwamilikisha wageni kutoka nchi za nje kiholela
   (c) kuzihifadhi kwa kushirikisha wananchi
   (d) kuzuia ujangili na uwindaji holela wa wanyama pori

4. Ipi kati ya vifuatavyo si miongoni mwa vitendo vya kulinda nchi yetu?
   (a) kutoa taarifa za uhalifu
   (b) kulinda mipaka ya nchi
   (c) kutoa taarifa kwa wahalifu kuhusu rasilimali zilizopo nchini
   (d) kusimamia sheria na kulinda rasilimali zetu.

5. Moja kati ya hizi si athari za rushwa katika jamii:
   (a) serikali kushindwa kufikia malengo yake
   (b) kuongezeka kwa gharama za kiutawala
   (c) kukosekana kwa ujasiri na kushindwa kufikia kiwango cha juu cha uadilifu
   (d) kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato

**B:** *Oanisha kipengele kutoka* ***Sehemu A*** *na kipengele kutoka* ***Sehemu B*** *ili kupata maana sahihi, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 90 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 6. Kutumia mali za umma kwa masilahi binafsi<br>7. Husaidia kupambana na matumizi mabaya ya rasilimali za nchi<br>8. Ni jukumu la wananchi wote<br>9. Rasilimali<br>10. Hutumia wakati wake kuelimisha jamii juu ya maendeleo | (a) mtu anayetumia vibaya elimu yake<br>(b) kufanya kazi kwa bidii<br>(c) mzalendo<br>(d) ufisadi<br>(e) sheria za kulinda rasilimali<br>(f) milima, mabonde, madini na mbuga za wanyama<br>(g) usalama wa taifa<br>(h) tija na ufanisi<br>(i) afya ya mwili na akili |

**C:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

11. Moja ya njia za kupambana na matumizi mabaya ya mali za umma ni kuelimisha watu._____
12. Tunalinda rasilimali za nchi kwa kuwa zina manufaa kwa nchi._____
13. Watu wote walioelimika wanajituma katika kuleta maendeleo ya nchi.__
14. Ni vyema kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi apate fursa ya kuajiriwa._____
15. Upokeaji na utoaji fedha ili kupata upendeleo wa jambo ni ufisadi. _____

## Msamiati

**Mrabaha** ushuru anaotozwa mfanyabiashara au mwekezaji na aliyemkodisha eneo la biashara au mtaji wa uwekezaji

**Ugaidi** vitendo vibaya vya kutumia nguvu vinavyofanywa na wavamizi wenye lengo la kutimiza mambo yao

**Utafiti** uchunguzi wa kina wa kisayansi wa jambo maalumu wenye lengo la kugundua na kupata maarifa mapya au kuongeza ufahamu

**Yakinifu** jambo lenye uhalisia, ukweli na uthibitisho

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Kusimamia majukumu

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kupokea majukumu, umuhimu wa kusimamia majukumu hayo, kuyatekeleza kwa ufanisi na kutii sheria. Katika sura hii, utajifunza kutambua majukumu yako kama kiongozi katika ngazi ya familia na shule, kubaini njia mbadala za kutatua matatizo, na kupendekeza njia stahiki za kuboresha utendaji wa kazi. Pia, utajifunza kutambua faida za kushirikisha watu wengine na hasara za kutowashirikisha wengine katika utekelezaji wa majukumu. Vilevile, utajifunza kushirikiana na wanajamii katika shughuli za maendeleo, na kufichua maovu yanayohusiana na ubadhirifu na ufisadi katika utekelezaji wa majukumu. Umahiri huu utakuwezesha kutambua na kutekeleza majukumu yako uwapo nyumbani, shuleni, ndani ya jamii na hata katika ngazi ya kitaifa. Halikadhalika, itakusaidia kusimamia na kuwashirikisha watu wengine katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.*

### Nafasi ya uongozi katika familia

Kiongozi ni mtu mwenye mamlaka ya kushawishi watu wengine waweze kutekeleza malengo yaliyowekwa. Jukumu kubwa la kiongozi ni kuelekeza njia ambayo watu wengine wataifuata. Katika familia, wazazi ndio viongozi wakuu wenye wajibu wa kuwalea na kuwaongoza watoto kwa kuhakikisha kuwa familia inajenga mtazamo wa pamoja katika kufikia malengo waliojiwekea.

Aidha, familia bora hutegemea uimara wa uongozi katika kuhakikisha kuwa kila mwanafamilia anaelewa na kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Matatizo mengi katika familia hutokana na hali ya kukosa maelewano miongoni mwa wanafamilia. Hivyo, viongozi wa familia wana wajibu adhimu wa kujenga mazingira ya upendo na ushirikiano ili kuondoa au kupunguza migogoro katika familia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Majukumu katika familia

Katika familia kuna mgawanyo wa majukumu ambayo kila mwanafamilia anapaswa kuyatekeleza kwa nafasi yake kama mzazi au mtoto.

### Majukumu ya mzazi au mlezi katika familia

Baba na mama ni viongozi walio sawa katika familia ingawa majukumu yao yanaweza kutofautiana kidogo. Kwa ujumla, mzazi au mlezi ana majukumu makuu manne kama ifuatavyo:

***Mwalimu wa familia:*** Mzazi au mlezi ndio mwalimu wa kwanza katika maisha ya watoto wake. Huyu ndiye anayewafundisha maisha kwa kuwaelekeza namna bora ya kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo kadri wanavyokua. Ili kutekeleza wajibu huu, mzazi anapaswa kukaa na watoto wake kwa muda wa kutosha, kuwapenda na kuwashirikisha katika kazi mbalimbali.

***Mlinzi wa familia:*** Usalama ni hitaji la msingi kwa familia nzima. Kama mlinzi, mzazi au mlezi ndiye anayehakikisha kuwa wanafamilia hawaishi kwenye hali ya wasiwasi na mashaka. Mzazi au mlezi hubaini mazingira hatarishi yanayoweza kuwaumiza, kuwadhalilisha au kusababisha madhara kwa watoto. Pia, mzazi au mlezi ndiye anayelinda ndoto za wanafamilia ili kuhakikisha kuwa anawasaidia kuzitimiza ndoto zao.

***Mtafutaji katika familia:*** Jukumu la mzazi au mlezi ni kuhakikisha wanafamilia wanapata mahitaji yao kama vile chakula, malazi, mavazi, matibabu na elimu kwa kadri uwezo wake wa kiuchumi unavyoruhusu. Mzazi anayefanya kazi kwa bidii huwarithisha wanafamilia tabia ya kufanya kazi kwa bidii tangu wakiwa wadogo ili waweze kujitegemea watakapokuwa watu wazima.

***Mfariji wa familia:*** Mzazi au mlezi ndiye anayehakikisha wanafamilia wanakuwa na furaha hata pale hali ngumu zinapojitokeza. Kupitia tabia zake, mzazi au mlezi ndiye anayehakikisha wanafamilia wanakuwa na matumaini ya kufanikiwa katika maisha. Katika nyakati za majonzi, mzazi ndiye mwenye jukumu la kuwatia moyo wanafamilia na kurejesha matumaini yao.

### Majukumu ya watoto katika familia

Watoto wanalelewa chini ya mamlaka ya wazazi au walezi wao. Yafuatayo ni majukumu makubwa ya watoto:

***Heshima na nidhamu:*** Wajibu mkubwa wa watoto wenye tabia njema ni kuwa na heshima na nidhamu kwa wazazi au walezi wao. Katika mila na desturi zetu, mathalani, haipendezi mtoto kubishana na mzazi wake kwa sababu yoyote

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ile. Inapotokea wazazi au walezi wametofautiana na hata kutengana, wajibu wa watoto wenye nidhamu ni kuwaheshimu wote bila kuegemea upande wa mzazi au mlezi mmojawapo.

***Kujifunza:*** Watoto wana wajibu wa kujifunza kwa wazazi au walezi wao kwa kuwasikiliza na kutekeleza kile wanachoelekezwa. Kwa umri wake, mzazi ndiye anayefahamu mambo mengi kuliko mtoto. Hivyo mtoto mwenye nidhamu hukaa karibu na mzazi au mlezi wake kujifunza namna bora ya kuishi na watu, namna ya kutatua migogoro na mambo ya kuepuka na kuzingatia ili apate mafanikio ayatakayo.

***Kuwajibika:*** Watoto wana jukumu la kushiriki kazi za mikono bila kulalamika, kusoma kwa bidii, kukiri makosa yao pale wanapokosea na kuishi kwa mwenendo safi unaokubalika katika jamii.

Aidha, wanaume, wanawake au watoto hupewa majukumu ya kifamilia kulingana na imani, tamaduni na desturi husika. Majukumu hayo hubainisha kile kinachochukuliwa kuwa kinafaa kwa wanaume, wanawake na watoto katika jamii. Majukumu yanatofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine na yanaweza kubadilika baada ya muda. Majukumu hayo hutofautiana pia kutoka kikundi kimoja cha jamii hadi kingine katika watu wenye utamaduni mmoja. Vilevile, rangi, tabaka, dini, kabila, hali za kiuchumi na umri mathalani, huathiri majukumu ya kifamilia. Majukumu ya kifamilia hutatiza pale ambapo jamii inapoweka thamani kubwa kwenye majukumu ya jinsia moja. Hali hiyo inaweza kusababisha kutokuwa na usawa katika kufanya maamuzi, hivyo husababisha unyanyasaji na kuzuia haki kutendeka kwa jinsia nyingine.

## Mambo yanayoathiri mabadiliko ya majukumu katika familia

Mambo yanayoweza kuchangia mabadiliko ya utekelezaji wa majukumu katika familia ni pamoja na haya yafuatayo:

**Mila na desturi:** Mgawanyo wa majukumu katika familia unaweza kukwamishwa na mila na desturi ya jamii husika. Kwa mfano, katika baadhi ya jamii ni mwiko kwa mwanaume kupika au kumpeleka mtoto kliniki. Hata hivyo, mabadiliko yanayoendelea katika jamii yamewezesha kuwepo kwa wanaume wanaopika hotelini na nyumbani. Lakini pia, wapo wanaopeleka watoto wao kliniki.

**Migogoro katika familia:** Wakati mwingine wanafamilia hukumbana na hali ya kutokuelewana. Mfano, mzazi anaweza kutofautiana na mtoto, mtoto akatofautiana na mwenzake au mzazi kutofautiana na mwenzake. Ingawa



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hali hii ni ya kawaida kutokea, huweza kusababisha nyufa katika familia na kuleta mabadiliko ya majukumu katika malezi ya familia.


**Ugonjwa au kifo:** Mzazi au mlezi mmoja anapofariki au kushindwa kuendelea na majukumu yake kutokana na kuugua, hali hiyo huathiri utekelezaji wa majukumu katika familia. Katika familia zinazoongozwa na wazazi au walezi wote wawili, mathalani, mke aliyekuwa anatoa malezi kwa familia akiugua au kufariki basi mume atapaswa kutimiza majukumu yote ya familia.

**Elimu:** Elimu husaidia kubadili mitazamo ya watu na kufanya majukumu ambayo hapo awali wasingeyafanya kulingana na jinsi zao. Kwa mfano; kwa asili kazi kama vile ya uhudumu wa ofisi, mapokezi au ukatibu muhtasi zilichukuliwa kuwa ni za wanawake lakini kwa sasa tuna wanaume wengi wanaofanya kazi hizo.

**Sera:** Kuna miongozo ya kitaifa kupitia asasi mbalimbali zinazoshughulikia kuleta usawa katika familia.

**Majanga:** Mara nyingi ikitokea hali ya hatari kama vile vita, mafuriko, tetemeko la ardhi na ukame husababisha mtawanyiko wa familia. Katika hali hiyo wanawake wengi huwa karibu na watoto hivyo huchukua jukumu la kuwa watafutaji wa mahitaji na walinzi wa familia.

### Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu majukumu ya kila mmoja katika familia yake. Andika majukumu hayo katika daftari lako la mazoezi.

### Njia mbadala za kutatua matatizo katika familia

Kila mtu ana mbinu au namna yake mwenyewe anayopendelea kushughulikia matatizo katika familia. Mbinu zifuatazo husaidia kupata ufumbuzi kwa haraka:

**Kuheshimu hisia za wengine:** Binadamu tunatofautiana mitazamo na hisia zetu. Jambo lilelile, linaweza kutazamwa kwa namna tofauti na kuibua hisia tofauti baina ya watu. Tunapotafuta ufumbuzi wa matatizo katika familia, hatua ya kwanza kuzingatia ni kuepuka kuwahukumu au kuwabebesha watu lawama kwa makosa yaliyokwisha kutokea. Hata kama mwenzako



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 95 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

anafikiri tofauti na wewe, bado unaweza kutofautiana naye kwa staha. Pasipo kuheshimiana ni vigumu watu wawili kuelewana na hivyo kupata ufumbuzi wa changamoto.

**Kubaini kiini cha tatizo:** Mara nyingi kiini cha tatizo hujificha na hakionekani kwa urahisi. Hata hivyo, ili kuweza kupata undani wake ni muhimu kutambua wahusika wakuu, mazingira yaliyosababisha tatizo likatokea na kubuni hatua au mwelekeo unaofaa kutatua tatizo hilo. Haya yote yanahitaji uvumilivu na staha.

**Kuelewa utashi wa kila upande:** Katika mazingira ambayo kuna pande mbili zinazotofautiana, ni busara kujitahidi kuelewa mtazamo wa kila upande. Ukweli wa jambo hauwezi kufahamika kwa kusikiliza upande mmoja na kupuuza upande mwingine. Ni vizuri kujipa muda wa kuelewa kwa kina pande zote mbili bila upendeleo.

**Kujadiliana kwa upendo:** Mazungumzo yanayofanyika katika hali ya upendo yanawawezesha watu kujieleza. Bila upendo baina ya pande mbili zinazotofautiana itakuwa vigumu watu kujadiliana kwa uhuru. Ili majadiliano yafanyike kwa ufasaha, ni vizuri hata anayeonekana kukosea aheshimiwe, kupendwa na kusikilizwa.

**Kukubaliana hatua za kuchukua:** Kila mtu hufikiri tofauti katika kutafuta hatua za kuchukua. Hivyo, ni muhimu mitazamo ya watu wote izingatiwe. Uamuzi bora unaopaswa kuchukuliwa ni ule unaozingatia hisia za kila mmoja anayehusika na tatizo kwa namna moja au nyingine.

**Utekelezaji wa makubaliano:** Hatua hii ya utekelezaji wa makubaliano na matazamio ya kuwa na suluhu ni muhimu. Katika hatua hii tathmini hufanyika ili kujua kama maafikiano ya makubaliano na utekelezaji wake umefanyika na suluhu imepatikana.

## Zoezi la 1

1. Eleza umuhimu wa kuheshimu hisia za wengine katika kutatua tatizo.
2. Mbinu gani utatumia kumfanya mwanafamilia asiyetaka mazungumzo awe tayari kuzungumza?
3. Taja matatizo mawili yaliyowahi kutokea katika jamii yenu na yaliyohitaji majadiliano kwa upendo katika kuyatafutia ufumbuzi.
4. Je, ni hatua gani za kufuata ili kupata ufumbuzi wa tatizo?


FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 96 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako kuhusu hasara za kutofuata hatua za kufanya tafakuri ya kina katika kutatua tatizo. Andika hasara hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Majukumu mbalimbali ya viongozi katika ngazi ya shule za msingi

Viongozi wa shule za msingi wapo katika ngazi zifuatazo; Kamati ya Shule, Mwalimu Mkuu, Mwalimu Mkuu Msaidizi, Mwalimu wa Taaluma, Mwalimu wa Nidhamu, Mwalimu wa Darasa na Viongozi wa Wanafunzi. Wajibu wa viongozi wa shule ni kusimamia maendeleo ya shule kwa ujumla. Majukumu ya viongozi wa shule yanatofautiana kama ifuatavyo:

**Kamati ya shule:** Kisheria, kila shule ya msingi inatakiwa kuwa na kamati ya shule. Kamati ya shule ni kikundi cha wajumbe waliochaguliwa kwa ajili ya kuongoza na kuangalia shughuli za shule ya msingi. Kamati ya shule inatakiwa kuwa na wajumbe nane au wajumbe tisa kama shule ina kitengo kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Wajumbe hao ni; Mwalimu Mkuu ambaye ndiye atakuwa katibu wa kamati ya shule, Mwalimu wa Taaluma katika shule, walimu wawili ambao watakuwa wawakilishi wa walimu wenzao, mkuu wa kitengo cha wanafunzi wenye mahitaji maalumu, wajumbe watatu watakaochaguliwa na mkutano wa wazazi, na mjumbe mkazi jirani mmoja ambaye atateuliwa na Mwalimu Mkuu. Mwenyekiti wa kamati ya shule na makamu wake atachaguliwa na wajumbe wa kamati ya shule kutoka miongoni mwa wale wajumbe watatu waliochaguliwa na mkutano wa wazazi.

**Majukumu ya Kamati ya shule:** Kamati ya shule ina jukumu la kuandaa na kuidhinisha mipango ya maendeleo ya shule na mikakati ya utekelezaji wake. Kamati hiyo itaitisha na kuendesha vikao vya wazazi na kutoa taarifa ya maendeleo ya shule kitaaluma, michezo, na miundombinu. Vilevile, kamati ya shule ina wajibu wa kuidhinisha na kusimamia matumizi bora ya fedha za maendeleo na uendeshaji wa shule. Aidha kamati ya shule inawajibika kusimamia ujenzi na ukarabati wa madarasa na miundombinu na utunzaji wake. Kusimamia ufundishaji na ujifunzaji pamoja na mahudhurio ya walimu na wanafunzi ni wajibu mwingine wa kamati ya shule.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muda wa kamati ya shule kuwa madarakani tangu ichaguliwe ni miaka mitatu. Endapo mkutano wa wazazi utaridhia na kuwapendekeza tena wajumbe hao wa kamati inayomaliza muda wake, basi wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kinachofuata.

**Majukumu ya Mwalimu Mkuu:** Mwalimu Mkuu ni kiongozi na msimamizi mkuu wa shughuli zote za uongozi na utawala katika shule. Pia, ana jukumu la kusimamia utekelezaji wa mtaala wa elimu na tathmini ya maendeleo ya shule kitaaluma. Aidha, ana jukumu la kusimamia ustawi wa wanafunzi, kuweka kumbukumbu za wanafunzi, kudhibiti nidhamu ya walimu, wanafunzi, na wafanyakazi wasio walimu katika shule yake.

Katika kusimamia rasilimali za shule, Mwalimu Mkuu kama mtendaji mkuu na msimamizi wa mali za shule, ana wajibu wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo utaratibu wa kuzitumia rasilimali hizo kwa uadilifu, uaminifu na umakini ili kuleta ufanisi shuleni. Pia, Mwalimu Mkuu analo jukumu la kujenga na kuimarisha uhusiano mzuri na wadau mbalimbali wa elimu katika ngazi za halmashauri, kata, kijiji au mtaa, asasi binafsi na madhehebu ya dini.

Ni wajibu wa Mwalimu Mkuu kutoa motisha kwa walimu na wafanyakazi wasio walimu ikiwemo kuwahusisha walimu katika mchakato wa kupanga na kufanya uamuzi unaohusu uendeshaji wa shule. Mwalimu Mkuu anawajibika kwa mamlaka za juu kama vile, Ofisa Elimu wa Mkoa, Mkurugenzi wa Manispaa au Halmashauri, Ofisa Elimu wa Wilaya na Ofisa Elimu wa Kata. Mwalimu Mkuu huteuliwa na Ofisa Elimu wa Wilaya.

**Majukumu ya Mwalimu Mkuu Msaidizi:** Majukumu ya Mwalimu Mkuu Msaidizi ni kumsaidia Mwalimu Mkuu kuongoza shule. Pia, hupanga zamu za walimu, huwasimamia walimu wa taaluma, miradi, mazingira, uchumi na mipango, michezo, afya na nidhamu. Vilevile, hukaimu madaraka kutoka kwa Mwalimu Mkuu na kusimamia maagizo mbalimbali apewayo kutoka kwake.

**Majukumu ya Mwalimu wa Taaluma:** Majukumu ya Mwalimu wa Taaluma ni kumshauri Mwalimu Mkuu katika mambo yote yahusuyo taaluma. Mwalimu wa Taaluma ni mwenyekiti wa kamati ya taaluma katika shule husika. Ana jukumu la kuhakikisha mihtasari na vitabu, maazimio na maandalio ya masomo yote yanayofundishwa yanakuwepo na kuhifadhiwa sawasawa kwa kumbukumbu. Pia, huratibu mitihani yote ya ndani na nje inayofanyika katika shule husika. Vilevile, huandaa ratiba kuu ya masomo na kuhakikisha walimu wanaifuata na kuzingatia kila siku katika ufundishaji wao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Majukumu ya Mwalimu wa Nidhamu:** Mwalimu wa Nidhamu husimamia utii, heshima na maadili ya wanafunzi wote na kuhakikisha kuwa wanafuata sheria za shule. Hutoa ushauri kwa wanafunzi na wazazi juu ya mambo mbalimbali yahusuyo tabia za watoto wao. Hushughulikia tuzo na zawadi mbalimbali za wanafunzi. Ana wajibu wa kuwaonya na kuwakanya wanafunzi wanapokosa akishirikiana na kamati ya nidhamu, mwalimu wa zamu na viranja wa zamu.

**Majukumu ya Mwalimu wa Darasa:** Mwalimu wa darasa ana jukumu la kuongoza darasa na kuchukua mahudhurio ya wanafunzi ya kila siku katika darasa lake. Husimamia nidhamu na kuandaa matokeo ya mitihani ya wanafunzi wa darasa lake. Hutunza mali za darasa lake kama vile viti, madawati, mbao za matangazo na ubao wa kufundishia na kujifunzia. Pia, ni kiunganishi kati ya Mwalimu Mkuu, wazazi na wanafunzi wa darasa lake. Huandaa ratiba ya masomo na kusimamia usafi wa darasa lake. Huhakikisha vipindi vyote vya siku katika ratiba vinafundishwa katika darasa lake. Hutoa na kupokea maombi ya ruhusa kwa wanafunzi wa darasa lake akishirikiana na mwalimu wa zamu.

**Majukumu ya viongozi wa wanafunzi (viranja):** Viranja huongoza wanafunzi. Viranja hao huchaguliwa na wanafunzi, kisha hufanya kazi kwa kushirikiana na walimu au wanafunzi wenzao. Baadhi ya kazi za viranja ni kusimamia nidhamu ya wanafunzi, kusimamia usafi wa mazingira na kuwasimamia wanafunzi katika utekelezaji wa majukumu yao. Viranja wana jukumu la kufikisha taarifa kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi wenzao. Kiranja mkuu ndiye mwenyekiti wa baraza la wanafunzi.

## Zoezi la 2

1. Taja wajumbe wa kamati ya shule.
2. Mwalimu Mkuu huteuliwa na nani?
3. Mwalimu wa Taaluma ana majukumu gani?
4. Taja kazi anazofanya mwalimu wako wa darasa.

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wenzako jinsi viranja wa shule yenu wanavyotekeleza majukumu yao. Andika mlichojadili katika daftari lako la mazoezi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 99 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mbinu za kurahisisha usimamizi wa majukumu shuleni

Kuna mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kurahisisha usimamizi wa majukumu mbalimbali shuleni. Mbinu hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

**Kudhibiti nidhamu shuleni:** Nidhamu hudhibitiwa kwa kutoa elimu ya tabia mbalimbali zisizofaa. Elimu hiyo hutolewa kupitia sheria za shule. Sheria hizi huwaongoza walimu na wanafunzi, kufuata taratibu za shule zilizowekwa. Nidhamu nzuri shuleni husababisha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo.

**Kuboresha kiwango cha taaluma shuleni:** Matokeo mazuri ya shule kitaaluma ndio lengo kuu la shule yoyote nchini. Kamati ya taaluma inapaswa kuwahamasisha walimu wote kufundisha kwa bidii ili kuboresha taaluma kwa wanafunzi. Masomo ya ziada na motisha mbalimbali huweza kusaidia kuinua kiwango cha taaluma shuleni.

**Kuimarisha ushirikiano baina ya walimu na wazazi au walezi:** Mwalimu Mkuu na walimu wenzake wanapaswa kuifanya shule kuwa kituo bora cha malezi. Wanapaswa pia kuwaelimisha wazazi kuwa shule ni sehemu ya jamii yao. Ushirikiano mzuri kati ya walimu, wazazi na jamii kwa ujumla husaidia watoto kujifunza vizuri na hatimaye hupata maendeleo mazuri kitaaluma na kimaadili.

**Kudumisha mawasiliano:** Ni muhimu kuimarisha mawasiliano kati ya shule na wazazi na wadau mbalimbali ili kudumisha nidhamu na taaluma shuleni. Mawasiliano yakiimarishwa vizuri huweza kuunganisha wanafunzi, wazazi na wadau mbalimbali na kuleta maendeleo ya shule.

**Vikao vya Wazazi:** Vikao ni nguzo muhimu sana katika usimamizi wa majukumu shuleni. Uongozi wa shule unapaswa kujua umuhimu wa vikao hivi ambavyo maazimio yake huwezesha kusimamia nidhamu na taaluma shuleni. Lengo kuu la vikao ni kutoa fursa ya kubadilishana mawazo, kufafanua baadhi ya mambo na kuainisha mikakati mbalimbali ya kuboresha mazingira, taaluma na nidhamu katika shule.

**Siku ya wazazi:** Siku hii huweza kufanyika kila muhula au mara mbili kwa mwaka ili wazazi au walezi wapate nafasi ya kutembelea shule, kujua na kujadili maendeleo ya kitaaluma ya watoto wao ndani na nje ya darasa na kupata fursa ya kutoa maoni yao. Pia, walimu hutoa taarifa zao kwa wazazi ili kuona mbinu zipi zingetumika kudumisha nidhamu na kuinua maendeleo ya shule kwa ujumla.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 100 2021/08/04 11:14


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mbinu hizi zikitumika ipasavyo zitasaidia kuinua kiwango cha taaluma na zitajenga nidhamu bora kwa wanafunzi kwani zitarahisisha usimamizi wa majukumu shuleni.

## Zoezi la 3

1. Eleza maana ya majukumu.
2. Eleza umuhimu wa nidhamu shuleni katika maendeleo ya mwanafunzi.
3. Taja mbinu zinazoweza kutumika kurahisisha usimamizi wa majukumu shuleni.
4. Eleza umuhimu wa kufanya shule kuwa kituo cha malezi.

## Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa kuwa na vikao vya wazazi/walezi katika kusimamia majukumu shuleni. Andika umuhimu huo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuwashirikisha watu katika utekelezaji wa majukumu

Ushirikishwaji wa watu katika utekelezaji wa majukumu ni jambo muhimu katika kujenga jamii yenye kuheshimu kazi kama msingi wa kufanikisha maendeleo yao.

**Faida za kuwashirikisha watu katika kutekeleza majukumu**

Kuna faida mbalimbali za kuwashirikisha watu katika kutekeleza majukumu yao. Faida hizo ni pamoja na:

(a) Kuongeza motisha na morali ya kazi kwa kuwa watu watajituma na kuona kazi kama yao;

(b) Kuongeza uwajibikaji wa viongozi na wanajamii kwa kuwa kila mmoja anajua amepewa dhamana ya kusimamia shughuli husika na atawajibika nayo;

(c) Kujenga nidhamu ya kazi kwa kuwa watu watatekeleza wajibu wao kama sehemu ya maisha yao ya kila siku hivyo kuondoa uvivu, utegaji kazi na uzururaji;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa ufanisi mkubwa kutokana na kila mmoja kutimiza wajibu wake ipasavyo;
(e) Kuwafanya viongozi kujiamini na kuaminiwa kwa kuwa wanaongoza kwa uwazi na ukweli. Kila mtu hushiriki na hufahamu kila kitu kinachoendelea; na
(f) Kusaidia kupunguza ufisadi, ubadhirifu, rushwa na matumizi mabaya ya madaraka kwa kuwa wananchi na viongozi wao hufanya kazi bega kwa bega katika kutekeleza majukumu yao.

Pamoja na faida hizo, kuna hasara za kutowashirikisha watu wengine katika kutekeleza majukumu yao.

**Hasara za kutowashirikisha watu katika kutekeleza majukumu**

Kuna hasara kubwa inayoweza kutokea pale ambapo watu wengine hawashirikishwi katika kutekeleza majukumu yao. Hasara hizo ni kama zifuatazo:

(a) Huweza kusababisha migogoro isiyo ya lazima kati ya viongozi na wale wanaoongozwa;
(b) Husababisha kukwama kwa shughuli mbalimbali kwa kuwa watu hawaoni umuhimu wa kujituma;
(c) Huondoa umoja na mshikamano wa watu katika kazi kwa kuwa kinachofanyika hawakielewi hivyo kukuza usaliti na unafiki katika kutekeleza majukumu;
(d) Husababisha viongozi kutojiamini na kukosa amani kwa kosa la kutowashirikisha watu wengine kutekeleza majukumu na hatimaye shughuli kuharibika;
(e) Ufanisi kupungua kwa kuwa kila mtu anafanya kile anachokijua kutokana na ukosefu wa mpango kazi unaoeleweka kwa watu wote. Hii hufanya watu kutokuwa na motisha; na
(f) Hufifisha uzalendo na kuchochea ufisadi kwa kuwa watu hawaoni faida ya kile wanachokifanya.

## Lugha inayounganisha watu katika kutekeleza majukumu

Katika jamii yoyote, lugha ni kiunganishi muhimu katika shughuli za utekelezaji majukumu ya kila siku. Lugha husaidia jamii katika utekelezaji wa majukumu kwa namna zifuatazo:

(a) Matumizi ya lugha yenye staha huwafanya watu kuwa wasikivu, hivyo kurahisisha uelewa wa kile wanachoelekezwa;



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Lugha huwaunganisha watu, hujenga umoja, upendo na uzalendo katika kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa;


(c) Ili lugha iweze kuwaunganisha watu ni lazima izingatie utu na maadili ya jamii; na

(d) Lugha yenye kueleweka na watu wote huwezesha shughuli iliyokusudiwa kutekelezwa kikamilifu na malengo kufikiwa.

## Zoezi la 4

1. Kuna faida zipi za kuwashirikisha watu katika kutekeleza majukumu?
2. Eleza hasara zinazoweza kujitokeza usipowashirikisha watu katika kutekeleza majukumu.
3. Ni majukumu gani uliyoshirikishwa nyumbani na ukayatekeleza?
4. Eleza namna walimu wanavyowashirikisha katika kutekeleza majukumu yenu shuleni.
5. Ushikirishwaji wa majukumu umeisaidiaje jamii katika eneo unaloishi?

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wenzako jinsi lugha ilivyokuunganisha na wenzako katika kutatua changamoto za masomo shuleni. Andika mlichojadiliana katika daftari lako la mazoezi.

### Kushirikiana na wanajamii katika shughuli za maendeleo

Kila jamii inahitaji maendeleo katika sekta mbalimbali ili iweze kustawi na kuendelea. Maendeleo hayo yanaweza kuwa ya mtu mmoja mmoja au ya vikundi. Ili kikundi kiweze kufanikiwa katika kutimiza malengo yake, kinapaswa kuwa na misingi ambayo itafuatwa na kila mwanachama wa kikundi hicho. Baadhi ya vikundi vimeweza kupitisha kanuni za kusimamia vikundi vyao. Miongoni mwa kanuni hizo ni:

(a) Kuheshimiana;
(b) Kufanya kazi kwa kujituma;
(c) Kutii sheria;



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 103 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kufichua maovu katika kikundi;
(e) Kushauri; na
(f) Kuadhibu kwa mujibu wa sheria.

*Soma habari na mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Naseku na Kisali ni marafiki. Wanasoma Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Oldonyosambu. Marafiki hawa huishi na wazazi wao katika miteremko ya Mlima Meru. Tangu walipokuwa wadogo walizoea kuwaona wazazi wao wakifanya kazi kwa kushirikiana. Mara nyingi walishirikiana katika kulima mashamba ya familia zao na wakati mwingine walichunga mifugo yao kwa pamoja. Vijana hawa walivutiwa na jinsi wazazi wao walivyoshirikiana katika kazi na mambo mbalimbali yanayohusu nyumba zao. Wazazi wa Naseku na Kisali walisifiwa kutokana na ushirikiano wao ambao umewawezesha kufanya mambo mengi ya kimaendeleo ikiwemo kujenga nyumba, na kumiliki mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kuku.

Siku moja baada ya kipindi cha Uraia na Maadili, mwalimu wa somo hilo aliwapa kazi ya kuunda kikundi kwa ajili ya kuelimisha wenzao juu ya ushirikiano na wengine. Marafiki hawa walifurahi sana kupata nafasi hii kwani wanao mfano mzuri wa ushirikiano kutoka kwa wazazi wao. Baada ya hapo waliwajulisha wanafunzi wenzao na wakapata majina ya wanafunzi wengine wanne ambao ni Lebayo, Matiila, Mandomi na Lesioni. Baada ya wanafunzi hao kupatikana, mwalimu aliwapa nafasi ya kukutana ili wapange malengo ya kikundi chao na jinsi watakavyowaelimisha wanafunzi wenzao. Walimchagua Naseku kuwa mwenyekiti na Kisali kuwa katibu. Katika mkutano wao, mazungumzo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Naseku**: Karibuni sana katika kikao chetu cha kwanza cha kamati. Kamati hii imepewa jukumu la kutoa elimu kwa wanafunzi wenzetu juu ya namna ya kushirikiana na wenzetu.

**Kisali**: Ili tufikie malengo yetu inabidi tujiwekee kanuni zitakazotuongoza kila siku. Je, kuna mtu mwenye wazo?

**Lebayo**: Ndiyo! Kwanza tunapaswa kujiwekea kanuni zitakazotuongoza.

**Naseku**: Na mimi naafiki, hivi kanuni hizo ni zipi? Ehee Mandomi!

**Mandomi:** Kwanza tunapaswa kuheshimiana sisi wenyewe na wote tutakaowaelimisha. Hii itatujengea picha nzuri mbele ya jamii.

**Naseku:** Zaidi ya heshima ni nini kingine zaidi? Ehee Lesioni!

**Lesioni:** Sote tunapaswa kufanya kazi kwa kujituma. Hii itatusaidia kukamilisha malengo yetu kwa wakati.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 104 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kisali** Mimi nakubaliana na Lesioni, hata hivyo tunapaswa kuheshimu ushauri wa mwingine na kutodharau mchango wa mtu yeyote.

**Naseku:** Lebayo nimekuona ukinyoosha mkono, una la kuongeza?

**Lebayo:** Asante mwenyekiti, sote tunapaswa kuwa waangalifu na tunapoona kuna jambo lolote ovu linaendelea katika kazi zetu, inatupasa kulifichua mara moja.

**Naseku:** Asante sana kwa kutukumbusha, Matiila una cha kuongeza?

**Matiila:** Ninacho! Sote tunapaswa kutii sheria zote za shule ili tuwe mfano kwa wenzetu.


**Kisali:** Hata mimi naafikiana nawe, pia tukubaliane kuwa iwapo mmoja wetu atakiuka sheria za shule au kanuni zetu, basi anapaswa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

**Naseku:** Nashukuru sana kwa mchango wa kila mmoja. Sasa tutaweza kupanga ratiba, malengo na madhumuni ya kikundi chetu.

## Zoezi la 5

1. Je, nini kiliwafanya Naseku na Kisali kupewa jukumu la kuongoza kikundi chao?
2. Umejifunza nini kutoka kwa wazazi wa Kisali na Naseku?
3. Ni mienendo gani ambayo wanakikundi walitakiwa kuiepuka ili kujenga kikundi chao?
4. Ni mambo gani mengine ungeshauri kikundi hiki kiyafanye zaidi ya uliyoyasoma?

## Kazi ya kufanya namba 6



Kwa msaada wa mzazi au mlezi tembelea kikundi chochote cha uzalishaji mali kilicho karibu na eneo unaloishi. Omba nafasi ya kuongea na kiongozi wao kuhusu kanuni anazotumia kurekebisha mienendo ya wanakikundi ili kufikia malengo yao. Andika kanuni utakazozipata katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Ushirikiano wa kundirika katika kufanya shughuli mbalimbali katika jamii

Katika jamii kuna makundirika mbalimbali yanayofanya shughuli tofauti tofauti kulingana na umri wao. Makundirika hayo yanayojumuisha kundi la vijana, watu wazima na wazee. Kila kundirika katika jamii lina wajibu wake wa kutekeleza. Ushirikishwaji wa makundirika katika kutekeleza shughuli mbalimbali hujitokeza pale makundi haya yanapojumuishwa katika uongozi. Uongozi unapoundwa na kujumuisha makundirika yote huleta umoja na usawa katika uongozi wa jamii.

Kushiriki katika vikao mbalimbali huwezesha kila kundi kutoa mawazo mbalimbali ya maendeleo yenye tija kwa jamii husika. Ushirikiano huu wa kundirika hujenga mshikamano katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii na kurahisisha utekelezaji wa maazimio ya vikao vya maendeleo. Kutambuliwa na kushirikishwa kwa kundirika huongeza morali na motisha ya kufanya kazi. Pia, ushirikishwaji hufanya makundi haya kuona yana umuhimu na nafasi katika kutekeleza shughuli za maendeleo kwenye jamii yao.

Kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa makundirika hufanya mgawanyo wa majukumu na usimamizi wake kuwa rahisi na hivyo uwajibikaji na ufanisi kuongezeka. Pia, ushirikiano hujenga hamasa na ushindani katika shughuli za maendeleo kwa kuwa kila kundirika hutaka kuonesha weledi katika majukumu waliyopewa na jamii.

FOR ONLINE USE ONLY

#### Zoezi la 6


1. Taja shughuli nne ambazo kundirika la vijana hufanya katika jamii unamoishi.
2. Eleza manufaa ambayo huletwa na ushirikishwaji wa kundirika katika shughuli za jamii.
3. Nani ana wajibu wa kuhamasisha ushirikiano wa kundirika katika shughuli za maendeleo ya jamii?



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 106 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 7



Jadiliana na wenzako mbinu za kuhamasisha kundirika kushiriki katika shughuli za maendeleo katika jamii unamoishi. Andika mbinu hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Kufichua maovu yanayohusiana na ufisadi katika utekelezaji wa majukumu

Ufisadi ni uharibifu au uozo uliopo katika jamii kwa sababu ya kukosekana kwa uadilifu. Ufisadi hutokea pale watu wenye dhamana wanapotanguliza mbele maslahi yao binafsi. Ufisadi unaweza kujitokeza kwa namna mbalimbali kama vile hongo, ubadhirifu, ulaghai, upokonyaji, upendeleo kwa ndugu au marafiki na matumizi mengine mabaya ya mali za umma. Mahali penye ufisadi majukumu hayatekelezwi kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo. Ufisadi ni kitu kibaya na kinapaswa kupigwa vita na wanajamii wote. Kazi ya kupiga vita ufisadi ni ngumu na inahitaji juhudi kubwa na uadilifu wa hali ya juu. Baadhi ya taarifa katika tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba hata baadhi ya wafanyakazi wa taasisi zilizowekwa na serikali kupambana na ufisadi nao pia hujihusisha na ufisadi.

Mapambano dhidi ya ufisadi yanapaswa kuelekezwa katika shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Pia, yanapaswa kuhusishwa na kujadiliwa pamoja na masuala mengine yanayohusiana na utawala bora, kama vile kukuza demokrasia, kuheshimu haki za binadamu na utunzaji wa mazingira.

### Athari za ufisadi katika kutekeleza majukumu

Ufisadi una athari kubwa kwa jamii. Baadhi za athari za ufisadi ni kama zifuatazo:

(a) Kudumaa kwa maendeleo ya watu katika jamii kwa vile fedha zilizotengwa kwa matumizi stahiki ya maendeleo huelekezwa katika matumizi mengine kinyume na utaratibu;

(b) Kuzuka kwa uhasama na kutoelewana katika jamii kutokana na tabia za upendeleo unaofanywa na baadhi ya viongozi wa umma au taasisi nyingine kwa misingi ya rangi ya mtu, ukabila, udini au ukanda;

(c) Wananchi wanaweza kupuuza wajibu wao wa kulipa kodi na kutoshiriki katika shughuli za maendeleo ya taifa;

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 107 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kuongezeka kwa matabaka ya watu kati ya matajiri na masikini katika jamii kutokana na kushamiri kwa matendo ya kifisadi;

(e) Kuongezeka kwa uhalifu katika jamii kutokana na vyombo au mamlaka za usimamizi kama polisi na mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(f) Huduma za jamii kama vile elimu, afya, umeme na maji kutolewa chini ya kiwango kilichokusudiwa kutokana na fedha zilizotengwa kwa huduma hizo kuliwa na baadhi ya viongozi wasio waadilifu;

(g) Ufisadi waweza kuhatarisha amani na usalama wa nchi. Kwa mfano, kuzuka kwa migogoro na vita miongoni mwa jamii inayopigania haki dhidi ya uonevu na dhuluma; na

(h) Wananchi kutokuwa na imani na uongozi wa nchi na serikali kwa ujumla.

### Jinsi ya kuzuia na kupambana na ufisadi katika jamii

Viongozi katika kila ngazi ya utawala wana wajibu wa kutengeneza mazingira rafiki kwa jamii ili kutokomeza ufisadi. Baadhi ya njia zinazoweza kutumiwa kuzuia na kupambana na ufisadi ni:

(a) Viongozi kutenda wanachosema na kuwa mfano wa kuigwa kwa kukemea ufisadi kwa uwazi na kuuzuia kwa bidii;

(b) Kujenga utamaduni wa uwazi ambao utawezesha watu kuwasiliana kwa uwazi na kutoa taarifa zinazohusu ufisadi katika jamii na namna ya kukabiliana na changamoto hiyo;

(c) Mahakama na vyombo vya usalama kama polisi kuwa waadilifu na kusimamia ipasavyo sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa dhidi ya ufisadi na mafisadi; na

(d) Bunge kufanya rejea ya sheria za ufisadi mara kwa mara ili kudhibiti mbinu zinazobuniwa na mafisadi kutekeleza matakwa yao.


### Zoezi la 7

1. Nini maana ya ufisadi?
2. Taja njia tano ambazo ufisadi hujitokeza.
3. Taja athari tano za ufisadi katika maendeleo ya jamii.
4. Eleza njia tano za kuzuia na kupambana na ufisadi katika jamii.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 8



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu sababu za kuwepo kwa ufisadi katika jamii yetu. Andika sababu hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Taarifa juu ya vitendo vya utoaji na upokeaji rushwa

Neno rushwa lina dhana pana kwa sababu jamii na mataifa mbalimbali yanalitafsiri kulingana na mazingira yao ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kwa kadri ya imani zao za dini. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya 2004 toleo la pili, rushwa inatafsiriwa kuwa ni fedha au kitu chochote aghalabu cha thamani kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili apate kupendelea au kutoa haki au kitu kwa asiyestahiki. Katika mazingira fulani, rushwa imetafsiriwa kuwa ni kitu chochote chenye thamani ambacho hutolewa na wakati mwingine kuombwa ili kununua haki ambayo yawezekana mtoaji au mwombaji wa rushwa hakustahili na kama alistahili basi hakuamini kama angepata haki au huduma hiyo. Rushwa haihusishi malipo ya pesa taslimu pekee, bali pia huhusisha utoaji wa kitu chochote cha thamani kwa mtu mwenye madaraka ili mtoaji rushwa apatiwe upendeleo.

Tendo la rushwa hutokea pale mtu anapoamua kupindisha sheria na taratibu za nchi kwa nia ya kujipatia manufaa binafsi, aidha kwa kuahidiwa au kupatiwa kiasi fulani cha pesa au kitu chochote chenye thamani hata kama kitu hicho kina thamani ndogo sana.

Rushwa ni pamoja na hongo, ubadhirifu au ufujaji, kuchepusha au kubadili matumizi ya mali ili kujinufaisha, kujilimbikizia mali zisizolingana na kipato halali, kutumia nyaraka kwa nia ya kudanganya ili kujipatia manufaa, huku mpokeaji akijua fika kwamba atatoa maamuzi katika jambo linalomhusu mtoaji.

Rushwa imekuwa ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania na imesababisha hasara kubwa kwa serikali. Wajibu mkubwa wa serikali ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na maendeleo endelevu. Rushwa inadhoofisha uwezo wa serikali katika harakati za kuwaletea wananchi maendeleo yao.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 109 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sababu za rushwa**

Uwepo wa rushwa katika jamii unasababishwa na vyanzo tofauti. Baadhi ya sababu hizo zinaweza kuwa katika makundi yafuatayo:

***(a)*** ***Kiuchumi:*** Umaskini, kupanda kwa gharama za maisha, ukosefu au uhaba wa vitendea kazi;

***(b)*** ***Kisiasa:*** Ubinafsi, kulindana kiitikadi ili kutimiza maslahi binafsi; na

***(c)*** ***Kijamii:*** Ukubwa wa familia, mashindano katika jamii.

**Aina za rushwa**

Rushwa inaweza kugawanywa katika makundi mawili; rushwa ndogo na rushwa kubwa. Rushwa ndogo ni ile inayotokea kila siku hususan kwa maofisa wa ngazi ya chini ambapo mtu hutoa fedha kwa lengo la kupata huduma ama upendeleo. Mifano mingine ni pale mtu anapotoa fedha au zawadi nyingine ili aweze kupata huduma kama leseni ya udereva, huduma za afya, nafasi ya kazi, au kutoa pesa ili ashinde kesi au apunguziwe kodi kinyume na sheria.

Rushwa kubwa hutokea ambapo maofisa wa ngazi za juu hutumia mamlaka yao kubadili au kutoa maamuzi kinyume na taratibu baada ya kupokea rushwa. Hii ni kama vile, mtu kutoa fedha ili ashinde zabuni ya miradi mikubwa ya fedha nyingi kama vile, ujenzi wa reli, barabara, visima vya maji, miradi ya umeme, sare za majeshi na ununuzi wa mitambo. Aina hii ya rushwa inahusu ubadhirifu wa fedha nyingi za umma. Rushwa ya namna hii huonesha jinsi maofisa hao wanavyoshindwa kusimamia majukumu yao.

**Uwepo wa TAKUKURU**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ipo kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007. TAKUKURU imekabidhiwa jukumu la kuongoza na kuratibu mapambano dhidi ya rushwa hapa Tanzania.

***Malengo ya TAKUKURU***

Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 malengo ya TAKUKURU ni mawili ambayo ni:

(a) Kuhakikisha nchi inaongozwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora; na

(b) Kuhakikisha rushwa inatokomezwa nchini.

***Majukumu ya TAKUKURU***

Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 hususani kifungu cha 4 kikisomwa pamoja na kifungu cha 7, kimeainisha

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 110 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

majukumu ya TAKUKURU ambayo yakitekelezwa ipasavyo yanatimiza malengo ya TAKUKURU. Majukumu yaliyoainishwa ni mawili ambayo ni:

(a) Kuzuia rushwa; na
(b) Kupambana na rushwa.

***Utekelezaji wa majukumu ya TAKUKURU***

Kifungu cha 4 kikisomwa pamoja na cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 kimeainisha mbinu zitakazotumika wakati wa kutekeleza majukumu ya TAKUKURU kama ifuatavyo:

*Jukumu la Kuzuia Rushwa*

Katika kutekeleza jukumu la kuzuia rushwa TAKUKURU imeelekezwa kisheria kufanya yafuatayo:

(a) Kupitia na kuchambua sheria, mifumo ya utendaji na mifumo ya utoaji huduma, kwa lengo la kubaini kama kuna mianya au viashiria vya uwepo wa rushwa;
(b) Kutoa ushauri wa namna ya kuzuia na kupambana na rushwa ndani ya sekta za umma na binafsi;
(c) Kuelimisha umma kuhusu dhana ya rushwa na madhara yake;
(d) Kuhamasisha wananchi ili watambue ubaya wa rushwa na hatimaye wajiunge katika vita dhidi ya rushwa;
(e) Kufuatilia thamani ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya nchi; na
(f) Kujenga ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha vita dhidi ya rushwa inafanikiwa.

*Jukumu la kupambana na rushwa*

Katika kutekeleza jukumu la kupambana na rushwa TAKUKURU imeelekezwa kisheria kufanya yafuatayo:

(a) Kupokea na kuchambua malalamiko yanayohusu vitendo vya rushwa na makosa yaliyoanishwa kwenye sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa;
(b) Kuchunguza malalamiko yaliyopokelewa kwa lengo la kupata ushahidi wa kuthibitisha au kutothibitisha malalamiko yaliyopokelewa; na
(c) Kuwashitaki mahakamani watuhumiwa kwa mujibu wa sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na sheria nyinginezo.

**Njia za kutoa taarifa ya rushwa kutoka katika jamii kwenda TAKUKURU**

Jukumu la kutoa taarifa za rushwa ni la kila mtu kwa mujibu wa sheria. Kila mtu ambaye anafahamu kusudio la kutendwa kwa kosa la rushwa ana



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wajibu wa kutoa taarifa moja kwa moja katika ofisi za TAKUKURU. Taarifa hiyo itakuwa ni siri kwa lengo la kulinda usalama wa mtoa taarifa. Taarifa za rushwa hutolewa kwa njia zifuatazo:

(a) Mwananchi anaweza kutoa taarifa za rushwa kwa kupiga simu ya bure namba 113 au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba *113#;

(b) Mwananchi anaweza kufika katika ofisi za TAKUKURU kutoa taarifa dhidi ya wale wote wanaojihusisha na masuala ya utoaji ama upokeaji rushwa ili waweze kushtakiwa mahakamani kwa mujibu wa sheria;

(c) Mwananchi anaweza kutoa taarifa ya rushwa kwa kuandika barua na kuituma kwa njia ya posta iliyo karibu naye au kutumia njia nyingine kama vile nukushi; na

(d) Mwananchi anaweza pia kutoa taarifa ya rushwa kwa kuandika taarifa na kutuma kwa njia ya baruapepe kwenda ofisi ya TAKUKURU.

**Namna rushwa inavyoweza kupunguzwa**

Njia kuu ya kuweza kupambana na kupunguza rushwa nchini ni kuweza kuziishi tunu za taifa ambazo ni utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwajibikaji na uwazi.

***Utu***

Kutanguliza utu katika matendo yetu yote kama binadamu, uungwana, kupenda haki, kauli njema na hekima.

***Uzalendo***

Juhudi ya kila mmoja wetu kwa pamoja katika kuipenda moyoni na kuitangaza nchi yetu katika matendo.

***Umoja***

Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, vita ya dhidi ya rushwa kwa umoja itapunguza na kuondoa kabisa tatizo hili tukishirikiana sote, na hili linafanikiwa ikiwa wananchi wote tutakuwa na nia moja ya kupinga rushwa.

***Uadilifu***

Hii ni hali ya kitu kuwa sawa kama invyopaswa kiwe, kuhukumu kwa haki bila ya upendeleo, kufanya lililo jema na haki bila kupendelea upande wowote.

***Uwajibikaji***

Uwajibikaji ni nyenzo mojawapo ya kuzuia rushwa sehemu za kazi. Kila mmoja wetu akiwajibika katika sehemu yake na akitambua kuwa yeye ni chachu ya mendeleo na mafanikio. Ili kuhakikisha uwajibikaji unazingatiwa, yafuatayo ni vyema yakatiliwa maanani:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Viongozi kuwa na uwezo wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wasiowajibika;
(b) Taarifa zitolewe kwa wakati, ziwe za ukweli, kamilifu na zinazoeleweka; na
(c) Sheria zilizopitwa na wakati zirekebishwe.


***Uwazi***

Ni moja ya nguzo za kuimarisha utawala bora na kupunguza rushwa, uwepo wa uwazi katika utendaji kazi na hasa katika mapato na matumizi.

## Zoezi la 8

1. Eleza maana ya rushwa.
2. Taja njia zinazoweza kutumika kutoa taarifa ya rushwa katika jamii.
3. Ni namba gani ya simu hutumika kutoa taarifa za rushwa TAKUKURU?
4. Taja majukumu ya TAKUKURU.

## Kazi ya kufanya namba 9



Jadiliana na mwalimu wenu wa somo kuhusiana na madhara ya rushwa kwa maendeleo ya shule yenu. Andika madhara hayo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 9

**A:** *Andika* ***Kweli*** *kwa sentensi iliyo sahihi na* ***Si Kweli*** *kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

1. Ushirikiano wa makundirika katika kutekeleza shughuli za maendeleo ni jambo muhimu katika jamii.________
2. Kamati ya shule inawajibika kushughulikia changamoto ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu katika shule husika.________
3. Mtendaji mkuu katika kamati ya shule ni Mwalimu Mkuu.________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Rushwa ni adui wa haki.________
5. Taarifa za rushwa huweza kutolewa kwa njia ya simu, mabango, barua au televisheni. ________
6. Madhara ya kutowashirikisha watu wengine katika kutoa uamuzi ni kuwafanya watu wagawanyike katika makundi na kufanya morali ya kazi kupungua.________
7. Lugha inayotakiwa kuunganisha watu katika kutekeleza majukumu yao ni ile yenye staha na yenye kuwaunganisha watu.________
8. Ukweli wa jambo hubainika kwa kusilikiza upande mmoja.________
9. Wajibu wa watoto katika familia ni kusoma tu.________
10. Baba na mama ni viongozi wenye hadhi sawa katika familia.________

**B:** *Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na kipengele kutoka **Sehemu B** ili kupata maana sahihi, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| *Majukumu ya viongozi wa shule* | *Cheo* |
| 11. Huandaa mipango ya maendelelo ya shule | (a) Mwalimu Mkuu wa shule |
| 12. Hupanga zamu za walimu | (b) Kiranja Mkuu |
| 13. Husimamia maadili | (c) Mwalimu wa Taaluma |
| 14. Huandaa ratiba | (d) Kamati ya shule |
| 15. Husimamia utekelezaji wa mtaala wa elimu shuleni | (e) Mwalimu wa Nidhamu |
| | (f) Mwalimu wa Darasa |
| | (g) Mwalimu Mkuu Msaidizi |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Hongo | fedha au kitu cha thamani anachotoa au kupewa mtu ili kutoa au kupata huduma asiyostahili |
| Ubadhirifu | ni tabia ya kutumia fedha au mali bila ya utaratibu mzuri |
| Ulaghai | uzungumzaji wa maneno yasiyo ya kweli, uongo au udanganyifu |



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 114 2021/08/04 11:14
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Kutii sheria na kanuni

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza umuhimu wa kutii sheria na kanuni za shule. Katika sura hii, utajifunza kutambua sheria za nchi na kuzifuata, kuoanisha utekelezaji wa sheria na kanuni katika maisha, kuhoji sheria na kanuni zinazotumika, na kutathmini hatua zinazochukuliwa kudhibiti uvunjifu wa sheria. Umahiri huu utakusaidia kutambua sheria na kanuni za nchi yako, kutathmini utekelezaji wake na kuzifuata. Aidha, utaweza kukusaidia kuhamasisha watu wengine katika jamii kutii sheria za nchi ili kudumisha amani.*

### Kutambua sheria za nchi na kuzifuata

Sheria ni kanuni zinazoongoza taratibu za uamuzi na utendaji wa jambo. Pia, sheria ni mamlaka au amri zilizowekwa ili kulinda au kuhakikisha eneo fulani linafanikiwa bila kujali kupenda kwa watu au kutopenda kwao. Kila jamii ina taratibu ilizojiwekea ambazo zinatakiwa kufuatwa na kila Mtanzania kuanzia katika ngazi ya familia hadi taifa. Sheria zimewekwa ili kuhakikisha kuwa jamii zinaishi kwa amani, upendo, furaha na maelewano. Vilevile, sheria zinatumika kudhibiti usalama wa watu na mali zao. Athari za kutotambua sheria na kuzifuata ni watu kuishi maisha yasiyo na utaratibu. Hivyo, kila Mtanzania anapaswa kuishi kwa kufuata na kutii sheria na taratibu zilizowekwa katika nchi. Kutii sheria ni kufuata maelekezo uliyopewa kuhusu eneo husika bila kusimamiwa na mtu au kiongozi. Halikadhalika, utii wa sheria ni nidhamu au usikivu wa kufuata sheria, kanuni, na taratibu zilizowekwa. Katika kutii sheria hakuna mbadala, kinachotakiwa ni kufuata maelekezo halali yaliyotolewa na mamlaka husika. Serikali ya Tanzania imefanya jitihada mbalimbali tangu uhuru zenye lengo la kuhamasisha utii wa sheria na kanuni ili kudumisha uadilifu katika jamii. Jitihada hizo ni pamoja na kutunga sheria za kupambana na utoaji na upokeaji wa rushwa na matendo mengine ya mmomonyoko wa maadili.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 115 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Misingi ya utawala wa sheria

Utawala wa sheria unawawezesha wanajamii kutii sheria na kanuni mbalimbali zilizowekwa ambazo zitawasaidia kuishi kwa amani na utulivu katika maisha yao ya kila siku bila kubughudhiwa. Baadhi ya misingi ya sheria na kanuni ni kama ifuatavyo:

**Kuheshimu haki za binadamu:** Haki za binadamu ni mambo yote ya msingi ambayo kila binadamu anastahili kuyapata bila kubaguliwa, mfano; haki ya kupata elimu bora, chakula bora, malezi bora, kuishi, kuheshimiwa, kusikilizwa, kulindwa na kupendwa. Pia, kuna haki za kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi. Baadhi ya athari za kukiuka haki za binadamu ni kukosa elimu, kukosa afya bora, maadili kuporomoka, na kukosa maendeleo katika jamii.

**Kuwa na vyombo vya kutetea haki na kutoa uamuzi:** Baadhi ya vyombo vinavyotetea haki za binadamu hapa Tanzania ni pamoja na: Katiba ya nchi, Bunge, Mahakama, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, vyama vya watu wenye mahitaji maalumu na vyombo vya habari. Vyombo hivi havitakiwi kuingiliwa kwa namna yoyote ile katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

**Kuimarisha ulinzi na usalama wa raia:** Vyombo vya ulinzi na usalama vinatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria za nchi, kwa kuepuka kuvunja haki za binadamu pasipo sababu ya kufanya hivyo. Katika jambo hili, wananchi wanatakiwa kutoa ushirikiano wa kutosha kuvisaidia vyombo vya dola kutovunja haki za binadamu kwa wanajamii wote kutii sheria zilizowekwa bila shuruti. Vyombo vya dola ni kama vile; Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Magereza na Usalama wa Taifa.

**Kutoa fursa sawa:** Utawala wa sheria huzingatia fursa sawa katika utoaji wa huduma za jamii kwa wananchi wake. Kila raia anastahili kupata huduma bora za kijamii kama vile, elimu, afya, maji na huduma zingine zitakazomwezesha kumudu maisha yake ya kila siku. Huduma hizi za jamii ni lazima zitolewe kwa usawa kwa wananchi wote bila kujali hali zao kijamii, kisiasa au kiuchumi. Viongozi wenye mamlaka husika wanapaswa kutoa huduma hizi muhimu kwa wananchi wote bila kupendelea upande wowote. Utoaji wa huduma bora kwa jamii hutasaidia kuepuka migogoro itokanayo na kukosekana kwa haki na usawa katika utoaji wa huduma za jamii.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Eleza maana ya sheria.
2. Taja vitendo vinne vinavyoheshimu haki za binadamu.
3. Taja vyombo vinavyosimamia haki za binadamu nchini.

## Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa sheria za nchi. Andika vitendo hivyo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuhamasisha jamii kutii sheria za nchi

Hamasa ni ile hali ya watu kuwa na shauku ya kutaka kufanya jambo fulani. Katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii watu hutiwa hamasa ili kufanikisha jambo lililokusudiwa. Hivyo, ili kujenga jamii yenye nidhamu hatuna budi kuhamasisha jamii kutii sheria za nchi kwa kutumia njia mbalimbali.

**Kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutii sheria:** Elimu itatolewa kupitia vyombo vya habari, mikutano ya hadhara, mabango, maigizo na matangazo ya wazi. Jamii ikielimishwa juu ya kutii sheria itasaidia watu kuepuka matatizo, kupata haki zao, kutekeleza majukumu yao kwa amani, kujenga nidhamu katika utendaji kazi, kuepusha uhalifu katika jamii na kuongezeka kwa ufanisi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii.

**Kutekeleza kikamilifu matakwa ya sheria zilizopo kikamilifu:** Viongozi wenye dhamana wanapofuata sheria kuiongoza jamii husaidia jamii kufahamu sheria inavyofanya kazi. Kwa mfano, mwanajamii akishtakiwa kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji au Kata kwa kutenda kosa fulani, atapelekwa ofisi ya kijiji, kata ama kituo cha polisi kujibu mashtaka aliyotuhumiwa kwayo. Kwa kitendo hiki, huwafanya wanajamii kutii sheria.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Kuwepo kwa maadhimisho ya siku ya sheria:** Hii itasaidia jamii kuhamasika kutii sheria kwa kuwa siku hii huzungumzia namna jamii inavyoweza kutii sheria, kutumia sheria kupata haki, kutatua migogoro katika jamii, haki sawa kwa watu wote, kufahamu sheria mbalimbali, na vyombo vya kutoa haki.

**Vyombo vinavyosimamia sheria kutoa haki bila upendeleo:** Chombo kikuu cha usimamizi wa sheria ni mahakama. Kama chombo hiki kitatoa haki kwa usawa bila ya upendeleo, basi hali hii itawafanya wanajamii kuona faida ya kutumia chombo hicho na hatimaye kuwafanya waamini kuwa haki inapatikana kwa usawa na hivyo kuepuka uvunjifu wa sheria.

### Zoezi la 2

1. Taja vitendo vitatu vinavyoonesha uhamasishaji wa utii wa sheria shuleni kwako.
2. Kuna umuhimu gani wa kutii sheria katika jamii unamoishi?
3. Ni njia gani hutumiwa na wanajamii kuhamasisha utii wa sheria katika eneo unaloishi?
4. Taja athari nne za kutotii sheria za nchi.

### Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako jinsi vyombo vya habari vinavyoweza kuhamasisha utii wa sheria katika jamii. Andika katika daftari lako la mazoezi.

### Kuoanisha utekelezaji wa sheria na kanuni katika miktadha mbalimbali

Jamii yoyote ile huongozwa na kanuni, taratibu na sheria zinazofuatwa ili kujenga jamii yenye maadili mema na kudumisha amani na upendo katika miktadha mbalimbali.

**Matumizi ya sheria na kanuni katika miktadha mbalimbali**

Sheria hutungwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika miktadha tofauti kwenye jamii tunamoishi. Baadhi ya miktadha hiyo ni nyumbani, shuleni, barabarani na kazini.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 118 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Matumizi ya sheria na kanuni katika familia:*** Kila familia huwa na utaratibu wake wa kuiongoza ili kujenga familia bora na yenye nidhamu. Kwa mfano, wazazi au walezi huweka utaratibu unaoelekeza haki na wajibu wa kila mwanafamilia kushiriki kazi mbalimbali kama kuosha vyombo, kufanya usafi wa mazingira, kulisha mifugo na kwenda shambani.

***Matumizi ya sheria na kanuni katika maeneo ya shule:*** Sheria na kanuni husaidia kutekeleza na kufikia malengo yaliyokusudiwa na shule. Sheria hizi husaidia kujenga nidhamu kwa wanafunzi na huwapa walimu njia za kupambana na changamoto zinazojitokeza wakati wa kutekeleza majukumu ya kuwalea na kuwafundisha wanafunzi.

Kwa mfano, sheria zinazohusu mwanafunzi kuvaa sare za shule awapo shuleni, kuhudhuria darasani kila siku, kuwahi shuleni, kutopigana, kutotupa takataka ovyo na kutotumia lugha isiyofaa shuleni. Shughuli nyingi hufanikiwa kutokana na matumizi ya sheria za shule. Aidha, mwanafunzi anayo haki ya kufundishwa vizuri, kulindwa na kuheshimiwa utu wake.

***Matumizi ya sheria na kanuni katika michezo:*** Michezo huongozwa na sheria mbalimbali. Ili mchezo wowote ufanyike vizuri sharti kanuni, taratibu na sheria za mchezo husika zifuatwe. Kuna sheria za michezo mbalimbali kama vile ngumi, mpira wa miguu, pete, kikapu na wavu. Mathalani, mpira wa miguu una sheria kumi na saba zinazoongoza mchezo huo. Sheria hizo hueleza haki na wajibu wa washiriki.

***Matumizi ya sheria na kanuni katika matumizi ya miundombinu ya barabara:*** Sheria hizi husaidia matumizi sahihi ya barabara ili kuepusha ajali. Sheria hizi huwaongoza madereva na watembea kwa miguu. Kwa mfano, uwepo wa alama ya kivuko kwa watembea kwa miguu, mteremko mkali, punguza mwendo, barabara nyembamba, daraja au kona.

***Matumizi ya sheria katika utunzaji wa mazingira:*** Utunzaji wa mazingira huongozwa na sheria mbalimbali zinazosaidia kuyahifadhi na kuyalinda kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kwa mfano, sheria za uhifadhi wa vyanzo vya maji, fukwe za maziwa na bahari, kulima kandokando ya mito, kutovuna miti ovyo, utunzaji wa mapori tengefu, sheria za mipango miji na za uchimbaji wa madini.

***Matumizi ya sheria katika maeneo ya kazi:*** Kuna sheria zinazotumika ili kuwaongoza na kuwasaidia wafanyakazi kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 119 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Kwa mfano, kuna sheria za kumsaidia mfanyakazi kudai haki zake na kumchukulia mfanyakazi hatua za kinidhamu anapokiuka sheria hizo.

Hivyo, matumizi ya sheria, kanuni na taratibu ni muhimu yaendane na utekelezaji wa majukumu ya wanajamii katika miktadha mbalimbali ya maisha yao ya kila siku.

## Zoezi la 3

1. Utekelezaji wa sheria shuleni umekusaidiaje katika kujifunza?
2. Eleza manufaa ya sheria za usalama barabarani.
3. Kuna umuhimu gani wa kuwa na sheria za kuongoza familia nyumbani kwenu?

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wenzako jinsi utekelezaji wa sheria za utunzaji mazingira ulivyooanishwa na maisha yako ya kila siku. Andika majadiliano hayo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuhoji sheria na kanuni zinazotumika

Ni jambo muhimu sana kuwa na tabia ya kuhoji mambo kabla ya kutenda au kupokea sheria na kanuni na kuzitumia. Tabia ya kuhoji itakupa nafasi ya kuelewa zaidi na kuimarisha kile unachokitenda. Vilevile, itakujengea stadi za kutambua, kudadisi na kuelewa changamoto za watu wengine na kukuza kipaji chako. Aidha, kuhoji sheria na kanuni zinazotumika katika jamii unamoishi inakuza uelewa na kujenga ari ya kudai haki kwa mujibu wa sheria. Katika ngazi ya shule, tabia ya kuhoji sheria na kanuni jinsi zinavyotumika shuleni ni muhimu sana katika ujifunzaji wako kwani huongeza maarifa, hukuza ubunifu, pia huchochea ari ya uwajibikaji na utii wa sheria bila shuruti.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 120 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Momose ni mwanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Mapangala. Shule hii ni ya bweni. Kwa kawaida kila mwanafunzi anaporudi shuleni hapa kutoka likizo ndefu huagizwa kuleta vitu kadhaa kwa matumizi yake binafsi na ya shule. Baadhi ya vitu hivyo ni fagio, ndoo, sabuni za kufulia na kuogea, dawa za kusafishia vyoo na dawa za meno. Vitu hivi hukusanywa na walezi wa wanafunzi hao na kutunzwa stoo. Kisha hugawiwa kwa wanafunzi kadiri wanavyoomba na si lazima vitu vilivyoletwa vikatumiwa na mwanafunzi aliyevileta. Hali hii ilileta manung'uniko mengi kwa wanafunzi. Siku moja Momose alihoji uongozi wa shule kuhusu sheria inayowataka wao kukusanya stoo vifaa vyote walivyonunuliwa na wazazi au walezi wao kwa matumizi yao binafsi. Siku chache baada ya kuhoji uhalali wa sheria hiyo, uongozi wa shule ulibadilisha utaratibu wa kutumia vitu vya wanafunzi. Kila mwanafunzi alipoleta vifaa hivyo viliandikwa majina na kutumiwa na mwanafunzi husika. Wanafunzi wote walifurahia utaratibu huo mpya wa utumiaji wa vifaa vyao. Lakini uongozi wa shule uliendelea kusisitiza kuwa wanafunzi hawatatunza vifaa hivyo bwenini, ila vitatunzwa na walezi wao katika stoo ya shule.*

## Zoezi la 4

1. Kwa nini vifaa vya wanafunzi vilitunzwa stoo badala ya kuwaachia wanafunzi wavitunze bwenini?
2. Ni sababu gani zilizofanya wanafunzi kunung'unika walipopewa vifaa?
3. Ungepewa nafasi ya kuhoji sheria zinazotumika shuleni kwako ungehoji sheria gani?
4. Nini kilitokea baada ya Momose kuhoji uongozi wa shule?
5. Umejifunza nini kutokana na kisa hiki?

## Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu matatizo yanayotokea katika jamii mnamoishi yanayosababishwa na tabia ya wananchi ya kutohoji sheria na kanuni zinazotumika. Andika matatizo hayo katika daftari lako la mazoezi.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 121 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutathmini hatua zinazochukuliwa kudhibiti uvunjifu wa sheria na kanuni nchini

Tathmini ni utaratibu wa kupima na kuchunguza hali halisi kwa lengo la kupata taarifa zitakazowezesha mtu kufanya uamuzi unaohusu urekebishaji au uboreshaji wa mambo mbalimbali. Kutathmini hatua za kudhibiti uvunjifu wa sheria na kanuni nchini kumesaidia kuimarisha na kudumisha amani, usalama na utengamano katika jamii zetu.

## Kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi

Kodi ni malipo ya lazima ya kifedha au tozo maalumu iliyowekwa na serikali ili ilipwe na mtu binafsi, taasisi au shirika fulani kwa ajili ya kusaidia kuchangia au kuboresha matumizi ya serikali. Kodi inaweza kuwa ya moja kwa moja au isiwe ya moja kwa moja na inaweza kulipwa kwa fedha taslimu au kwa kufanya kazi. Kushindwa au kukwepa kulipa kodi ni kosa la jinai kwani unaweza kuadhibiwa kisheria.

*Kodi ya moja kwa moja:* Hii ni aina ya kodi ambayo inalipwa na mtu au taasisi au shirika moja kwa moja kwa serikali, mfano, kodi ya kipato kutokana na kazi fulani.

*Kodi isiyo ya moja kwa moja:* Hii ni aina ya kodi ambayo hailipwi na mtu, taasisi au shirika moja kwa moja kwa serikali bali inalipwa katika mfumo wa bidhaa au huduma, mfano, unaponunua bidhaa dukani au hotelini asilimia fulani ya bei huwa ni kodi na hupelekwa serikalini.

### Manufaa ya kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi

Kodi ni chanzo kikuu cha mapato ya serikali, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kulipa kodi kwa hiari. Nchi nyingi zilizoendelea duniani, zimeendelea kutokana na kodi zinazolipwa na wananchi. Baadhi ya faida za kulipa kodi ni:

***Kuongeza mapato ya nchi:*** Licha ya miradi ya kijamii, pia serikali inatumia mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye kodi kwa ajili ya kugharamia suala la ulinzi na usalama wa raia wake. Fedha hizi hutumika kuendesha majeshi, tafiti za kisayansi, pamoja na ulinzi wa mazingira.

***Kuanzisha na kuendeleza miradi ya maendeleo:*** Ulipaji wa kodi huisaidia serikali kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopangwa pamoja na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya biashara kwa wadau mbalimbali. Miradi hiyo ni kama vile, kuboresha miundombinu ya maji, umeme, barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege ili kuinua uchumi wa raia wake. Hivyo basi, wananchi wasipolipa kodi, serikali itashindwa kufanya hayo yote kwa ajili ya maendeleo ya raia wake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


***Husaidia katika malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa umma:*** Kodi husaidia kugharamia malipo ya mishahara na posho mbalimbali za wafanyakazi na wastaafu wa serikali.

***Makusanyo ya kodi husaidia kutoa na kuboresha huduma za jamii:*** Mfano, fedha zinazotokana na malipo ya kodi hutumika kutoa huduma za afya, elimu, maji, umeme na miundombinu.

## Zoezi la 5

1. Je, kodi ni nini?
2. Fafanua aina mbili za kodi nchini.
3. Unafikiri kwa nini serikali inatoza kodi kubwa kwenye bidhaa za vileo?
4. Eleza umuhimu wa wananchi kulipa kodi stahiki.
5. Unawashauri nini watu wenye tabia ya kukwepa kulipa kodi?

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu kuanzisha klabu ya “Elimu kwa mlipa Kodi” shuleni kwenu, kisha mjulisheni mwalimu wa somo juu ya mpango wenu. Andika majadiliano yenu katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 6

**A:** *Jibu maswali yafuatayo, kisha andika majibu yake katika daftari lako la mazoezi.*

1. Orodhesha haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Kuna faida gani ya kufahamu sheria za nchi?
3. Ni chombo gani nchini Tanzania huridhia mikataba inayotetea haki za binadamu?
4. Taja sehemu tano ambazo sheria hutumika katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku?



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 123 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

5. Viongozi kufuata sheria kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao huchochea jamii pia kufuata sheria.________
6. Tarehe 5, Februari ya kila mwaka ni siku ya kuadhimisha siku ya sheria nchini Tanzania.________
7. Kulipa kodi ni wajibu wa kila Mtanzania.________
8. Miradi ya maendeleo nchini haitegemei tozo ya kodi kutoka katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.________
9. Tabia ya kuhoji haiongezi uelewa wa kutenda jambo kwa uhakika.________

**C:** *Katika jedwali lifuatalo, oanisha kipengele cha haki za binadamu kutoka **Sehemu A** na kipengele cha wajibu wa raia kutoka **Sehemu B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A: Wajibu wa raia | Sehemu B: Haki za raia |
|---|---|
| 10. Kulipa kodi | (a) vyombo vya dola |
| 11. Kutii sheria | (b) kupata elimu |
| 12. Kukemea rushwa na ufisadi | (c) kupata fursa sawa |
| 13. Kuongeza ufanisi wa kazi na tija | (d) utawala bora |
| 14. Kushiriki katika kutoa uamuzi | (e) kuishi kwa amani |
| | (f) kupata huduma nzuri za jamii |
| | (g) vyombo vya uamuzi |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Dola | chombo chenye madaraka kamili ya kusimamia shughuli za utawala na siasa ndani ya nchi |
| Stoo | mahali panapotumika kuhifadhia vitu au bidhaa |
| Tume | kikosi cha watu walioteuliwa kwa ajili ya kufanya shughuli maalumu aghalabu ya uchunguzi wa jambo kwa niaba ya kiongozi fulani |
| Miktadha | mazingira yanayobainisha mahali jambo lilikofanyika |
| Jinai | shitaka la uhalifu linalomsababishia mtu mashitaka |
| Tija | manufaa ya jambo fulani |
| Manung'uniko | ni maneno au maandishi yatolewayo na mtu kuonesha kutoridhika na jambo fulani alilotendewa |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 124 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na moja

## Nidhamu binafsi

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza umuhimu wa kuwa na nidhamu katika kufikia malengo uliyojiwekea. Katika sura hii, utajifunza umuhimu wa kubainisha vipaumbele vyako na kuvizingatia, kutetea msimamo wako kwa hoja na nidhamu, kufanya uamuzi kwa wakati katika kutekeleza majukumu yako na kuthibitisha kauli ya kweli kwa mifano dhahiri katika maisha yako ya kila siku. Pia, utaweza kuonesha tabia ya kupiga vita unafiki katika maisha. Umahiri huu utakusaidia kujenga nidhamu binafsi katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku katika maisha husuan kubainisha vipaumbele katika kufanya maamuzi sahihi. Vilevile, utaweza kuonesha tabia za kupendeza katika jamii unayoishi.*

### Kubainisha vipaumbele vyako na kuvizingatia

Vipaumbele ni mambo yanayopaswa kukamilika kabla ya mengine kwa kupewa nafasi ya kwanza kutekelezwa kulingana na umuhimu wake. Unapokuwa na malengo ya kufikiwa katika maisha yako, unapaswa kuyapanga kulingana na umuhimu wake. Mwanafunzi unatakiwa kuwa na vipaumbele katika maisha ambavyo utavizingatia katika kuvitekeleza shuleni, nyumbani na katika jamii. Mfano, kipaumbele cha kwanza kwa mwanafunzi uwapo shuleni ni kusoma kwa bidii na kufaulu vizuri mitihani yako. Kwa kulitambua jambo hili, utatumia muda mwingi na akili yako kuhakikisha unafanikiwa kusoma kwa bidii na kufaulu mitihani yako.

### Kutambua upungufu ulionao katika kukabiliana na mambo mbalimbali

Kila mtu ana upungufu wake katika maisha. Unaweza kutambua upungufu huo kutokana na tabia ya utovu wa nidhamu, kutojiamini, kutokuhoji mambo, kukosa uvumilivu, kukosa uadilifu na kukosa uzalendo.

Unaweza kujijengea nidhamu binafsi kwa kuwa na tabia ya kujiamini. Kujiamini ni msukumo unaotoka ndani yako na nguvu ya pekee katika kufanikisha mambo. Ukijiamini utaongeza bidii na kutafuta misaada mbalimbali ili uweze





FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kufanya vizuri zaidi. Pia, unaweza kutumia njia mbalimbali kuwajengea wenzako uwezo wa kujiamini. Kwa mfano, kutokosoa wenzako kwa njia isiyo ya kistaarabu. Kukosoa kusiko na ustaarabu husababisha woga, chuki na kudhoofisha uwezo wa mtu wa kutenda jambo. Kamwe usitumie lugha ya kumkatisha tamaa mwenzako kwani tabia hiyo hushusha morali na kuvunja nguvu ya kutenda jambo. Hata wewe mwenyewe unatakiwa kuyakwepa mazingira ya kutendewa vitendo hivyo.

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Kajole na Mwajuma ni wanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Gezaulole. Shule hii ina uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa na madawati, hivyo wanafunzi wengi hukaa chini na wengine husomea chini ya miti. Vilevile, shule haina vyoo na vitabu vya kutosha hivyo wanafunzi wengi huchangia kusoma kitabu kimoja. Aidha, shule ina upungufu wa walimu wa baadhi ya masomo. Pamoja na upungufu huo, wanafunzi wengi ni waoga wa kuhoji mambo isipokuwa wachache wanaojitambua ndio hufanya hivyo. Siku moja, Ofisa Elimu wa Wilaya alipanga kufanya ziara katika Shule ya Msingi Gezaulole. Kajole na Mwajuma waliposikia mgeni huyo atatembelea shule yao, wakashirikiana na wanafunzi wenzao wakapanga namna ya kudai haki yao ya kupata elimu bora. Wakaandaa ngonjera na mabango yanayobainisha vipaumbele vyao vya kuzingatiwa ili waweze kupata elimu bora. Mgeni alipowasili, wakaomba wamuimbie ngonjera yao. Ngonjera hiyo ilieleza changamoto zinazoikabili shule yao kama vile kukosa madarasa, vitabu, vyoo na walimu kwa baadhi ya masomo. Ofisa Elimu alisikiliza ngonjera na kusoma mabango yao, kisha akaahidi kutatua changamoto za shule ya Gezaulole.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 1


1. Eleza maana ya kipaumbele.
2. Wanafunzi wa Shule ya Msingi Gezaulole walikuwa na changamoto gani?
3. Ni nini kilikuwa kipaumbele cha kwanza cha wanafunzi wa Gezaulole?
4. Wanafunzi wa Shule ya Msingi Gezaulole walitumia njia gani kupata suluhisho la changamoto zao?



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 126 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya namba 1



Shirikiana na wenzako katika kikundi, kuandaa ngonjera inayobainisha mambo yanayotakiwa kuboreshwa katika shule yenu ili kupata elimu bora. Andika ngonjera hiyo katika daftari lako la mazoezi.

### Kutetea msimamo wako kwa hoja

Msimamo ni hali ya mtu kutetea jambo bila kutetereka. Katika maisha ya kila siku watu huwa na mitazamo tofauti katika masuala mbalimbali. Kila mtu hutetea kile anachokiamini kwa kujenga hoja. Hali hii humfanya mtu kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia malengo aliyojiwekea katika maisha.

### Kuishi kwa kuzingatia malengo yako ya maisha

Kuwa na malengo husaidia kuwa na mwelekeo au dira katika maisha. Pia, huwezesha mtu kujua nini cha kufanya ili kupata maendeleo yake binafsi.

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Babu Chale:** Wajukuu wangu Mandomi na Makisi nimewaita hapa ili kila mmoja anieleze malengo yake katika maisha. Nitaanza kumsikiliza Mandomi, kisha Makisi utafuata.

**Mandomi:** Wakati ninasoma nilijiwekea lengo la kujiajiri kupitia kilimo cha biashara.

**Babu Chale:** Kilimo cha biashara maana yake nini?

**Mandomi:** Ahaah! Babu, ni kilimo cha kulima mazao mbalimbali na kuyauza. Pia, kununua mazao ya kilimo kutoka kwa wakulima na kuuza.

**Babu Chale:** Kwa hiyo, utakuwa unalima na kununua mazao ya wakulima na kuyasafirisha kwenda kuuza katika nchi za mbali?

**Mandomi:** Ndio babu.

**Babu Chale:** Je, utajishughulisha na kilimo cha mazao gani?

**Mandomi:** Nitajishughulisha na kilimo cha viazi mviringo pamoja na kufanya biashara ya nafaka yaani mahindi, maharage, kunde na mbaazi. Nitafanya shughuli hizi kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo. Nimeshafanya utafiti wa soko la mazao hayo na nimeshaandaa ekari mbili kwa ajili ya kilimo cha viazi. Pia,



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 127 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nimechukua mkopo katika kikundi cha kuweka na kukopa. Robo ya fedha hizi nitazitumia kwa kilimo cha viazi na robo tatu nitazitumia katika biashara ya nafaka. Baada ya miaka mitano natarajia kuwa na mtaji mkubwa wa kupanua shughuli hizi. Nitakuwa nimetengeneza faida kubwa itakayoniwezesha kuwa na nyumba ya kuishi na gari dogo la kusafirisha mizigo kwenda sokoni.

**Babu Chale:** Asante! Nawe Makisi nieleze malengo yako.

**Makisi:** Babu, mimi nimeweka malengo ya kufuga ng'ombe wa kisasa na biashara ya maziwa. Pia, nitakuwa nikisafirisha abiria kwa bodaboda pamoja na kujishughulisha na kilimo cha migomba.

**Babu Chale:** Unataka kurithi kazi ya babu yako?

**Makisi:** Ndio babu, ila mimi nitafanya ufugaji wa kisasa zaidi.

**Babu Chale:** Ebu nifafanulie vizuri nielewe mjukuu wangu.

**Makisi:** Awali nilipata semina ya jinsi ya kufuga kisasa kutoka kwa daktari wa mifugo wa kata yetu. Kisha nikachukua mkopo kwenye kikundi chetu cha kuweka na kukopa cha "CHAPUCHAPU SACCOS". Tayari nimeshatumia sehemu ya mkopo huo kununua mitamba minne yenye mbegu ambayo tayari ipo bandani. Sehemu ya mkopo iliyobaki nimenunua bodaboda ili inisaidie kubeba majani ya ng'ombe. Pia, bodaboda itanisaidia kukusanya na kusambaza bidhaa kwa wateja wangu. Vilevile, samadi inayozalishwa na ng'ombe itatumika kuzalisha umeme wa gesi kwa ajili ya kupikia na kutupatia mwanga. Hii itanisaidia kuacha kutegemea kuni zinazochangia kuharibu mazingira. Pia samadi itanisaidia katika kurutubisha ardhi kwa ajili ya kilimo cha migomba, mbogamboga na mahindi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na biashara.

**Babu Chale:** Wajukuu wangu! Mmenifurahisha kwelikweli! Hivyo, kila mmoja nitamwongezea mtaji baada ya kuuza fahali wangu mnadani. Mungu awawezeshe kufanikisha malengo yenu mliyojiwekea.

**Wote:** Tunashukuru sana babu.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

1. Ni mambo gani ya kujifunza kutokana na mazungumzo ya babu Chale na wajukuu wake?
2. Orodhesha malengo aliyojiwekea Mandomi.
3. Kuna umuhimu gani wa kujiwekea malengo katika maisha?
4. Unadhani kwa nini ni muhimu kuwa na msimamo katika malengo uliyojiwekea?
5. Kwa nini Babu Chale alifurahi?

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako nini kifanyike kabla ya kuchukua mkopo katika vikundi vya kuweka na kukopa ili kutimiza malengo yako. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.

### Kufanya maamuzi kwa wakati katika kutekeleza majukumu

Kuna faida nyingi zinazoweza kupatikana kwa kufanya maamuzi wakati wa kutekeleza majukumu yako ya kila siku. Unapaswa kujenga tabia ya kufanya maamuzi sahihi kwa wakati baada ya kushauriwa na watu mbalimbali. Unaweza kujifunza mambo mengi mazuri kutoka kwa watu wengine na ukatumia uzoefu wao kufanya maamuzi ya busara wakati wa kutekeleza majukumu yako.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Mzee Mtokambali alikuwa na mke na watoto wawili. Mtoto wa kwanza alikuwa na miaka tisa. Mtoto wa pili alikuwa na miaka sita. Maisha yao yalikuwa duni. Waliishi kwenye nyumba ya udongo iliyoezekwa kwa nyasi. Siku zote walipika kwa kutumia mkaa au kuni kama nishati ya kupikia. Kila walipotaka kupika chakula waliwasha mkaa au kuni kwa kutumia kiberiti na mafuta ya taa yaliyonunuliwa kwa kazi hiyo. Mafuta hayo yalitunzwa kwenye dumu na kuhifadhiwa jikoni.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Siku moja Mzee Mtokambali na mkewe walipanga kwenda shambani. Kabla ya kuondoka, mke wake aliwaandalia watoto chakula. Kisha akawaagiza walinde nyumba na akawakataza wasishike kiberiti wala kuwasha moto jikoni. Aliwaambia "Msicheze mbali na nyumbani, siku hizi kuna wezi sana". Lakini Mzee Mtokambali alimshauri mkewe asiwaamini sana watoto. Alimwambia watoto wa siku hizi hawazingatii maelekezo wanayopewa na wazazi au walezi wao. Akashauri ahamishe kiberiti na mafuta ya taa kutoka jikoni na avifungie chumbani. Mke wake hakutekeleza hilo. Akasema; "Nitavitoa nikirudi kutoka shambani". Walipoondoka tu, watoto wakaanza kucheza karibu na nyumba yao. Baadaye wakawafuata wenzao waliokuwa wanacheza mbali na kwao na kuacha nyumba bila ulinzi wowote. Baada ya kucheza kwa muda mrefu watoto walihisi njaa. Hivyo, wakarudi nyumbani kula chakula. Baada ya kula wakaingia chumbani kwao na kuanza kucheza tena.*

*Mara wakaanza kuchezea kiberiti kilichokuwa juu ya meza sebuleni. Mtoto mmoja akawasha kiberiti na kuweka njiti ya moto juu ya godoro. Mara godoro likashika moto na kuanza kuwaka. Mtoto mmoja akakimbia jikoni kuchukua maji ya kuzimia moto. Bila kujua akachukua dumu la mafuta ya taa na kumwagia juu ya godoro akidhani ni maji. Loo! moto mkubwa sana ukawaka na watoto wakaogopa sana na kukimbia nje. Moto ulisambaa haraka na nyumba yote iliungua na kuteketea kabisa.*

## Zoezi la 3

1. Taja mambo matatu ambayo mke wa Mzee Mtokambali aliwaagiza watoto wake.
2. Taja mambo mawili ya hatari ambayo watoto walifanya hata baada ya kukatazwa na wazazi wao.
3. Je, kosa gani alilofanya mke wa Mzee Mtokambali?
4. Orodhesha madhara yaliyotokana na watoto kutotii maagizo ya wazazi au walezi.
5. Unawashauri nini wazazi au walezi wasiopenda kusikiliza ushauri kutoka kwa watu wengine?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 3

Andika katika daftari lako la mazoezi kisa chochote kilichosababisha madhara katika familia yako baada ya kushindwa kuwasikiliza wazazi au walezi wako.

### Kutathmini maisha ya kila siku

Kutathmini ni hali ya kuangalia jambo kwa kina, kuzingatia faida na hasara zake ili kuweza kutoa uamuzi sahihi wenye busara na ufanisi. Hivyo, maisha bora ni matokeo ya tathmini ya kina ya namna ya kufanya vitendo vyako vya kila siku kwa ufanisi. Tathmini ya maisha yako inaweza kufanyika kwa kuangalia matokeo ya utendaji wako shuleni, kwa kuangalia kadi za maendeleo ya taaluma na mwenendo ili kubaini tabia yako kwa ujumla ikiwemo namna unavyoshirikiana na wenzako. Pia tathmini hii itabainisha ushiriki wako katika kazi za nje ya darasa. Kwa mfano, kushiriki kwenye michezo na shughuli za elimu ya kujitegemea shuleni na ushiriki wako katika shughuli za kuiletea familia yako maendeleo.

Ni muhimu sana kufanya tathmini ya maisha yako. Tathmini itasaidia katika ustawi wa maisha yako kwa kukurekebisha na kukujengea tabia ya kujitegemea. Tathmini itakujengea uwezo wa kudadisi kwani utaweza kuhoji na kutafuta majibu ya changamoto zinazojitokeza katika maisha yako na wanafamilia. Vilevile, itakujengea ujasiri na uwezo wa kujiamini katika kufanya mambo yanayoleta maendeleo. Halikadhalika, utapaswa kufanya tathmini ya maisha yako ili kujua ulikotoka, ulipo sasa na unaelekea wapi. Usikubali kuishi leo kama ulivyoishi jana.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 4


1. Eleza maana ya tathmini.
2. Utawezaje kufanya tathmini ya maisha yako ya kila siku?
3. Kuna umuhimu gani wa kufanya tathmini ya maisha yako ya kila siku?



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 131 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 4



Jadiliana na wenzako namna tathmini ya maisha yenu inavyofanyika hapo shuleni. Andika tathmini hiyo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuthibitisha kauli ya ukweli kwa mifano dhahiri katika maisha ya kila siku

Ukweli hujengwa kwa kutenda mambo au vitendo visivyotiliwa shaka katika jamii, kama vile kutenda mema, kutimiza ahadi, kuwa na uaminifu, na kufichua uovu.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Mtonyo na Mwemwele ni wanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Mapogoro. Siku moja wakiwa matembezini walikutana na Mzee Kibonye akiendesha bodaboda yake. Mara alipowapita alidondosha pochi yake. Mtonyo akaiokota pochi ile na kumuonesha Mwemwele. Mwemwele aliipekua na kukuta ina pesa nyingi sana ndani yake. Akamshauri Mtonyo wagawane lakini Mtonyo alikataa. Wakati Mtonyo na Mwemwele wakiendelea kubishana, Mzee Kibonye alirudi akitafuta pochi yake aliyoipoteza. Walipoona anawakaribia, Mwemwele akaificha pochi ile kwenye majani. Walipoulizwa kama wameiona na kuiokota pochi yoyote njiani walikopita, Mwemwele alikuwa wa kwanza kujibu kwamba hawajaiona na wala hawajaokota pochi yoyote. Mzee Kibonye alikata tamaa ya kuipata pochi yake akageuza bodaboda yake ili aendelee na safari. Mtonyo akasema tumeiokota pochi yako hii hapa. Mzee Kibonye aliikagua pochi yake na kukuta pesa zote. Alimshukuru sana Mtonyo kwa kuwa mtoto mwaminifu na mkweli. Akafungua pochi yake na kumpa zawadi ya shilingi elfu hamsini. Lakini Mtonyo alikataa kupokea ile pesa. Baada ya Mzee Kibonye kuondoka, Mwemwele alimlaumu sana Mtonyo kwa kufichua pochi ilipofichwa na kuzikataa zile pesa.*

FOR ONLINE USE ONLY




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 132 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Je, umejifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Unawashauri nini watoto wenye tabia kama ya Mwemwele?
3. Unadhani kwa nini Mzee Kibonye alitaka kumpa zawadi Mtonyo?
4. Eleza madhara ambayo watoto wanaweza kuyapata kutokana na tabia ya Mwemwele.
5. Kati ya wanafunzi wawili, ni nani aliyeonesha tabia ya uaminifu?

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu faida za kusema ukweli katika maisha ya kila siku shuleni na nyumbani. Andika faida hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Kutambua matendo ya mtu mnafiki

Katika jamii tunamoishi kuna watu wenye tabia mbalimbali, mojawapo ya tabia hizo ni unafiki. Unafiki ni kitendo cha mtu kufanya jambo kinyume na anavyosema. Mtu mnafiki huweza kutambulika kutokana na kauli zisizo za kweli anazotoa. Mnafiki hupenda kuchukua taarifa za mtu wa upande mmoja na kwenda kusema kwa mtu wa upande wa pili kwa lengo la kupata au kulinda masilahi yake binafsi. Mtu mwenye tabia hii hufahamu ukweli ulivyo lakini huupindisha ili kutimiza dhamira yake mbaya. Mtu mwenye tabia hii hupenda kutoa ahadi bila kuzitekeleza na wakati mwingine hukana kile alichokisema hadharani bila aibu. Vilevile, mtu mnafiki hana siri, husema mambo ya mtu mwingine bila kujali athari zinazoweza kujitokeza.

Tabia hii haikubaliki na huleta madhara mbalimbali katika jamii. Baadhi ya madhara hayo ni pamoja na ugomvi, migongano na kupotoshwa kwa ukweli. Ni vyema kuwashauri watu wenye tabia kama hii kuiepuka ili wawe na mwenendo mwema katika jamii.


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

1. Unafiki ni nini?
2. Katika jamii unayoishi, watu wanafiki wamesababisha madhara gani?
3. Utamtambuaje mtu mnafiki?
4. Unadhani ni jambo gani lifanyike ili kukabiliana na tabia ya unafiki?

## Kazi ya kufanya namba 6



Jadiliana na wenzako ni njia zipi zitumike kupambana na wanafunzi wanafiki shuleni. Andika njia hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuonesha tabia ya kupiga vita unafiki katika maisha

Mtu mnafiki hana sura yenye kuonesha kama ni mwongo katika maneno au vitendo vyake. Dalili za mtu mnafiki hutambulika kutokana na kauli zake na vitendo vya nafsi yake. Mnafiki hapaswi kuvumiliwa wala kujenga naye urafiki. Mnafiki si mtu wa kupanga naye mipango ya maendeleo. Mnafiki yupo tayari kuisaliti imani yake, familia yake, jamii yake na hata taifa lake kwa masilahi binafsi.

Jambo la msingi la kufanya pale tunapobaini kuwa kuna watu wanafiki mahali popote pale, ni kuwakemea waache tabia ya unafiki. Unafiki kwa hali zote unastahili kukemewa hadharani hususan pale panapokuwa na ushahidi kamili. Hivyo, tunaweza kuipinga tabia ya unafiki kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

(a) Kufafanua ukweli kuhusu unafiki. Yaani tuwaambie wanaofanya unafiki kuwa hatufurahishwi na unafiki wanaoufanya na waombe msamaha ikibidi;

(b) Tujilinde wenyewe na watu wanafiki kwa kupunguza ushirikiano kwa vitendo na kauli;

(c) Tutumie muda mwingi sana kuambatana na wanaotupenda na kupata faraja kwao, lengo ni kuharibu hisia mbaya zitakazokuwepo kwenye akili zetu juu ya wanaotuchukia na kutufanyia vitendo vya unafiki;



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 134 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Tusijione wanyonge kwa kuziachia nafasi za kimaisha wazitawale adui zetu kwa kusema; “Mimi sitafanya kazi na fulani, nitaacha kazi ili tusigombane naye zaidi.” Kamwe tusitoe nafasi za utawala badala yake tuoneshe wengine kwamba tunatekeleza majukumu yetu ya kimaisha vizuri ingawa tunachukiwa kwenye familia zetu, shuleni au kazini;


(e) Tuwashirikishe ndugu au rafiki wenye busara katika kila jambo linalotukwaza ili wasaidie namna ya kufanya. Tusichukue uamuzi wetu wenyewe bila ushauri hasa tunapokuwa na hasira. Tujipe muda wa kutafakari zaidi kila jambo la unafiki au chuki tunalofanyiwa kabla ya kuamua kufanya chochote; na

(f) Tusimwambie kila mtu changamoto zetu. Tusimame kwenye nguzo ya uvumilivu kabla ya kukata tamaa.

## Zoezi la 7

1. Taja tabia za mtu mnafiki.
2. Taja sababu tatu za watu kuwa na tabia ya unafiki.
3. Eleza namna utakavyokemea tabia za unafiki wa baadhi ya wanafunzi shuleni kwako.

## Kazi ya kufanya namba 7



Jadiliana na wenzako kuhusu athari za unafiki kwa maendeleo ya taaluma shuleni kwako. Andika athari hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Uelimishaji jamii kutojihusisha na unafiki

Katika jamii watu huwa na tabia mbalimbali, zikiwemo za kupendeza na zile za kuchukiza. Mazoea hujenga tabia ya kutenda mambo yenye kujenga au kubomoa maadili ya jamii. Unafiki ni mojawapo ya tabia zilizopo katika jamii. Tabia hii ni mbaya na husababisha kuwa na migogoro inayoweza kuepukika.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 135 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jamii inaweza kuepuka tabia hii kwa kutoa elimu ya kutojihusisha na unafiki kwa kutumia mbinu mbalimbali. Baadhi ya mbinu hizo ni kama zifuatazo:

**Kutumia vyombo vya habari:** Makala huweza kuandikwa katika magazeti kuelezea madhara ya unafiki katika jamii, kuonesha maigizo kuhusu vitendo vya unafiki kwenye runinga, mikanda ya video au michezo ya kuigiza jukwaani, kughani mashairi na kutamba ngonjera kwenye redio na runinga.

**Kwa kutumia mikutano ya hadhara:** Tabia ya unafiki inaweza kuwa mojawapo ya ajenda ya kudumu katika mikutano ya hadhara ili jamii ipate ujumbe wa kuepukana na tabia hii dhalala. Vivyo hivyo semina, mahubiri au makongamano ya dini huweza pia kusaidia kufikisha ujumbe kwa jamii juu ya madhara ya unafiki katika maisha yetu ya kila siku. Baadhi ya madhara hayo ni migogoro, kukosa ushirikiano, chuki na uhasama.

**Mijadala katika mitandao ya kijamii:** Elimu katika jamii kuhusu kutojihusisha na tabia ya unafiki inaweza kutolewa kupitia mijadala ya kijamii kwa kutoa maoni yao ili kuirekebisha jamii. Kwa mfano, kugonganisha watu kwa habari za uongo. Kutumia kampuni za simu kutuma ujumbe mfupi kwenye simu za wateja wao kuhusu kujiepusha na unafiki na madhara yake.

**Masimulizi ya hadithi:** Hadithi zinaweza kuelezea visa vya watu wenye tabia ya unafiki katika jamii na athari walizopata kutokana na kujihusisha na tabia hii.

**Kuwatangaza wanafiki hadharani:** Jamii inaweza kujiwekea kanuni ya kubainisha wanafiki na kuwatangaza hadharani.

Mbinu hizi zitasaidia watu wenye tabia ya unafiki katika jamii kutambua madhara ya tabia hiyo na kujiepusha kujihusisha nayo.


## Zoezi la 8

1. Taja mbinu zitakazotumika kuelimisha jamii kutojihusisha na unafiki.
2. Kuna faida gani ya jamii kuelimishwa kuhusu ubaya wa tabia ya unafiki?
3. Je, tabia ya unafiki imeleta athari gani kwenye darasa lako?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 8



Jadiliana na mwanafunzi mwenzako njia utazotumia kuelimisha wenzako kutojihusisha na tabia ya unafiki shuleni kwako. Andika njia hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Hoja juu ya mambo yanayobainika na kuthibitika kuwa kweli

Mtu hufikiri jambo ndipo hulitenda ili kupata ufumbuzi wa changamoto inayomkabili katika mazingira yake. Kufikiri huku humfanya mtu kujenga hoja na namna ya kuitetea ili afanikishe alichokusudia. Ili kujenga hoja mtu hupenda kudadisi au kuuliza maswali mbalimbali kwa lengo la kufahamu na kuelewa mambo katika mazingira yanayomzunguka.

*Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mzee Masanja anaishi katika Kijiji cha Likwidi na ana familia yenye watoto watatu ambao ni Adamu, Mwanaheri na Samata. Mwanaheri na Samata ni watoto mapacha. Watoto hawa walikuwa wanasoma katika Shule ya Msingi Likwidi. Adamu alikuwa Darasa la Sita wakati Mwanaheri na Samata walikuwa darasa la nne. Masanja na familia yake siku zote hufanya kazi kwa bidii. Hali hii imemwezesha kumiliki shamba kubwa la mahindi, migomba, ng'ombe na mbuzi. Mzee huyu ana utamaduni wa kushirikisha familia yake katika mipango ya maendeleo kila wakati. Hivyo kuifanya familia yake ifahamu na kushiriki katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali na kufanikisha malengo hayo. Yafuatayo ni majadiliano ya kikao cha familia ya Mzee Masanja.

**Masanja:** Wanangu msimu wa kilimo umewadia, mnapenda tulime nini?

**Mwanaheri:** Mahindi pamoja na kuendelea kutunza shamba la migomba.

**Adamu:** Kabla ya kujibu swali, baba naomba utuambie msimu uliopita tulipata kiasi gani cha mazao na tulipata faida au hasara?

**Masanja:** Tulipata faida kidogo iliyotusaidia kununua mbuzi watatu wa maziwa.

**Adamu:** Baba, kwa nini hukupanda mbegu za kisasa katika shamba letu la mahindi msimu uliopita ili kupata mazao mengi?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwanaheri:** Shuleni tunahimizwa tuoteshe kwa mistari na kutia mbegu mbili katika shimo. Mbona shambani hatutumii mistari na tunaweka mbegu tatu mpaka nne kwenye shimo?

**Masanja:** Wanangu nilikosa hela za kutosha kununua mbegu za kisasa pia nilidhani mbegu nyingi zingetoa mazao mengi zaidi. Msimu huu, tutafuata kanuni zote za kilimo bora na nimemwalika Bwana shamba siku ya kupanda. Pia, nimepata mkopo wa kilimo kutoka kwenye kikundi chetu cha maendeleo hivyo pembejeo zote za kilimo zitakuwepo.

**Adamu:** Mmenunua mbuzi watatu wa maziwa. Mnaonaje wale mbuzi mkatugawia sisi tukawalisha?

**Mama:** Mmeuliza maswali mazuri wanangu, tangu tumeanza mazungumzo, kila mmoja atapata mbuzi na tutashirikiana kuwalisha.

**Samata:** Mama, shuleni tumeambiwa tunywe maziwa ya kutosha ili tuwe na afya bora. Kwa nini sisi hatuna ng'ombe wa kisasa kama akina Daudi?

**Mama:** Wanangu, tukivuna mazao ya msimu huu tutawauza ng'ombe wa kienyeji, tutabakiza mafahali wanne kwa ajili ya kuwafanya wawe maksai wa kilimo, na kununua ng'ombe wanne wa kisasa ili kupata maziwa ya kutosha.

**Masanja:** Haya tuliyoyajadili tutayatekeleza kwa faida yetu sote wanangu.

**Mama:** Sasa wanangu nendeni mkafanye usafi wa mazingira kama nilivyowaeleza jana.


## Zoezi la 9

1. Taja hoja zilizojadiliwa katika kikao cha familia ya Masanja.
2. Hoja ya Adamu ilithibitisha ukweli upi?
3. Swali la Samata limeleta faida gani kwa familia?
4. Kwenye familia yenu uliwasilisha hoja gani na kuitetea?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 9



Jadiliana na wenzako kuhusu umuhimu wa kujenga hoja na kuitetea ili kuthibitisha ukweli wa jambo. Andika umuhimu huo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 10

*Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

1. Msimamo ni ile hali ya mtu kutetea jambo kwa kutetereka.________
2. Vitendo visivyotiliwa shaka katika jamii hujenga ukweli.________
3. Wanafiki wanahitajika ili kupeleka ujumbe haraka kwa jamii.______
4. Hoja hujengwa baada ya kufanya udadisi wa jambo.________
5. Dawa pekee ya unafiki ni kukemea hadharani baada ya kupata ushahidi kamili.________
6. Kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine katika jamii ni kosa.________

### Msamiati

| | |
|---|---|
| Bodaboda | pikipiki inayotumika kusafirisha watu au mizigo kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa malipo |
| Dhalala | mwenendo au tabia isiyofaa |
| Maksai | ng'ombe dume aliyehasiwa na anayetumiwa katika shughuli za kilimo au kukokota mkokoteni |
| Pembejeo | vitu vinavyohitajika katika shughuli za kilimo |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 139 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Kuvumilia katika maisha

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza vitendo vya uvumilivu katika kukuwezesha kukabiliana na changamoto za maisha ya kila siku na umuhimu wa kuwa mvumilivu katika maisha. Katika sura hii, utajifunza kutenda vitendo vya kuhimili changamoto zinazokukabili, kuhamasisha wengine kukabiliana na changamoto za maisha kwa kutumia uzoefu wako, kuishi kwa matumaini na kukiri ushindi dhidi ya mabadiliko. Umahiri huu utakujengea tabia ya kuwa mvumilivu katika maisha kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali. Pia, utakujengea tabia ya kuwasaidia watu wengine katika jamii unamoishi katika kuhimili changamoto wanazokabiliana nazo.*

### Kutenda vitendo vya kuhimili changamoto

Changamoto ni jambo linalomkabili mtu na linahitaji ufumbuzi. Changamoto ni sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Hivyo, unapaswa kuwa mstahimilivu unapopata changamoto. Pia, unatakiwa kuikubali na kutafuta namna ya kukabiliana nayo. Vilevile, hupaswi kujidhuru kwa sababu ya changamoto. Aidha, ni vyema ukaomba ushauri kwa watu au ukatumia uzoefu wa watu wengine ili uweze kutekeleza mpango mkakati wa kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika maisha.

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mwambene ni mwanafunzi wa Darasa la Sita katika Shule ya Msingi Mbuyuni. Alifanya mitihani ya muhula wa kwanza na kuwa mwanafunzi wa kumi na tano darasani kwao. Mwambene hakukata tamaa, aliongeza bidii katika masomo yake ili aweze kufaulu na kushika nafasi ya kwanza darasani. Alijiwekea ratiba ya kusoma nyumbani na kuifuata. Alizingatia sheria na taratibu za shule na kufanya kwa wakati kazi zake zote alizopewa na walimu. Mara nyingi Mwambene alikosa vitabu vya kujisomea. Hivyo, aliazima vitabu kwa walimu au wanafunzi wenzake. Kila Jumamosi, Mwambene alitembea umbali wa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 140 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kilometa tano kwenda shule za jirani kufanya mitihani ya kujipima. Hatimaye, alifanya vizuri sana katika masomo yake shuleni kwake na kutimiza lengo lake la kushika nafasi ya kwanza.

## Zoezi la 1

1. Taja vikwazo alivyokutana navyo Mwambene.
2. Mwambene alitaka kutimiza lengo gani?
3. Je, tabia ya Mwambene inafaa kuigwa? Kwa nini?
4. Mwambene alifanya vitendo gani kuhimili changamoto zilizomkabili?

## Kazi ya kufanya namba 1

Andika katika daftari lako la mazoezi vikwazo unavyovipata wakati wa kujifunza somo la Uraia na Maadili, kisha, eleza jinsi utakavyokabiliana na vikwazo hivyo.

### Kuhamasisha wengine kukabiliana na changamoto za maisha

Unapaswa kutumia uzoefu wako kuhamasisha watu wengine kukabiliana na changamoto za maisha. Wakati wa uhamasishaji, unapaswa pia kuwa mvumilivu kwani binadamu tunatofautiana kwa umri, maumbile na mawazo. Wapo wenye umri mdogo, mkubwa au sawa na wako, wenye mawazo chanya na wenye mawazo hasi, hivyo unapaswa pia kuwavumilia na kuwakubali watu wengine wenye mawazo tofauti na yako.

### Changamoto zinazowakabili watu katika jamii

Zipo changamoto mbalimbali zinazowakabili watu katika jamii. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na ulemavu, kukosa makazi, ukosefu wa ajira, kukosa huduma za kijamii, kutokuwa na mtaji wa kujiajiri, maradhi na umaskini. Tunapokuwa na changamoto hizi tusikate tamaa, tuwe jasiri na tujaribu kufikiri na kubuni mbinu za kukabiliana nazo. Vilevile, tuwasaidie wengine katika jamii wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali. Mfano, watoto wanaoishi katika changamoto ya ulemavu wasaidiwe kuyakabili na kuyaelewa mazingira wanayoishi. Vilevile, watoto hawa wasaidiwe kuweza kupata elimu. Iwapo

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 141 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

familia ina mtoto mwenye ulemavu wa aina yoyote ile mtoto huyo asaidiwe kuweza kwenda na kurudi shuleni. Watoto wenye ulemavu wafundishwe kujiamini, kujipenda, kujithamini na kushiriki katika shughuli ndogondogo za familia. Tunapopata changamoto katika maisha tuziangalie kama mlango wa fursa. Fursa ni mazingira yanayotengeneza uwezekano wa jambo kufanyika. Hivyo tufikirie na kuzibadilisha changamoto zinazotuzunguka kuwa fursa.

## Zoezi la 2

1. Wewe unafanya matendo yapi kuwahudumia wanafamilia?
2. Utamshauri nini mwenzako asiyependa kuhudumia wanafamilia wenye uhitaji?
3. Unapokuwa na changamoto unapaswa kufanya nini?

## Kazi ya kufanya namba 2

Orodhesha changamoto zinazoikabili jamii yako, kisha pendekeza namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

### Kuwashauri wengine kutumia njia sahihi kukabili matatizo mbalimbali

Kuna matukio mengi yanayojitokeza katika jamii. Matukio hayo yanaweza kuwa ya kufurahisha au kuhuzunisha. Baadhi ya matukio hayo huhitaji ushauri makini ili kukabiliana nayo. Ushauri waweza kutolewa na mtu yeyote unayeamini anaweza kukusaidia.

Ushauri hutolewa kwa kufuata njia sahihi za kutatua matatizo yaliyojitokeza. Njia ya kwanza ni utayari wa kutatua tatizo ambapo mwenye tatizo huwa tayari kueleza tatizo linalomkabili au walio karibu na mwenye tatizo kuwa tayari kupata ushauri kutoka kwa watu wengine. Pili, ni kubaini tatizo ambapo tatizo huainishwa na kujulikana. Tatu, ni kujua chanzo cha tatizo ambapo chimbuko la tatizo husika hutafutwa. Nne, ni kuwa na mbinu za kukabili tatizo ambapo utaratibu huandaliwa ili kukabili tatizo husika. Tano, ni kutumia mbinu hizo na kukabili tatizo kwa kuweka utaratibu wa kutatua tatizo husika.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Natani ni mtoto wa Mzee Kivuyo anayeishi katika Kijiji cha Magugu. Natani alikuwa kijana mstaarabu sana. Pia, alikuwa fundi maarufu wa kutengeneza bodaboda katika kijiji hicho. Alifanya kazi yake vizuri na kwa uaminifu wa hali ya juu. Kazi hii ilimpatia fedha nyingi za kuendesha maisha yake. Kipato kikubwa alichokipata kilimbadilisha tabia na kumfanya ajihusishe na unywaji wa pombe wa kupindukia na kugombana na wateja pasipo sababu. Tabia hii iliwasikitisha sana wazazi kwa sababu vitendo alivyofanya kijana wao havikukubalika katika jamii. Halikadhalika, wateja wake walipungua mno na kuhamia sehemu nyingine kupata huduma ya matengenezo ya bodaboda zao.*

## Zoezi la 3

1. Natani anakabiliwa na tatizo gani?
2. Chanzo cha tatizo la Natani ni nini?
3. Mbinu gani itumike kumsadia Natani?

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wenzako umuhimu wa kutumia njia sahihi kukabili tatizo. Andika umuhimu huo katika daftari lako la mazoezi.

### Kuonesha tabia za kuishi kwa matumaini na kukiri ushindi dhidi ya mabadiliko

Katika maisha ya kila siku, tunapaswa kutenda vitendo mbalimbali vinavyoonesha tabia ya kukiri ushindi dhidi ya mabadiliko. Kwa mfano, mwanafunzi anawasimulia wenzake jinsi alivyokuwa anashindwa somo la Uraia na Maadili na sasa anafaulu vizuri baada ya kuanza kuuliza na kujibu maswali darasani.

### Kuonesha vitendo vya kukabiliana na hali ngumu katika maisha

Hali ngumu katika maisha humfanya mtu kushindwa kuvumilia na hivyo kukata tamaa na kuathiri mambo anayoyatenda. Hujikuta anapata hofu, kutojiamini, na kujiona mnyonge. Hali hii isipodhibitiwa mapema, huweza kumsababishia mtu maradhi na hata kifo. Tunapaswa kukabiliana na hali ngumu ya maisha inapotokea.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 143 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

**Sudi:** Baba, mbona siku hizi mama hapiki nyama, pilau na hata hutununulii nguo mpya za sikukuu. Pia, hutupeleki ufukweni kuogelea na wenzetu?

**Baba:** Mwanangu Sudi, siku hizi maisha yamebadilika. Hali ya uchumi wa familia nyingi imeyumba sana. Si ulisikia zoezi la kupunguza wafanyakazi wasiokuwa na vyeti halali?

**Sudi:** Ndiyo baba!

**Baba:** Hali hii ngumu ya maisha ni baada ya mimi kufukuzwa kazi, kwa vile sina cheti halali cha kidato cha nne.

**Sudi:** Nimekuelewa baba, sasa itakuwaje? Tutaendelea na hali hii mpaka lini?

**Baba:** Hata mimi nachanganyikiwa, labda tushauriane cha kufanya.

**Sudi:** Mimi ninaona ni bora tuanzishe bustani ya mbogamboga. Tukiuza mazao yatakayopatikana kwenye bustani yetu, tutapata pesa ya kununua nguo, chakula na hata kugharamia matibabu yetu.

**Baba:** Wawoo! Wazo zuri sana mwanangu, ngoja kesho tuanze kulima hiyo bustani.

**Sudi:** Sawa baba.

Baada ya Sudi kushirikiana na baba yake kulima bustani ya mbogamboga waliuza na kupata pesa nyingi zilizowawezesha kukidhi mahitaji yao muhimu.

## Zoezi la 4

1. Vitu gani vilidhihirisha kuwa familia ya Sudi inakabiliwa na hali ngumu ya maisha?
2. Ungekuwa Sudi, ungemshauri nini baba yako ili kuongeza kipato cha familia yenu?
3. Taja njia mbili mbadala unazoweza kutumia kutatua changamoto ya kipato cha familia yenu.


FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 144 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 4



Shirikiana na wenzako kubaini mabadiliko yaliyotokea shuleni kwenu toka ulipojiunga na shule hiyo. Eleza namna mlivyoweza kukabiliana na mabadiliko hayo. Andika maelezo hayo katika daftari lako la mazoezi.

### Matumizi ya njia mbadala kukabiliana na changamoto za maisha

Maisha ni safari ndefu yenye milima na mabonde ya kupanda na kushuka. Maisha haya yana changamoto nyingi zenye kuhitaji njia mbadala za kuzikabili. Changamoto haziepukiki katika maisha, hivyo ili maisha yaendelee tunapaswa kutumia njia mbadala kuzikabili na kuzitafutia suluhu.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali yanayofuata.

*Maroroi ni mzee mwenye juhudi katika kazi za ufugaji na kilimo. Anajishughulisha na ufugaji wa mbuzi, kondoo na ng'ombe. Ana ng'ombe wa maziwa na jozi nne za maksai kwa ajili ya kulimia mashamba yake na kubebea mizigo kupeleka sokoni. Kwa miaka mingi, alifanikiwa sana katika shughuli za kilimo na ufugaji na kuwa na maendeleo makubwa. Watu walimsifu kwa juhudi za kufanya kazi kwa kujituma na tabia yake ya kusaidia watu wengine katika kijiji chake.*

*Miaka ya karibuni maisha yake yalibadilika kutokana na kuwepo kwa baa la ukame wa muda mrefu. Hali hii ilisababisha mifugo yake kuathirika kwa njaa na mazao kukauka kwa kukosa mvua na kusababisha Mzee Maroroi ayumbe kiuchumi.*

*Baada ya hali hiyo kumpata Mzee Maroroi alikaa kitako na kuwaza kwa makini njia ya kukabiliana na hali hii ngumu. Baadaye alipata njia mbadala ya kukabiliana na hali hiyo. Hivyo, akaamua kuuza ng'ombe wote na kubaki na fahali, mbuzi na kondoo. Pia, alianzisha miradi ya ufugaji wa nyuki wakubwa na wadogo pamoja na ufugaji wa kuku wa kienyeji.*

*Miradi hii mipya ilimpatia fedha kutokana na soko kubwa la asali, kuku na mayai alilolipata katika mji wa Puma ambako kuna soko la bidhaa mbalimbali. Mji huu unapitiwa na barabara kuu na reli ambapo abiria hununua kuku, mayai na asali. Maisha ya mzee huyu yalibadilika na anaishi kwa raha na amani na familia yake baada ya kukabiliana na changamoto.*

FOR ONLINE USE ONLY




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 145 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

1. Eleza maana ya changamoto kutokana na kisa ulichosoma.
2. Mzee Maroroi alikuwa mtu wa namna gani?
3. Mzee Maroroi alipata changamoto gani?
4. Mzee Maroroi alikabiliana vipi na changamoto?
5. Taja mambo matatu uliyojifunza kutokana na kisa hiki.

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wenzako jinsi ya kukabiliana na wanafunzi wanaoharibu bustani za maua na kuvunja madawati kwa makusudi shuleni. Andika majadiliano hayo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 6

*Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

1. Uvumilivu haumfanyi mtu kustahimili changamoto za maisha.________
2. Unapopata changamoto ndio mwisho wa kufanikiwa katika maisha.____
3. Mtoto hawezi kumshauri mzazi au mlezi wake kuhusu kubuni njia mbadala za kuongeza kipato cha familia yake.________
4. Unaweza kugeuza changamoto ikawa fursa ya kuboresha kipato chako na maisha yako.________
5. Kushindwa mtihani ni changamoto kwa mwanafunzi.________
6. Ushauri hutumiwa na watu kumaliza matatizo yanayowakabili.________
7. Ili kumudu maisha ni vyema kuzikimbia changamoto.________
8. Ili kulitatua tatizo unapaswa kulibaini kwanza.________
9. Kuwa na miradi midogomidogo husaidia kukabiliana na changamoto za maisha. ________
10. Maisha ni safari ndefu yenye milima na mabonde ya kupanda na kushuka.____

### Msamiati

Baa — balaa linalomfika mtu, maafa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 146 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Kujifunza mambo kiyakinifu

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kuchanganua mambo kiyakinifu, kuhoji mambo, na kujifunza kutokana na uzoefu wa watu wengine. Katika sura hii, utajifunza kudadisi kwa kutumia mazingira, kutathmini uwezo wako katika kujifunza na umuhimu wa ushirikiano na watu wengine katika kujifunza. Umahiri huu utakuwezesha kuwa mdadisi katika mazingira unamoishi na kufanya vitu kwa kuthibitisha nadharia kwa kuhusianisha dhana na maisha yako ya kila siku kwa kujenga hoja.*

### Kudadisi kwa kutumia mazingira

Mazingira yanaweza kutumika kudadisi jambo ambalo mtu anataka kujifunza na kuelewa kwa kina. Kwa mfano, tunaweza kutumia kazi za sanaa zinazoonesha maisha ya binadamu toka zama zilizopita, zinazopatikana katika mazingira yetu ili kukuza mtazamo wa kujali kile walichofanya watu wa zama za kale. Pia, tunaweza kutumia baadhi ya vifaa vilivyotengenezwa na kutumiwa na watu wa kale.

### Kujaribu nadharia mbalimbali kwa vitendo ili kuthibitisha ukweli wake

Nadharia ni mfumo au wazo linalotumika kuthibitisha ukweli wa jambo fulani au ni mfumo wa mawazo ya kifalsafa yanayoeleza kuhusu uhalisia fulani katika maisha ya mwanadamu na mazingira yake.

*Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Majula ni mwalimu wa Somo la Maarifa ya Jamii katika Shule ya Msingi Kwembe. Muda wa likizo amekuwa akiutumia mjini Bagamoyo katika pwani ya Bahari ya Hindi. Awapo pwani, wakati wa mawimbi amezoea kuona mchanga ukisombwa kwenye ufukwe, hivyo, kuacha wazi sehemu zilizokuwa zimefunikwa na mchanga na udongo kwa miaka mingi. Akiwa anaendelea kuzunguka ufukweni, mara anaviona vipande vya vyungu vya zamani na kushangazwa jinsi vilivyotengenezwa na kupambwa. Pia, anaviona vipande

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vya mawe vilivyochongwa ambavyo vilitumika zama za kale kwa ajili ya kukatia, kugongea na kusagia vitu. Vilevile, kuna mabaki ya mifupa ya wanyama waliowindwa zama za kale. Mara nyingine, mwalimu Majula hupeleka wanafunzi katika sehemu hiyo. Wanafunzi wanapogusa vitu hivyo na kutafakari watu wa miaka iliyopita, muda na jitihada walizotumia kutengeneza zana au vitu hivyo, wanapata picha halisi ya hatua ya maendeleo ya binadamu wa kale hadi sasa.

## Zoezi la 1

1. Taja vitu vitatu alivyoviona mwalimu Majula ufukweni mjini Bagamoyo.
2. Unafikiri kwa nini mwalimu Majula alikuwa anawapeleka wanafunzi wake safari mafunzo?
3. Je, unatoa ushauri gani kwa walimu wa masomo mengine ambao wanafundisha nadharia tu?

## Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wenzako kuhusu faida ya kujifunza kwa vitendo shuleni. Andika faida hizo katika daftari lako la mazoezi.

### Kutathmini uwezo wako katika kujifunza

Maisha ya watu yanahitaji kujifunza kila siku. Kujifunza husaidia watu kumudu mazingira yao kwa urahisi. Vitendo vya kujifunza hutathmini dhana mbalimbali alizonazo mtu. Dhana hizo humsaidia mtu kuthibitisha nadharia kwa kuzihusianisha na maisha ya kila siku.

### Kuthibitisha nadharia kwa kuhusianisha dhana na maisha ya kila siku

Nadharia mbalimbali huweza kuthibitishwa baada ya mtu kuweka dhana alizonazo katika vitendo. Mtu anaweza kuwa amefundishwa au amehawilisha maarifa aliyonayo kwa kutenda jambo wakati akitekeleza shughuli zake. Kwa kufanya hivyo, mtu huthibitisha uhalisia wa nadharia husika.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Soma habari na mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.*

Mama Twilumba ni mama mwenye juhudi katika shughuli zake za kujikimu kimaisha. Ni mlezi mzuri wa watoto na watoto wake ni wenye nidhamu ya hali ya juu na mfano wa kuigwa na kila mtu. Watoto hawa husalimia wakubwa kwa wadogo kwa heshima, huwapokea mizigo wale waliowazidi umri. Pia, hushiriki katika kazi za mikono shuleni kama vile kufagia na kumwagilia bustani za maua. Warudipo nyumbani hulisha kuku na mbuzi. Mama yao Twilumba alikuwa anafanya shughuli za upambaji kumbi za sherehe. Shughuli hizi alizifanya kwa muda mrefu na zimemsaidia kumudu kuendesha maisha yake na ya familia yake. Faida ya fedha aliyoipata katika shughuli zake aliigawa mara mbili. Sehemu moja aliitumia kwa chakula na kusomeshea watoto wake na sehemu iliyobaki alijiwekea akiba. Shughuli hizi zimemwezesha pia kufungua duka kubwa la vipodozi.

Siku za Jumamosi watoto wake humtembelea dukani na kumsaidia shughuli ndogondogo anapokuwa anawahudumia wateja. Mwanaye Twilumba alimchunguza mama yake muda wote pale dukani na hakumwona akitoa risiti kwa wateja wake. Mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:

**Twilumba:** Mama, mbona hutoi risiti kila unapouza bidhaa kwa wateja?

**Mama Twilumba:** Mwanangu, sioni faida ya kutoa risiti kwani inanipotezea muda tu na mapato.

**Twilumba:** Mama tumefundishwa shuleni faida za kutoa risiti. Kwanza husaidia kujua faida na hasara katika biashara yako, kuweka kumbukumbu ya manunuzi na mapato ya biashara. Vilevile, husaidia serikali kupata mapato yatakayoiwezesha kutoa huduma za jamii kama vile, kujenga shule, vituo vya afya, miundombinu ya maji, barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari.

**Mama Twilumba:** Nimekuelewa mwanangu nitafanya hivyo kuanzia leo na itanisaidia sana katika biashara yangu.

**Twilumba:** Mwalimu wetu hakuishia katika kutufundisha kuhusu faida za kutoa risiti ukiuza bidhaa, pia alielezea kuhusu kupambana na malaria. Alisema ili kupambana na malaria tunapaswa kufukia mashimo yanayotuamisha maji,



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 149 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kufyeka nyasi ndefu kwenye mazingira ya kuishi na kutumia chandarua.

**Mama Twilumba:** Kumbe ndio sababu nawaona wanangu mnazingatia kutumia chandarua na kufyeka nyasi ndefu! Kweli sasa mmeelimika na mmethibitisha nadharia kwa vitendo, yaani yale mliyojifunza shuleni mnaonesha kwa vitendo kule nyumbani.

**Twilumba:** Mama hata yale uliyotufundisha nyumbani tunayafanya kwa vitendo shuleni. Kwa mfano, tukiwa shuleni walimu na wanafunzi wanasema tuna heshima na tunajituma katika kazi mbalimbali. Haya yote ni yale uliyotufundisha nyumbani tunayatenda kwa vitendo shuleni.

## Zoezi la 2

1. Ni vitendo gani watoto wa Mama Twilumba wanavionesha baada ya kufundishwa kinadharia na mama yao?
2. Nadharia ya matumizi ya risiti aliyopata Twilumba shuleni imemsaidiaje mama yake kuithibitisha kwa vitendo katika biashara yake?
3. Taja mambo matatu uliyojifunza shuleni kinadharia yalivyokusaidia nyumbani katika kuendeleza maisha yako ya kila siku.

## Kazi ya kufanya namba 2

Eleza ni kwa namna gani elimu ya afya shuleni ilivyokusaidia kupambana na homa ya malaria kwa vitendo. Andika maelezo yako katika daftari lako la mazoezi.

### Umuhimu wa kushirikiana na watu wengine katika kujifunza

Zipo faida mbalimbali unazoweza kuzipata kwa kushirikiana na wanafunzi wengine katika kujifunza. Baadhi ya faida hizo ni:

(a) Kutumia uzoefu na uelewa wa watu wengine kwa vile vipaji na uwezo hutofautiana. Kusoma kwa kushirikiana huwawezesha washiriki kufaidi uwezo na vipaji vya wanafunzi wengine;



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kujenga kumbukumbu ya muda mrefu, kukuza uwezo wa kujieleza na kujiamini;
(c) Kupata nafasi ya kutoa uzoefu na kukuza kipaji chako;
(d) Kujenga tabia ya uvumilivu na usikivu wa mawazo ya wengine; na
(e) Kujenga tabia ya umoja na ushirikishaji.

Ili kuongeza ufanisi katika kujifunza unapaswa kuelewa umuhimu wa unachojifunza katika maisha yako ya kila siku. Uwe na tabia ya kujisomea kwa kufuata na kuheshimu ratiba uliyojipangia. Vilevile, uwe na tabia ya kushirikiana na wenzako katika kusoma na kufanya mazoezi. Wanafunzi wanashauriwa kuanzisha vikundi vya kujisomea ambavyo vitashirikisha wanafunzi wenye uwezo wa juu kitaaluma na wale wenye uwezo wa kawaida. Vikundi hivi vinaweza kuwa na utaratibu wa kukutana shuleni baada ya vipindi au katika siku za mapumziko. Lengo la vikundi hivi ni kujisomea, kufanya kazi wanazopewa na walimu kwa pamoja na kufanya majadiliano ya mahiri mbalimbali kwa pamoja. Majadiliano ya kikundi ni njia madhubuti katika kuongeza muda wa wanafunzi kuwa makini. Majadiliano hutoa fursa ya wanafunzi kusikia sauti na maoni ya wanafunzi wenzao.

Majadiliano ya kikundi huhamasisha wanafunzi kushirikiana. Katika vikundi hivi kila mwanakikundi ashiriki kuwaelekeza wenzake mambo anayoyafahamu. Iwapo kila mwanafunzi atashiriki kikamilifu katika kikundi chake na kutekeleza majukumu yake ipasavyo basi maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wote katika darasa husika yataimarika.

## Zoezi la 3

1. Kuna faida gani za kujifunza katika vikundi?
2. Unapaswa kuzingatia mambo gani ili kuongeza ufanisi katika kujifunza?
3. Eleza faida tatu za kujifunza kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako.


FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 151 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 3


Jadiliana na wenzako kuhusu athari za kutoshirikiana na wanafunzi wenzako katika kujifunza shuleni. Andika athari hizo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 4

**A:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

1. Tunaweza kujifunza mambo katika mazingira yetu kwa njia zifuatazo isipokuwa:
   (a) kusoma magazeti na vitabu
   (b) kusikiliza redio na kuangalia runinga
   (c) kupitia ndoto zetu
   (d) mahubiri kanisani na msikitini

2. Kwa nini tunajaribu nadharia mbalimbali kwa vitendo?
   (a) kuthibitisha ukweli wake
   (b) kuzitofautisha
   (c) kuzifanya ziweze kukubalika kimataifa
   (d) kubaini zisizofaa

3. Tunawezaje kuthibitisha mambo tuliyojifunza?
   (a) iwapo tutafaulu katika mitihani
   (b) iwapo tutaeleza wengine
   (c) iwapo tutayatumia katika maisha yetu
   (d) iwapo tutayakariri

4. Tunapojifunza na wenzetu tunapata faida zifuatazo isipokuwa:
   (a) kujenga kumbukumbu ya muda mrefu
   (b) kujenga tabia ya uvumilivu
   (c) kupendelea wengine
   (d) kujenga urafiki

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Unawezaje kuongeza ufanisi katika kujifunza?
   (a) kubeba vitabu vingi
   (b) kusoma kwa vikundi
   (c) kucheza na wenzako
   (d) kufanya mitihani

**B:** *Katika jedwali lifuatalo, oanisha kipengele kutoka* ***Sehemu A*** *na kipengele kutoka* ***Sehemu B,*** *kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 6. Kushiriki katika kazi za mikono | (a) kuwaburudisha wazee |
| 7. Kusikiliza hadithi | (b) kuelewa maisha ya wahenga |
| 8. Kuuliza maswali | (c) kuwakomoa wanafunzi |
| 9. Kuchunguza mabaki ya watu wa kale | (d) kupata maadili mema |
| 10. Kudadisi kwa kutumia mazingira | (e) kukuza udadisi |
| | (f) kupata umahiri |
| | (g) kuthibitisha ukweli wa nadharia |

**C:** *Andika* ***Kweli*** *kwa sentensi iliyo sahihi na* ***Si Kweli*** *kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

11. Kusoma kwa ratiba huongeza ufanisi katika kujifunza.________
12. Kujifunza na watu wengine hujenga kumbukumbu ya muda mrefu. ________
13. Nadharia ni wazo linalotumika kuthibitisha ukweli wa jambo fulani.___
14. Unaweza kuthibitisha ukweli wa dhana kwa kuuliza wenzako.________
15. Kujenga tabia ya uvumilivu hutokana na kutoshirikiana na wengine.________

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Hawilisha | hamisha maarifa kutoka kwa mtu anayejua kwenda kwa mwingine asiyejua |
| Zama | kipindi fulani cha wakati katika maisha |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Kuaminika katika jamii

**Utangulizi**

*Katika sura hii, utajifunza kutathmini utekelezaji wa wajibu wako na kujiepusha na vitendo vinavyosababisha kutoaminika katika jamii au vyenye kuharibu uhusiano mzuri baina ya watu. Umahiri huu utakuwezesha kutenda matendo ya kuaminika katika kujenga uhusiano mwema na wenzako. Pia, utaweza kutathmini utekelezaji wa wajibu wako na kuhamasisha wenzako kutenda matendo mema katika jamii.*

### Kutathmini utekelezaji wa wajibu wako

Wajibu ni jambo linalomlazimu mtu kulitimiza. Mfano, ni wajibu wa kila mwanafunzi kusoma kwa bidii. Hivyo, ni muhimu kwa mwanafunzi kutathmini wajibu wake shuleni na nyumbani.

### Kufanya kazi kwa bidii kwa faida yako na jamii inayokuzunguka

Unapaswa kufanya kazi kwa bidii, hasa ya kujisomea na nyingine unazopewa shuleni na nyumbani.

*Chunguza vitendo hivi, kisha jibu maswali yanayofuata*

(a) Mwanafunzi amekamilisha kazi aliyopewa na mwalimu kwa wakati.

(b) Mwanafunzi amejiwekea utaratibu wa kujisomea nyumbani na kuufuata.

(c) Mwanafunzi anajitolea kupanga madawati darasani kabla ya vipindi vya masomo kuanza.

(d) Mwanafunzi anakamilisha mapema usafi wa eneo alilopangiwa kabla ya kwenda kwenye paredi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 154 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Unajifunza nini kutokana na vitendo hivi?
2. Ni vitendo gani kati ya hivyo unaweza kuvitenda?
3. Ni vitendo gani vingine tofauti na hivyo utakavyovifanya shuleni?

## Kazi ya kufanya namba 1

Andika katika daftari lako la mazoezi faida tano anazoweza kuzipata mtu mwenye bidii ya kufanya kazi.

### Kutekeleza majukumu unayopewa nyumbani na shuleni

Wanafunzi wawapo nyumbani hutekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni kuamka mapema asubuhi na kufanya usafi wa chumba cha kulala, kuosha vyombo na kufanya usafi wa mazingira ya ndani na nje ya nyumba. Majukumu mengine ni kulisha mifugo na kumwagilia bustani za mboga au maua. Pamoja na kutimiza majukumu haya watoto waheshimu maagizo mengine ya nyumbani yanayopangwa na wazazi au walezi na wawaheshimu watu wote wakubwa na wadogo.

Pia wanafunzi wana majukumu mbalimbali wanayopewa wawapo shuleni. Baadhi ya majukumu hayo ni:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za masomo kwa kuhudhuria masomo darasani na kufanya mazoezi yote yanayotolewa;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za shuleni mfano, michezo na usafi wa mazingira; na

(c) Kulinda na kutunza mali za shule.

Baadhi ya wanafunzi huchaguliwa kuwa viranja wa shule. Kila kiranja ana majukumu mbalimbali ya kutekeleza. Mfano, baadhi ya majukumu ya kiranja wa mazingira ni:

(a) Kupanga maeneo ya wanafunzi kufanya usafi wa mazingira ya shule;

(b) Kusimamia usafi wa mazingira ya shule;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kuandika majina ya wanafunzi wanaofanya usafi vizuri na kuyabandika katika mbao za matangazo;
(d) Kuhamasisha wanafunzi wote kupenda kufanya usafi wa mazingira ya shule;
(e) Kushirikiana na wanafunzi wengine kufanya usafi wa mazingira ya shule; na
(f) Kupanga utaratibu wa kuwapongeza wanafunzi au darasa linaloongoza kwa kufanya usafi vizuri.

Vilevile baadhi ya wanafunzi huchaguliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa shule kupitia baraza la wanafunzi. Wanafunzi wanaoshiriki katika utawala wanapaswa kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Kuwasilisha maoni na mahitaji ya wanafunzi wote,wakiwemo wale wenye mahitaji maalumu kwa utawala wa shule;
(b) Kupanga na kusimamia mipango ya shule na matumizi ya fedha; na
(c) Kusambaza taarifa kati ya wanafunzi, uongozi wa shule na jamii inayozunguka shule.

Mwongozo kuhusu majukumu ya wanafunzi katika utawala wa shule unawapa wanafunzi haki yakusikilizwa na fursa ya kushauri namna bora ya kuboresha shule. Vilevile, wanafunzi wanatarajiwa kuwajibika, kufikiri, na kutenda haki. Ni muhimu kutekeleza majukumu ya shuleni na nyumbani, kushindwa kutekeleza majukumu haya vyema kunaweza kuathiri ujifunzaji wako na wa wanafunzi wengine.

## Zoezi la 2

1. Je, ni majukumu yapi unayoyatekeleza kabla ya kwenda shuleni au katika siku zisizo za masomo?
2. Je, ni majukumu gani unayoyatekeleza uwapo shuleni?
3. Taja jukumu moja la wanafunzi wanaochaguliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa shule.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 156 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya namba 2

Andika katika daftari lako la mazoezi jukumu ulilowahi kulitekeleza kwa kujituma, kisha bainisha faida ulizozipata kwa kujituma huko.

### Kutathmini tabia na mwenendo wako na kufanya mabadiliko

Ni muhimu kufanya tathmini ya tabia na mwenendo wako katika maisha ya kila siku. Tathmini hii itakusaidia kujielewa na kuchukua hatua stahiki iwapo kuna mabadiliko hasi katika mwenendo wa maisha yako. Mfano, unaweza kufanya tathmini ya maendeleo yako ya masomo. Tathmini ya aina hii inaweza kufanywa kila baada ya kukamilika kwa muhula wa masomo. Fanya tathmini kuangalia kiwango chako cha ufaulu katika kila somo. Linganisha ufaulu wa muhula husika na muhula uliopita au linganisha ufaulu wako na ule wa wanafunzi wenzako. Tathmini hii itakuwezesha kujua iwapo unafanya vyema katika masomo yako au la! Iwapo matokeo ya tathmini hii yataonesha kuwa hufanyi vizuri katika masomo yako, unashauriwa kuonana na mtu atakayekushauri juu ya mbinu zinazoweza kutumika kukuwezesha kufanya vyema katika masomo. Watu wanaoweza kukushauri ni kama vile; mwalimu wako wa somo, mwalimu wa darasa, wanafunzi wenzako wanaofanya vizuri shuleni au darasani kwako na wazazi au walezi. Baadhi ya njia zinazoweza kusaidia kukuwezesha kufanya vizuri katika masomo ni pamoja na kuongeza bidii katika kujisomea, kupanga na kufuata ratiba itakayoonesha utaratibu wa kujisomea na kutumia muda wako vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 3

1. Kuna faida gani ya kufanya tathmini ya tabia na mwenendo wako?
2. Ni mambo gani mengine mawili yatakayokujengea tabia ya kupenda kujisomea?
3. Utamshauri nini mwanafunzi mwenzako asiyefanya vizuri katika masomo yake?
4. Taja makundi matatu ya watu wanaoweza kukupa ushauri iwapo utaona mabadiliko hasi katika mwenendo wa maisha yako.



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 157 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 3

Andika katika daftari lako la mazoezi faida tano za kuwa na ratiba ya kujisomea nyumbani.

### Kujiepusha na vitendo vyenye kuharibu uhusiano baina ya watu

Uhusiano katika makundi ya watu huweza kuharibika kutokana na baadhi ya watu kukosa uvumilivu. Kila mmoja anapaswa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuharibu uhusiano wake na watu wengine katika jamii.

**Kubaini matendo yenye kuharibu uhusiano baina ya watu**

Maendeleo ya familia, jamii au nchi fulani hubainishwa kupitia mambo mbalimbali ikiwemo kiwango cha uhusiano mzuri katika familia, jamii au nchi husika. Jamii yenye migogoro hutumia muda mwingi kusuluhisha migogoro na kukosa muda wa kutosha wa kushiriki katika shughuli za maendeleo. Hivyo, ni vyema jamii ikabaini matendo yanayoweza kuharibu uhusiano na kuwa na njia madhubuti ya kuyaepuka. Baadhi ya matendo hayo na namna ya kukabiliana nayo ni kama ifuatavyo:

***Ulevi wa kupindukia, uvutaji bangi, wizi, ugomvi na utapeli:*** Ulevi wa kupindukia unaweza kusababisha ugomvi ambao mara nyingine madhara yake yanaweza kuwa makubwa mpaka kusababisha vifo. Jamii ielimishwe juu ya madhara ya unywaji wa pombe wa kupindukia. Vilevile, tatizo la ulevi wa kupindukia linaweza kudhibitiwa kwa kuweka muda maalumu wa kufungua na kufunga baa na vilabu vyote vya vileo. Katika sehemu nyingi za Tanzania, baa na vilabu hufunguliwa saa kumi alasiri na kufungwa saa sita usiku. Kufanya hivi husaidia kuzuia watu kunywa na kulewa wakati wa muda wa kazi.

Aidha, vitendo hivi vyaweza kudhibitiwa kwa kuwa na juhudi za dhati za kujenga jamii yenye maadili kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuwahimiza wazazi au walezi kuwalea watoto wao katika maadili mema. Wazazi wanapaswa kuwaelekeza watoto wao kutokujihusisha na vitendo vya kuvuta bangi, wizi, utapeli na vitendo vingine visiyo na maadili mema. Katika ngazi ya mtaa au kijiji tatizo hili linaweza kushughulikiwa kwa kuwa na mikutano ya hadhara ya mara kwa mara ya kukubaliana kwa pamoja juu ya mbinu za kupambana na vitendo hivi. Vilevile, kijiji au mtaa unaweza kuanzisha ulinzi shirikishi au

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 158 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuwa na kikosi cha sungusungu kwa ajili ya kusaidia kuhakikisha ulinzi na usalama wa watu na mali zao.

***Migogoro au ukosefu wa rasilimali muhimu katika jamii:*** Migogoro au ukosefu wa rasilimali muhimu katika jamii inaweza kusababisha uhusiano mbaya baina ya watu. Mfano, upungufu mkubwa wa rasilimali maji katika kijiji au mtaa husababisha watu kugombania maji machache yaliyopo. Vilevile, migogoro ya rasilimali ardhi husababisha uhusiano mbaya baina ya watu. Mfano, migogoro kati ya wafugaji na wakulima juu ya sehemu za kulima na kuchungia mifugo. Viongozi wa serikali ya kijiji au mitaa wahakikishe kuwa rasilimali muhimu zinapatikana kwa wananchi wote. Aidha, migogoro ya rasilimali ardhi inaweza kutatuliwa kwa mazungumzo yenye lengo la kukubaliana kwa pamoja maeneo ya shughuli za kilimo na kuchungia mifugo.

***Migogoro ya kisiasa:*** Migogoro ya kisiasa inaweza kusababisha uhusiano mbaya. Wananchi waelimishe kufanya siasa za kistaarabu zisizo na chuki.

## Zoezi la 4

1. Serikali ya kijiji au mtaa inawajibu gani katika kutatua migogoro ya upatikanaji wa rasilimali kwa wananchi wake?
2. Elezea njia moja inayoweza kutumika kuthibiti tatizo la migogoro ya rasilimali ardhi.
3. Je, hatua gani zinaweza kuchukuliwa kukabiliana na vitendo vya ulevi wa kupindukia, uvutaji bangi na wizi?

## Kazi ya kufanya namba 4

Eleza kwa kifupi chanzo cha vitendo vinavyoharibu uhusiano katika jamii unamoishi. Andika chanzo cha vitendo hivyo katika daftari lako la mazoezi.

### Njia za kujenga uhusiano mwema baina yako na watu wengine

Uhusiano mwema katika jamii ni jambo la kutilia mkazo ili kuishi kwa amani na kuweza kusaidiana katika maisha. Uhusiano mwema hujengwa kwa njia mbalimbali. Baadhi ya njia hizo ni:



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 159 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Kuwa mkweli, mwaminifu na kuwaheshimu watu wanaokuzunguka;

(b) Kutii sheria na taratibu;

(c) Kumcha Mungu na kufuata maelekezo ya viongozi wetu wa dini; na

(d) Upendo kwa watu wote.

## Zoezi la 5

1. Taja njia tatu zinazoweza kujenga uhusiano mwema katika jamii.
2. Taja faida ya kuwa na uhusiano mwema katika jamii.
3. Taja faida ya kuwa mwaminifu na kuwaheshimu watu wanaokuzunguka.

## Kazi ya kufanya namba 5



Jadiliana na wenzako njia zinazoweza kutumika kujiepusha na vitendo vinavyoharibu uhusiano wa watu katika jamii unamoishi. Andika njia hizo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 6

**A:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

1. Lipi kati ya yafuatayo si wajibu wa mtoto?
   (a) kuwasaidia wazazi shughuli za nyumbani
   (b) kuwasaidia wadogo wake
   (c) kulipa karo ya shule
   (d) kufua nguo zake

2. Kufanya kazi kwa bidii kuna faida nyingi. Lipi kati ya yafuatayo si mojawapo ya faida hizo?
   (a) kuongeza kipato cha familia
   (b) kuchoka kutokana na kazi nyingi
   (c) kuheshimika katika jamii
   (d) kuburudika kimwili na kiakili

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Lipi kati ya matendo yafuatayo huharibu uhusiano wa watu?
   (a) kuwa mkweli na mwaminifu
   (b) kuwaheshimu watu wanaokuzunguka
   (c) kutosaidia jirani wakati wa shida
   (d) kuwajali watu wengine

4. Lipi kati ya majukumu yafuatayo si jukumu la mwanafunzi awapo shuleni?
   (a) kupika chakula cha wanafunzi wenzake
   (b) kufanya usafi darasani
   (c) kuhudhuria paredi
   (d) kufanya bidii masomoni

5. Kipi kati ya vifuatavyo ni kitendo kinachoharibu uhusiano baina ya watu?
   (a) kutothamini wengine
   (b) kuwaonya wengine
   (c) kufanya kazi kwa bidii
   (d) kusema ukweli

**B:** *Katika jedwali lifuatalo, oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na kipengele kutoka **Sehemu B**, kisha, andika herufi ya jibu sahihi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| ***Vitendo vya kujituma*** | ***Faida za kujituma*** |
| 6. Kuhudhuria masomo | (a) kuonesha upendo |
| 7. Kumsaidia mwanafunzi mwenye ulemavu | (b) kudhihirisha uadilifu |
| 8. Kujifunza kazi za mikono | (c) usafi wa mazingira |
| 9. Kutoa taarifa ya uhalifu ulioshuhudia wewe | (d) kuongeza ufaulu |
| 10. Kujiunga na klabu ya mazingira | (e) kujipendekeza |
| | (f) kuwa mjasiriamali |
| | (g) kuwa mchezaji bora |

**C:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

11. Unaweza kubadili mwenendo mbaya kuwa mzuri utakapoweza kujitathmini.
____________

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 161 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

12. Ili kutoharibu uhusiano wa watu inakupasa kuwa na upendo.______
13. Ili kupata mahitaji muhimu ya maisha si lazima kufanya kazi kwa bidii.________
14. Majukumu ya nyumbani na ya shuleni hayatofautiani.________
15. Tunaweza kumsaidia mtu mwenye tabia ya ugomvi kwa kumtenga.________

**Msamiati**

| | |
|---|---|
| Mwenendo | mazoea ya mtu katika matendo yake |
| Rasilimali | vitu muhimu na vya thamani vinavyomilikiwa na nchi |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 162 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tano

## Kusimamia haki za binadamu

**Utangulizi**

*Katika sura hii, utajifunza kuainisha mila na desturi zinazokiuka haki za binadamu, madhara ya rushwa katika kusimamia haki za binadamu na kushirikiana na vikundi vya kijamii kutetea haki za binadamu. Umahiri huu utakuwezesha kuheshimu na kutetea haki za wenzako, kukemea mila na desturi zinazokiuka haki za binadamu. Pia, utaweza kushirikiana na jamii kukemea vitendo vinavyokiuka haki za binadamu.*

### Maana ya haki za binadamu

Haki za binadamu ni haki za msingi na uhuru ambao kila binadamu anastahili kupewa tangu kuzaliwa hadi kifo kwa sababu ya ubinadamu wake. Haki hizi zinatumika kwa binadamu wote bila kujali taifa, umri, rangi, kabila, cheo, tabaka, jinsi au dini. Haki za binadamu zimeorodheshwa katika Azimio la Kimataifa juu ya haki za binadamu ambalo hujulikana pia kama tangazo la kiulimwengu la haki za binadamu lililotolewa na Umoja wa Mataifa mwaka 1948. Haki zilizomo katika tangazo hili zimekubaliwa na kila taifa lililojiunga na Umoja wa Mataifa. Baadhi ya haki za binadamu ni pamoja na haki ya kuishi, kupata elimu, kushiriki katika uongozi, kumiliki mali, kutoteswa na kudhalilishwa, utaifa na kusikilizwa na mahakama huru inayozingatia sheria na usawa kwa wote. Haki za binadamu zinapaswa kuheshimiwa, kulindwa na kutekelezwa ipasavyo bila kukiukwa na mtu au taasisi yoyote.

### Mila na desturi zinazokiuka haki za binadamu

Mila na desturi zinaweza kutafsiriwa kama mitindo ya maisha ambayo jamii hurithishana kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa ujumla, mila na desturi huunda utamaduni wa jamii na kuwa utambulisho wao. Nchini Tanzania, kuna mila na desturi mbalimbali ambazo hubeba utambulisho wa jamii zetu. Licha ya umuhimu wake, pia zina madhara yake katika jamii. Baadhi ya mila na desturi zinakiuka haki za binadamu ni; watoto wa kike kuozwa katika umri



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 163 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mdogo, ubaguzi wa kijinsia katika kupata elimu, kurithi wajane, wanawake kukosa haki ya kumiliki mali, wanawake kubaguliwa katika nafasi mbalimbali za maamuzi na ukeketaji.

**Madhara ya ukeketaji kwa wanawake**

Ukeketaji hufanywa na mtu ajulikanaye kama ngariba. Mara nyingi ngariba huteuliwa na jamii kulingana na imani zao na uzoefu wa mtu huyo katika shughuli hiyo. Ukeketaji wa wasichana na watoto kuolewa katika umri mdogo ni ukiukaji wa haki za binadamu.

Baadhi ya madhara ya ukeketaji kwa wanawake ni kama yafuatavyo:

(a) Mshtuko, maumivu na uharibifu wa mwili;

(b) Kutokwa na damu nyingi;

(c) Maambukizi ya maradhi mbalimbali ikiwemo UKIMWI;

(d) Kupata matatizo wakati wa kujifungua; na

(e) Kifo.

**Sababu za ndoa za utotoni**

Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inawaruhusu wasichana waolewe wakiwa na umri wa miaka 14 wakati wavulana wanaruhusiwa kuoa wakiwa na angalau miaka 18. Kutokana na mila na desturi potofu, wasichana wengi wanaelekezwa kuolewa na kuzaa katika umri mdogo kupitia mafunzo ya unyago. Ndoa za utotoni husababishwa na:

(a) Umaskini;

(b) Mila na desturi potofu;

(c) Mafunzo ya unyago katika umri mdogo;

(d) Kupata mahari;

(e) Kupunguza gharama mbalimbali ndani ya familia;

(f) Ngoma za kienyeji zinazowajumuisha watoto katika mazingira hatarishi;

(g) Elimu duni kuhusu afya ya uzazi; na

(h) Aibu kwa familia kama msichana atapata mimba kabla ya kuolewa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Madhara ya ndoa za utotoni**

Yapo madhara mbalimbali yatokanayo na ndoa za utotoni. Baadhi ya madhara hayo ni kama yafuatavyo:


(a) Huongeza kiwango cha vifo kwa mama na mtoto;
(b) Maambukizi ya UKIMWI;
(c) Hakuna msaada kwa wasichana walioathiriwa na ndoa za umri mdogo kwa sababu wengi wao hutengwa;
(d) Ukosefu wa elimu hususan kutojua kusoma hupunguza uwezo wa kupata elimu ya uzazi;
(e) Kushindwa kulea mtoto kutokana na kukosa uwezo wa kukidhi mahitaji yake ya msingi; na
(f) Umaskini.

Kutokana na madhara ya mila potofu ni vyema jamii ikaelimishwa kushiriki kupinga mila na desturi zote zinazokiuka haki za binadamu katika jamii yetu.

## Zoezi la 1

1. Orodhesha mila na desturi zinazokiuka haki za binadamu katika jamii unamoishi.
2. Taja madhara yatokanayo na ukeketaji kwa wanawake.
3. Je, ni sababu zipi zinazosababisha ndoa za utotoni?

## Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wenzako ili kubainisha mbinu mtakazotumia kupinga mila na desturi zinazokiuka haki za binadamu katika maeneo mnayoishi. Andika mbinu hizo katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Madhara ya rushwa katika kusimamia haki za binadamu

Rushwa ikishamiri katika jamii husababisha madhara mengi ambayo uhatarisha uhai wa taifa. Baadhi ya madhara hayo ni:



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 165 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kukosekana kwa huduma muhimu na bora katika jamii**: Rushwa husababisha ukiritimba katika sekta za huduma za jamii kama vile, elimu, afya, maji na miundombinu. Kukosekana kwa huduma hizi ni kutokana na fedha nyingi kuishia katika mifuko ya wala rushwa. Hivyo, Serikali kushindwa kutimiza wajibu wake wa kutoa huduma hizo kwa jamii na kuchangia kutokea kwa migogoro kutokana na jamii kugombea huduma chache, hivyo kutoa mwanya kwa baadhi ya wananchi wasio waadilifu kutoa rushwa kupata huduma hizo na wananchi wengine kukosa huduma hizo muhimu. Kwa mfano, sekta ya elimu, kukosa fedha za kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kujenga madarasa na maabara za mafunzo kwa vitendo, kushindwa kuajiri walimu na kuwalipa kwa wakati. Sekta ya afya, kushindwa kujenga vituo vya afya na kutoa huduma za kitabibu kutokana na ukosefu wa fedha. Serikali kushindwa kujenga miundombinu ya mawasiliano na usafirishaji. Kwa mfano, Baadhi ya kandarasi za ujenzi kutolewa kwa upendeleo kwa makampuni yasiyo na uwezo kutokana na baadhi ya wakandarasi kutoa rushwa ili washinde zabuni. Hali hii husababisha miundombinu iliyo chini ya kiwango, hivyo kuisababishia serikali hasara na jamii kushindwa kunufaika na huduma hiyo muhimu kama ilivyokusudiwa.

**Kuongezeka kwa magonjwa ya kuambukiza:** Rushwa inapokithiri husababisha ongezeko la magonjwa yanayoambukiza kwa sababu muuguzi anaweza kupewa fedha kubadilisha majibu ya mgonjwa ili kuficha ukweli wa jambo au pale mtu anapoomba rushwa ya ngono ili aweze kutoa upendeleo wa jambo fulani.

**Kupata wataalamu wasio na sifa:** Rushwa inasababisha mtu asiye na sifa kwenye taaluma fulani kutoa hongo ili aongezewe alama za bure zitakazo msaidia kuhitimu masomo yake lakini hana sifa za taaluma hiyo.

**Kuongezeka kwa maovu katika jamii:** Rushwa husababisha kuongezeka kwa maovu pale sheria, taratibu na kanuni zinapokuwa hazifuatwi. Kwa mfano, baadhi ya polisi wanapomwachia mwizi au mhalifu hii husababisha vitendo viovu viendelea na wananchi kuchukua sheria mkononi.

**Uchaguzi wa viongozi wasio waadilifu:** Vitendo vya rushwa katika uchaguzi husababisha kupata viongozi wasiokuwa waadilifu na sifa zinazostahili. Utoaji wa rushwa husababisha wananchi kushawishika kuchagua viongozi wasio na sifa, viongozi hawa wanapochaguliwa wanaishia kusimamia maslahi yao binafsi badala ya kusimamia maslahi ya waliowachagua au taifa kwa ujumla ili kurudisha fedha aliyotoa kama rushwa.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 166 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kukosekana kwa haki:** Rushwa husababisha vyombo vyenye dhamana ya kutoa haki kushindwa kutoa haki au mwenye haki kununua haki yake au asiye na haki kupata upendeleo na kupewa haki.

**Kuongezeka kwa matabaka:** Rushwa uchochea kuongezeka kwa pengo kati ya wenye nacho na wasio nacho (matabaka kwa misingi ya kipato).

**Gharama za vitu na huduma kupanda:** Rushwa inasabisha gharama za maisha kupanda kwa kuwa watu wanafidia gharama walizotoa kama rushwa.

**Kuongeza Migogoro:** Rushwa inasababisha migogoro isiyoisha na kutokuwa na maelewano kati mtu na mtu, mtu na jamii.

**Vifo:** Vifo huweza kutokea iwapo daktari, muuguzi au mhudumu wa hospitali atashindwa kutoa huduma stahiki kwa mgonjwa mpaka apewe rushwa. Vilevile, vifo huweza kusababishwa na baadhi ya madereva kutoa rushwa na kuruhusiwa kuendesha magari mabovu. Magari haya yanaweza kupata ajali na kusababisha vifo kwa wananchi, hivyo kupotea kwa nguvukazi ya taifa.


**Mimba zisizotarajiwa:** Vitendo vya rushwa husababisha mimba zisizotarajiwa katika jamii.

Pamoja na rushwa kuwa na madhara mengi katika jamii, pia huathiri utekelezaji wa majukumu ya serikali kwa kuwa husababisha pato la taifa kupungua.

## Zoezi la 2

1. Eleza madhara matano ya rushwa.
2. Kwa nini tunasema kuwa rushwa ni adui wa haki na maendeleo?
3. Je, kuna madhara gani mhalifu anapoachiwa?

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wanafunzi wenzako ili kubaini jinsi rushwa inavyochangia ukiukaji wa haki za binadamu katika maeneo mnayoishi. Andika majadiliano hayo katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 167 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kushirikiana na vikundi vya kijamii kutetea haki za binadamu

Jamii yenye ushirikiano na mshikamano hujali na kutetea haki za binadamu. Ni muhimu kushirikiana na watu au mashirika mengine ili kuleta ufanisi katika kudai haki za binadamu katika jamii. Mojawapo ya njia ya kutetea haki za binadamu ni kuunda vikundi vya kijamii. Vikundi hivi huundwa baada ya kuwapatia baadhi ya wanajamii mafunzo kuhusu haki za binadamu kupitia semina au makongamano kwa lengo la kuwajengea uwezo. Pia, vikundi hivi huweza kushirikiana na asasi za kijamii zilizopo karibu na maeneo wanamoishi katika kuelimisha jamii kwa kuandaa semina na machapisho mbalimbali ya haki za binadamu.

### Kutathmini hali ya utekelezaji wa haki za binadamu katika jamii unamoishi

Jamii yenye kutekeleza haki za binadamu huweza kupimwa kutokana na kuwepo kwa vitendo vinavyoonesha hali ya kujali utu na haki za watu katika shughuli mbalimbali za kijamii. Vitendo vinavyoonesha utekelezaji wa haki za binadamu ni kutolewa kwa huduma za jamii kwa haki kama vile huduma ya maji safi, hospitali zenye kutoa huduma bora za afya, shule zenye kutoa elimu bora kwa maana ya mazingira mazuri ya kujifunzia na vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia, ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano kama barabara na simu. Huduma hizi zinapaswa kutolewa bila kuwepo kwa upendeleo kwa mujibu wa hadhi, rangi, kabila au uwezo wa kiuchumi wa mtu.

Kipimo kingine ni kuwepo kwa utawala bora katika kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kama vile jamii kushirikishwa katika maamuzi yanayohusu maendeleo yao, kuchagua viongozi wao, kuwa huru kutoa maoni yao katika masuala mbalimbali ya kijamii bila kuvunja sheria, kanuni na taratibu.

Halikadhalika, kutokuwepo kwa vitendo vya ukandamizaji na unyanyasaji watu kwa mfano, watu kufungwa au kuteswa bila sababu na aina nyingine za uonevu katika jamii.

Pia, uwepo wa ulinzi na usalama pamoja na kusikilizwa kwa mashauri mbalimbali katika jamii tunamoishi, ni sehemu ya utekelezwaji wa haki za binadamu. Hivyo, utekelezwaji wa haki za binadamu ni jambo la kuzingatia ili kujenga jamii yenye utu, uadilifu na ustawi.

FOR ONLINE USE ONLY




URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 168 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Kuna huduma gani zinazoonesha utekelezwaji wa haki za binadamu katika jamii unamoishi?
2. Taja madhara yatokanayo na ukiukwaji wa haki za binadamu katika jamii unamoishi.
3. Taja njia mojawapo inayoweza kutumika katika kutetea haki za binadamu katika jamii unamoishi.

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wenzako kwa kubainisha vitendo vya haki za binadamu vinavyotekelezwa katika shule yako. Andika vitendo hivyo katika daftari lako la mazoezi.

### Vyombo vyenye mamlaka ya kudai na kutetea haki za binadamu

Haki za binadamu ni lazima zilindwe kikatiba na kisheria ili kuleta hali bora kwa watu kwenye jamii. Ili haki za binadamu ziweze kuzingatiwa kikamilifu ni lazima pawepo na vyombo vyenye mamlaka ya kudai na kutetea haki za binadamu. Vyombo hivyo ni pamoja na Katiba ya nchi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Tume ya Haki za Binadamu, Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania, Mtandao wa Jinsia Tanzania, Vyama vya Watu Wenye Mahitaji Maalumu, na Vyombo vya Habari. Vyombo hivi hufanya kazi mbalimbali katika kudai na kutetea haki za binadamu. Kazi za vyombo hivi ni kama zifuatazo:

**Katiba ya nchi:** Katiba ya nchi imeainisha haki anazostahili kupata mtu katika Ibara ya 12 hadi 24. Haki hizo ni; haki ya kutoa mawazo, haki ya kuishi, haki ya kuwa huru na haki ya kuabudu dini anayoipenda. Serikali na taasisi zake zina wajibu wa kuzilinda na kuzitekeleza haki hizi kikamilifu kwa mujibu wa sheria. Hivyo, kuwepo kwa katiba kunasaidia kuidhibiti serikali, taasisi au watu binafsi kuzingatia haki za binadamu wakati wote.

**Mahakama:** Kazi kubwa za chombo hiki, kulinda na kutetea haki za binadamu. kutafsiri katiba ya nchi na orodha ya haki za binadamu, kutafsiri sheria

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mbalimbali zinazohusu haki za binadamu na kutumia tafsiri hizo kulinda haki za binadamu, na kutoa haki bila woga wala upendeleo.

**Bunge la Tanzania:** Bunge hutunga sheria mbalimbali za kutetea haki za binadamu. Vilevile ni chombo cha wawakilishi wa wananchi ambacho hujadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu katika jamii na kutafutia ufumbuzi. Pia, Bunge linaweza kuunda tume kuchunguza matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu, kujadili taarifa na kutoa maazimio yanayolinda haki za binadamu.

**Tume ya Haki za Binadamu:** Tume hii ina majukumu mbalimbali kuhusu haki za binadamu. Majukumu hayo ni kukuza juhudi za kutetea haki za binadamu nchini, kupokea na kuchunguza malalamiko dhidi ya uvunjwaji wa haki za binadamu. Majukumu mengine ni kufanya utafiti juu ya hali ya haki za binadamu nchini na kupeleka mashauri mahakamani, kuchunguza malalamiko ya watu au taasisi yoyote juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu. Pia, huwezesha nchi kuridhia mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu na kuwezesha kuwepo uwiano wa sheria za nchi na sheria za kimataifa za haki za binadamu.

**Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa:** Hiki ni chombo mahususi cha kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Hulinda haki za binadamu zisikiukwe katika utoaji huduma kama vile mahakamani, hospitalini, taasisi za elimu na sehemu nyingine nyingi.

**Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania:** Chama hiki kinatetea haki za binadamu kwa wanawake katika jamii.

**Mtandao wa Jinsia Tanzania:** Mtandao huu hujishughulisha kupigania usawa wa haki za binadamu kwa wanawake na wanaume.

**Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania:** Chama hiki huwapatia wanawake na watoto usaidizi na ushauri wa kisheria wanapodhulumiwa, kunyanyaswa na kunyimwa haki zao.

**Vyama vya Watu Wenye Mahitaji Maalumu:** Vyama hivi hutetea haki za watu wenye mahitaji maalumu. Vyama hivi hudai na kutetea haki za watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kwa mfano, haki za msingi kulingana na ulemavu walionao, haki ya uwakilishi katika vyombo vya maamuzi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 170 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Vyombo vya Habari:** Vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kutoa habari na kufichua vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu. Habari hizo husaidia wahusika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

## Zoezi la 4

1. Taja vyombo vitano vinavyodai na kutetea haki za binadamu hapa nchini.
2. Taja wajibu wa Tume ya Haki za Binadamu.
3. Taja njia nne utakazotumia kuhamasisha utekelezaji wa haki za binadamu katika jamii unamoishi.

## Kazi ya kufanya namba 4

Chunguza taarifa za vyombo vya habari kama vile magazeti, redio na runinga, kisha bainisha mchango wake katika kudai na kutetea haki za binadamu nchini. Andika matokeo ya uchunguzi huo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 5

**A:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

1. Haki za binadamu zipo kwa ajili ya watu wazima tu.________
2. Mojawapo ya kazi za vyombo vya kutetea haki za binadamu ni kudai haki kwa watu wanaoonewa.________
3. Tume ya Haki za Binadamu ni chombo cha kiraia kinachopambana na kuzuia rushwa.________
4. Vikundi vya kutetea haki za binadamu vinaongozwa na Bunge.______
5. Mila potofu zinachangia uvunjwaji wa haki za binadamu.________

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 171 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B:** *Katika jedwali lifuatalo, oanisha kitendo kinachokiuka haki za binadamu kutoka **Sehemu A** na kipengele cha chombo au mkakati wa kutetea haki za binadamu kutoka **Sehemu B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako.*

| Sehemu A<br>***Vitendo vinavyokiuka haki za binadamu*** | Sehemu B<br>***Chombo au mkakati wa kutetea haki za binadamu*** |
|---|---|
| 6. Kupokea na kutoa rushwa | (a) Mtandao wa Jinsia Tanzania |
| 7. Kukeketa watoto wa kike | (b) kuzingatia utawala bora |
| 8. Kumuoza binti aliye chini ya miaka 14 | (c) elimu kwa umma |
| 9. Kutoa huduma kwa upendeleo | (d) afya bora |
| 10. Kutoshirikishwa kwenye maamuzi muhimu | (e) kuzingatia sheria |
| | (f) TAKUKURU |
| | (g) Bunge la Tanzania |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Ridhia | kubali au ruhusu jambo au kitu kifanyike |
| Kandarasi | kazi inayofanywa kwa makubaliano maalumu ya mkataba mfano, mkataba kwa ajili ya ujenzi |
| Ukiritimba | hali ya mtu mmoja, serikali moja au chama kimoja kujikusanyia madaraka ya kila kitu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Sita

## Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kuhusu ushirikiano baina ya mataifa, uhusiano wa kibalozi na jumuiya za kimataifa. Pia, ulijifunza faida na hasara za utandawazi. Katika sura hii, utajifunza umuhimu wa kudumisha uhusiano wa kiutamaduni, kibiashara na kimichezo kwa watu wenye asili ya mataifa tofauti. Vilevile, utajifunza jinsi ya kuishi na watu wa asili nyingine, na mikakati ya kukabiliana na madhara ya utandawazi. Umahiri huu utakuwezesha kujenga uhusiano katika nyanja za utamaduni, michezo na biashara na watu wa mataifa mengine. Vilevile, utakusaidia kufahamu njia za kudhibiti athari za utandawazi.*

### Umuhimu wa kudumisha uhusiano na watu wenye asili tofauti

Uhusiano baina ya watu ni hali ya kufahamiana na kutenda mambo kwa kushirikiana. Uhusiano unaweza kuwa wa kiutamaduni, kibiashara na kimichezo. Uhusiano baina ya mataifa mbalimbali ni muhimu sana na unafaa kudumishwa kwa sababu hukuza mshikamano, upendo na uelewano. Kudumisha uhusiano katika biashara, utamaduni na michezo kwa watu wenye asili tofauti husaidia katika kudumisha amani. Uhusiano wa aina hii hujenga upendo na mshikamano. Pia, hukuza mawasiliano na kujifunza tamaduni za mataifa au makabila mengine. Halikadhalika, huwapa watu nafasi ya kubadilishana ujuzi na uzoefu, fursa ya kujifunza mambo mapya na kubadilika au kuondokana na taratibu zisizofaa. Vilevile, huwawezesha watu kufaidi vipaji vya wengine na kudumisha udugu na urafiki.

Uhusiano wa kimataifa wa kibiashara, huhusisha watu wa taifa moja kufanya biashara na watu wa mataifa mengine. Uhusiano huu husaidia kuongeza pato la taifa na kupanua wigo wa biashara. Kwa upande mwingine, uhusiano wa kimichezo huhusisha watu wa mataifa mbalimbali kukutana kwa shughuli za michezo na burudani. Ushirikiano huo unaweza kuwa katika muundo au mfumo wa mchezaji wa nchi moja kwenda kushiriki michezo katika nchi nyingine

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 173 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

au timu ya nchi moja kwenda kucheza na timu ya nchi nyingine. Aidha, timu kutoka nchi mbalimbali zinakutana katika nchi moja kwa ajili ya mashindano ya michezo. Kitendo hiki hukuza vipaji vya wachezaji na kuitangaza nchi husika kwa nchi nyingine. Vilevile, uhusiano wa kiutamaduni ni ule ambao taifa moja huruhusu tamaduni zake kufahamika na kutumika na mataifa mengine. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili huweza kufundishwa na kuzungumzwa na Wachina, Wajapani, Wakorea, Wamarekani, Waingereza na watu wa mataifa mengine ambayo asili yao siyo Tanzania. Uhusiano huu husaidia kukuza biashara, michezo na utamaduni wa Kitanzania. Njia nyingine ya kukuza uhusiano wa kiutamaduni ni kutoa fursa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwenda kusoma katika nchi nyingine. Mifano mingine ya uhusiano wa kimataifa ni uhusiano wa kijeshi ili kulinda usalama na uhusiano wa kitaalamu katika kufanya utafiti.

### Tamaduni za watu wa asili nyingine

Utamaduni ni mfumo wa maisha ya watu na jinsi wanavyoishi na taratibu zao kijamii, kiuchumi na kisiasa. Tanzania ni moja kati ya nchi zinazosifika duniani kwa ukarimu, amani na upendo kwa wageni, licha ya kuwa na makabila zaidi ya mia moja na ishirini ambayo yote hutunza mila na desturi zao. Watanzania wanaishi kwa umoja, upendo na mshikamano. Hali hii huwavutia watu wa mataifa mengine na wengine hupenda kuishi Tanzania.

Wageni hawa hutoka katika jamii za nchi tofauti zikiwemo zile za Asia, Ulaya na Amerika. Pamoja na tofauti za lugha, vyakula, mavazi, shughuli za kiuchumi, michezo na burudani, tunapaswa kuishi pamoja kwa kuheshimiana kwa upendo na amani.

### Mitindo ya maisha inayofaa ili kuishi vizuri na watu wenye asili tofauti

Ni vyema kufahamu mila na desturi na asili za watu mbalimbali unaoishi nao. Hivyo, tunatakiwa kujifunza mitindo mbalimbali ya maisha yao. Tukishafahamu mitindo ya maisha yao ni vyema tukaiheshimu na kuijali. Tukifanya hivyo, tutaweza kujenga uhusiano mwema na kuishi kwa furaha katika jamii.

Inatupasa kuishi kwa upendo, kwa kuheshimiana, kwa kushirikiana, na kwa kufuata au kutii sheria za nchi husika.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 174 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

1. Je, umewahi kuishi na watu wenye asili tofauti na taifa lako?
2. Taja umuhimu wa kudumisha uhusiano na mataifa mengine.
3. Taja mambo yanayotambulisha asili yako kwa nchi nyingine.
4. Eleza umuhimu wa michezo katika uhusiano wa kimataifa.

## Kazi ya kufanya namba 1

Chagua makabila matano yaliyopo nchini Tanzania, kisha andika lugha, vyakula, na kazi za asili wanazofanya watu wa makabila hayo. Andika kazi hiyo katika daftari lako la mazoezi.

### Mikakati ya kukabiliana na madhara ya utandawazi

Licha ya faida zake, utandawazi una madhara mengi kwa maisha ya watu na mazingira ya nchi yetu. Baadhi ya madhara hayo ni kama vile biashara na bidhaa za nje kutawala soko la ndani, rushwa, mmomonyoko wa maadili, rasilimali za nchi kuchukuliwa na wageni, wageni kutawala soko la ajira, sera za mataifa yenye nguvu kutawala sera za ndani na uharibifu wa mazingira unaotokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu.

Inatupasa kuweka mikakati na kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na madhara ya utandawazi katika nchi yetu. Kuna njia nyingi za kukabiliana na madhara ya utandawazi, lakini hapa tutajadili baadhi kama ifuatavyo:

(a) Kukuza uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi ili kuepuka kutegemea bidhaa za nchi nyingine katika kuendesha maisha yetu. Tujiimarishe kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Umoja wa Afrika, kuzalisha bidhaa za kutosha katika nchi wanachama ili kupambana na athari za kutegemea bidhaa za mataifa tajiri;

(b) Kuwa na sauti moja katika kupinga sera kandamizi za utandawazi kutoka katika nchi tajiri dhidi ya nchi masikini;

(c) Kuboresha elimu ya taifa letu hususan katika mfumo na mazingira ya elimu ili kupata elimu bora yenye kiwango cha kusaidia nchi kupata wataalamu wa sekta zote. Hii itasaidia Watanzania kushindana na watu wa mataifa mengine katika soko huria la ajira na uchumi;



URAIA DARASA LA 6 Dummy Final.indd 175 2021/08/04 11:14

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kuanzisha na kuimarisha vikundi vya uzalishaji mali ili kuweka nguvu ya pamoja ya kukusanya mitaji na kuwekeza katika biashara;

(e) Kuungana pamoja kutokomeza rushwa na ufisadi katika nchi yetu. Tuwadhibiti viongozi wetu wasiandae mazingira ya kupewa na kutoa rushwa au kufanya ubadhirifu wa mali za umma kwa faida zao. Kuzuia na kupambana na rushwa na ufisadi katika nchi kutasaidia watu wengi kufaidi rasilimali za nchi yao;

(f) Kuwepo na uwiano wa kutumia rasilimali za nchi kama vile madini, ardhi, maji, na misitu kwa faida ya wananchi wote;

(g) Kuwawezesha Watanzania kupata mitaji au mikopo kutoka taasisi za fedha kwa riba nafuu ili iwe rahisi kwa wananchi wengi kuendeleza makampuni, viwanda na biashara binafsi;


(h) Sheria za uwekezaji zilenge kuwainua na kuwafaidisha wawekezaji wazawa bila kupendelea makampuni ya kigeni; na

(i) Sheria zinazohusu uwekezaji zilenge katika kuhifadhi mazingira na kulinda haki za wafanyakazi na haki za binadamu.

## Zoezi la 2

1. Eleza maana ya utandawazi.
2. Kwa nini ni muhimu kutunga sheria kudhibiti makampuni yanayo wekeza hapa nchini?
3. Taja njia tano za kukabiliana na athari za utandawazi nchini.

## Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wenzako kuhusu namna utandawazi unavyoweza kuathiri utamaduni wa nchi. Andika mambo mliyojadili katika daftari lako la mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**A:** *Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na kipengele kutoka **Sehemu B** ili kupata maana kamili, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika daftari lako la mazoezi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Utamaduni | (a) huwaunganisha watu wa tamaduni tofauti |
| 2. Elimu bora | (b) kukua kwa biashara, teknolojia ya habari na mawasiliano na kuongezeka kwa uhusiano baina ya watu |
| 3. Lugha | (c) kupinga rushwa na ufisadi katika jamii yetu |
| 4. Kusikilizana | (d) kumomonyoka kwa maadili |
| 5. Utandawazi | (e) husaidia nchi kupata wataalamu wa sekta mbalimbali |
| | (f) huepusha migogoro katika jamii |
| | (g) unajumuisha lugha, sanaa, mavazi, na imani |

**B:** *Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si kweli** kwa sentensi isiyo sahihi. Andika majibu katika daftari lako la mazoezi.*

6. Nchi zinazoshirikiana na Tanzania zina utamaduni unaofanana._____
7. Utaweza kuishi vyema na watu wa mataifa mengine utakapoiga mitindo ya maisha yao.______
8. Lugha, vyakula, mavazi na sanaa kwa pamoja vinaunda utamaduni.______
9. Uwajibikaji katika jamii unatokana na kukua kwa utandawazi.______
10. Tanzania ni nchi mojawapo inayosifika kwa ukarimu, amani na upendo.______

**C:** *Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika daftari lako la mazoezi.*

11. Uhusiano kati ya Tanzania na mataifa mengine ya kiafrika umekua kutokana na nini?
    (a) utandawazi
    (b) utunzaji wa mazingira
    (c) jumuiya zilizopo
    (d) uhusiano wa kimichezo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

12. Tanzania imefanya nini katika kujenga jamii inayoheshimu utamaduni wake?
    (a) kuwakinga raia wake na utandawazi
    (b) kufundisha lugha za asili
    (c) kuwa na vyombo vya kuendeleza utamaduni
    (d) kuzuia tamaduni zote za kigeni

13. Utawezaje kuishi vyema na watu wa jamii na asili tofauti?
    (a) kufahamu mila na desturi zao
    (b) kuheshimu utamaduni wao
    (c) kufahamu lugha zao
    (d) kuwafundisha utamaduni wetu

14. Upi si umuhimu wa kuendeleza uhusiano kati ya Tanzania na mataifa mengine?
    (a) kupata utaalamu na teknolojia
    (b) kudumisha utamaduni wa Mtanzania
    (c) kukuza migogoro kati ya nchi na nchi
    (d) kupata pesa za kigeni

15. Lugha ya Kiswahili imejenga uhusiano na mataifa mengine katika nyanja zifuatazo isipokuwa:
    (a) biashara za ndani na nje ya nchi
    (b) michezo ya kimataifa
    (c) utalii na utamaduni wa Kitanzania
    (d) kuharibu ushirikiano


FOR ONLINE USE ONLY


**Msamiati**


| | |
|---|---|
| Mikakati | mipango inayolenga matokeo fulani |
| Riba | faida au ziada anayopata mkopeshaji |
| Ufisadi | ubadhirifu au wizi wa mali alizokabidhiwa mtu |


## Vitabu vingine vya Darasa la Sita
## Taasisi ya Elimu Tanzania


### Darasa la Sita









ISBN 978-9987-09-335-9

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*